# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

**RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**FEBRUARI, 2025**

**YALIYOMO**

1. UTANGULIZI ....................................................................- 5 -

1.1 UTARATIBU NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI..............................- 6 -

1.2 MISWADA YA SHERIA ..........................................................- 7 -

1.3 MUUNDO WA KAMATI...........................................................- 8 -

1.4 HADIDU REJEA...................................................................- 8 -

SEHEMU YA PILI.....................................................................- 10 -

2. MAUDHUI YA RIPOTI YA KAMATI...........................................- 10 -

2.1 OFISI YA RAIS – IKULU.........................................................- 10 -

2.2 OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI.............................................- 12 -

2.3 TAASISI YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZANZIBAR.....................- 14 -

2.4 AFISI YA USALAMA WA SERIKALI (GSO)......................................- 16 -

2.5 MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR...............................- 18 -

2.6 TAASISI YA RAIS, UFUATILIAJI NA USIMAMIZI WA UTENDAJI SERIKALINI – ZANZIBAR (ZPDB).........................................................- 20 -

2.7 AFISI KUU – PEMBA.............................................................- 22 -

3. OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS ..................................- 23 -

4. OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA B L W....- 33 -

4.1 BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR.....................................- 34 -

4.2 TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR ..............................................- 36 -

4.3 KAMISHENI YA KUKABILIANA NA MAAFA....................................- 39 -

4.4 IDARA YA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA........................- 40 -

4.5 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)...................................- 41 -

4.6 OFISI YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ DODOMA.......................- 44 -

4.7 OFISI YA AFISA MDHAMINI PEMBA…..…………………………………..- 45 -

5. OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BOR…..- 46 -

5.1 MAHAKAMA KUU….……………………………………………………..- 48 -

5.2 AFISI YA MWANASHERIA MKUU………………………………………..- 52 -

5.3 AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA……………..…………………- 54 -

5.4 SKULI YA SHERIA ZANZIBAR…..……………………………………..- 56 -

5.5 IDARA YA KATIBA NA MSAADA WA KISHERIA……………………..- 58 -

5.6 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA ZANZIBAR……….- 59 -

5.7 OFISI YA MUFTI MKUU ZANZIBAR ……………………………….- 61 -

5.8 TUME YA UTUMISHI SERIKALINI………………………………….. - 63 -

5.9 CHUO CHA UTAWALA WA UMMA (IPA)…………………………… - 64 -

5.10 KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA ………………………………- 66 -

5.11 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR (ZAECA)………………………………………………………………………..- 67 -

5.12 TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA………………………..- 69 -

5.13 OFISI KUU – PEMBA ………………………………………………………- 71 -

6.OR, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ………………………………………………………………………………..- 72 -

6.1 JESHI LA KUJENGA UCHUMI *(JKU)* ZANZIBAR……………………..- 73 -

6.2 WAKALA WA ULINZI WA JESHI LA KUJENGA UCHUMI………..- 75 -

6.3 CHUO CHA MAFUNZO (MF) ZANZIBAR ……………………………..- 77 -

6.4 KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) ………………- 79 -

6.5 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU)…………………………..- 82 -

6.6 KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ)…...…………………………- 84 -

6.7 OFISI YA MKOA WA MJINI MAGHARIBI……………………………..- 86 -

6.8 BARAZA LA JIJI LA ZANZIBAR …………………………………………- 87 -

6.9 BARAZA LA MANISPAA MJINI .............................................- 89 -

6.10 BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI “A” ............................- 91 -

6.11 BARAZA LA MANISPAA YA MAGHARIBI “B”..............................- 92 -

6.12 OFISI YA MKOA WA KUSINI UNGUJA....................................- 94 -

6.13 BARAZA LA MJI KATI .......................................................- 96 -

6.14 HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA.......................- 97 -

6.15 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA................................- 100 -

6.16 BARAZA LA MANISPAA KASKAZINI “A” ..................................- 100 -

6.17 BARAZA LA MJI KASKAZINI “B” ............................................- 102 -

6.18 OFISI YA MKOA WA KUSINI PEMBA ....................................- 104 -

6.19 BARAZA LA MANISPAA CHAKE CHAKE....................................- 105 -

6.20 BARAZA LA MJI MKOANI – PEMBA ...................................- 107 -

6.21 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI PEMBA ............................- 109 -

6.22 BARAZA LA MJI WETE .......................................................- 110 -

6.23 HALMASHAURI WILAYA YA MICHEWENI ...........................- 112 -

6.24 AFISI YA MRAJIS WA JUMUIYA ZISIZO ZA KISERIKALI (NGO’s) ZANZIBAR.........................................................................- 114 -

6.25 WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR.......- 115 -

7.0 MAAGIZO YA JUMLA............................................................- 118 -

8.0 HITIMISHO ...........................................................................- 124 -

# SEHEMU YA KWANZA

---

## 1. UTANGULIZI

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambayo imeundwa na kupewa majukumu kwa mujibu wa kifungu cha *85* cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984* na Kanuni ya *119(1)* ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la mwaka *2024*.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 124(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2024 Kamati imepewa jukumu la kuwasilisha Ripoti ya shughuli zake mbele ya Baraza katika Mkutano wa Februari. Aidha, Ripoti hii inaakisi kazi zote za Kamati ambazo zimefanywa kuhusiana na utekelezaji wa Taasisi ambazo zipo chini yake kwa kipindi cha mwaka wa fedha, 2024/2025 na kwa kuzingatia Mipango mikuu ya Kitaifa ambayo inajumuisha Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 na Ilani ya Chama Chama Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 – 2025. Aidha, majukumu ya Kamati hii, yameelezwa katika *Jadweli la Kwanza* la Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar kama ifuatavyo:

(i) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa katika Baraza wakati wa uwasilishwaji wa Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza;
(ii) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika;
(iii) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;

(iv) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka;

(v) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;

(vi) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika;

(vii) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo;

(viii) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati hii ni ya Kisekta ambayo inasimamia utekelezaji wa majukumu ya wizara *Tano (5)* zifuatazo: -

*(a)* Ofisi ya Rais Ikulu

*(b)* Ofisi ya Makamu wa Kwanza Rais.

*(c)* Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

*(d)* Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. na

*(e)* Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum.

## 1.1 UTARATIBU NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Sehemu hii inaelezea utaratibu uliotumiwa na Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika utekelezaji wa kazi zake ambazo zilifanywa kwa mujibu wa Kanuni ya 122(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la mwaka 2024. Shughuli hizo ni pamoja na:

(a) Kupokea taarifa mbali mbali za kila robo mwaka (quarterly reports);

(b) Kupokea taarifa za utekelezaji wa malengo ya bajeti ya kila wizara;

(c) Utekelezaji wa maagizo ya kamati;

(d) Kukutana na wadau mbali mbali wa sekta zinazosimamiwa na kamati;

(e) Kukagua baadhi ya maeneo na miradi mbali mbali ya kimaendeleo inayosimamiwa na wizara zinazohusika ili kuona hatua za utekelezaji

changamoto hizo; na

(f) Kupitia miswada mbali mbali ya sheria ambayo iliwasilishwa mbele ya kamati katika kipindi chote hicho.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, kamati ilitekeleza kazi zake kwa kusimamia malengo yafuatayo:

*(a)* Kufuatilia maagizo yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka *2023/2024*;

*(b)* Kufuatilia ahadi za Serikali zilizotolewa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka wa fedha *2024/2025*;

*(c)* Kufuatilia utekelezaji wa Bajeti (kazi za kawaida na kazi za maendeleo) ya mwaka wa fedha *2024/2025*; na

*(d)* Kufuatilia ukusanyaji wa mapato katika Taasisi za Serikali pamoja na kufanya ziara za ukaguzi katika Taasisi husika.

## 1.2 MISWADA YA SHERIA NA TAARIFA ZA SERIKALI

Miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati hii ni kushughulikia miswada ya sheria ambayo itahitaji kufanyiwa mapitio na kujadiliwa katika Baraza la Wawakilishi ili kuwa sheria kamili. Katika kipindi hiki, Kamati ilipitia Miswada na Taarifa za Serikali zifuatayo:

*(a)* Mswada wa Sheria ya Mahkama ya Kadhi na Kuweka mambo Mengine yanayohusiana na hayo Nam. 8 ya 2023;

*(b)* Mswada wa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo Nam. 5 ya 2023;

*(c)* Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali mbali na Kuweka Masharti Bora ndani yake Nam. 6 ya 2023;

*(d)* Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali mbali na Kuweka Masharti Bora ndani yake Nam. 5 ya 2024;

*(e)* Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao, kusimamia huduma za Serikali Mtandao Zanzibar na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo, Nam. 1 ya 2024;

*(f)* Ripoti ya Hali ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2023/2024;

*(g)* Ripoti ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa mwaka 2023/2024;

*(h)* Ripoti ya Kazi za Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2023/2024;

*(i)* Ripoti ya Nane ya Tume ya Maadili kwa mwaka 2023/2024.

## 1.3 MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inaundwa na Wajumbe wafuatao:

| ***Nam.*** | ***Jina*** | ***Wadhifa*** |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Maryam Thani Juma | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Haji Shaaban waziri | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |
| *8.* | Mhe. Jamal Kassim Ali | Mjumbe |
| *9.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *10.* | Ndg.Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *11.* | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu |
| *12.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

## 1.4 HADIDU REJEA

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika kutekeleza majukumu yake ilitumia:

*(a)* Katiba ya Zanzibar ya Mwaka *1984*;

*(b)* Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka *2024*;

*(c)* Ripoti ya Kamati ya Mwaka 2023/2024;

*(d)* Hotuba za Bajeti kwa Mwaka wa fedha *2023/*2024 na *2024/2025* za Wizara zifuatazo:

   *(i)* Ofisi ya Rais Ikulu,

   *(ii)* Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais;

   *(iii)* Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;

   *(iv)* Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora;

   *(v)* Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ;

*(e)* Taarifa za Utekelezaji wa bajeti za Wizara na Taasisi husika.

# SEHEMU YA PILI

## 2. MAUDHUI YA RIPOTI

Sehemu hii itaelezea kwa kina mafanikio, changamoto na maagizo kwa kila taasisi ambayo ipo chini ya usimamizi wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kipindi cha mwaka 2024/2025.

Taasisi hizo ni:

(a) Afisi ya Rais Ikulu.

(b) Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais;

(c) Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;

(d) Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora; na

(e) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ;

### 2.1 OFISI YA RAIS – IKULU

Afisi ya Rais – Ikulu inatekeleza na kusimamia programu kuu Kumi na Moja (11) ambazo ndani yake zimo programu ndogo ndogo Kumi na Tisa (19), Programu hizi zimejumuisha mafungu makuu matano ya voti yenye kuakisi mipango yote ya Afisi kwa upande wa Unguja na Pemba. Katika utekelezaji wa kazi za kawaida na kazi za mandeleo, Kamati imefanikiwa kutembelea na kukagua shughuli mbali mbali ambazo zimepangwa kutekelezwa kwa kipindi hiki cha utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2024/2025.

**Mafanikio ya Utekelezaji wa Afisi ya Rais Ikulu**

Kimsingi, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa programu zote zilizopangwa na Afisi ya Rais Ikulu kwa namna zilivyotekelezwa kwa wakati na kwa ufanisi wa hali ya juu, utekelezaji ambao umeweza kutoa mafanikio mengi na makubwa kiasi kwamba hatuwezi kuyaeleza kwa kirefu. Hata hivyo, kamati imebainisha mafanikio machache kama ifuatavyo: -

*(i)* Kamati inampongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuadhimisha miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambapo amezindua miradi muhimu ya maendeleo inayolenga kuimarisha miundombinu na ustawi wa jamii. Miongoni mwa miradi hiyo ni uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa barabara ya juu (flyover) ya kwanza Zanzibar katika eneo la Mwanakwerekwe, Mkoa wa Mjini Magharibi, na barabara ya Kizimbani-Kiboje yenye urefu wa kilomita 7.2 katika Mkoa wa Kusini Unguja, iliyojengwa kwa kiwango cha lami.

*(ii)* Afisi imeimarisha mawasiliano na wananchi kupitia tovuti rasmi ya Ikulu (https://www.ikuluzanzibar.go.tz), ambapo taarifa 200 zimechapishwa na kutembelewa na watu 25,000, ikilinganishwa na 24,000 kwa robo moja ya mwaka 2024. Ongezeko hili linatokana na juhudi za kuwafikishia wananchi taarifa za utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais, pamoja na maagizo aliyoyatoa katika mikutano mbalimbali.

*(iii)* Afisi kupitia Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti. Afisi inaendelea na utafiti wa Tathmini ya utekelezaji wa Ahadi na Maagizo ya Mheshimiwa Rais kwa wananchi, kwa sasa, Afisi imefanikiwa kukusanya taarifa muhimu kutoka kwa Wizara na Taasisi za Serikali ambazo kwa njia moja au nyingine zimehusika na maagizo na ahadi hizo kwa upande wa Unguja.

*(iv)* Kupitia programu ya kusimamia huduma na shughuli za Mhe. Rais wa Zanzibar, Kamati inampongeza Mhe. Rais kwa kufanya

uzinduzi wa rasimu ya Dira ya Taifa 2050 ikibainisha mafanikio ya Dira ya Maendeleo ya 2025. Aidha, Mhe. Rais alieleza kuwa huduma za Afya zimeimarishwa kwa asilimia 78, huku wastani wa maisha ukiongezeka kutoka miaka 52 (2000) hadi 65.5 (2022).

*(v)* Kuimarika kwa mfumo wa Sema Na Rais Mwinyi (SNR) kwa kupokea malalamiko 1,481 ambapo malalamiko 741 sawa na asilimia 50.03 yamepatiwa ufumbuzi kwa kipindi cha miezi mitatu ya Oktoba, Novemba na Disemba 2024.

*(vi)* Afisi pia kupitia mfumo wa Sema Na Rais Mwinyi imechapisha vipeperushi 2,000 kwa wananchi Unguja na Pemba na kutoa mafunzo kwa wananchi wa Shehia 22 (Unguja 7 na Pemba 15).

*(vii)* Kuimarika kwa ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje wa Nchi (Diaspora).

*(viii)* Kuimarika kwa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kikanda na Kimataifa na kuifanya Zanzibar kushiriki katika mikutano na makongamano mbali mbali ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

**Maagizo ya Kamati:**

Katika programu kuu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi; Kamati inaishauri Afisi kuzidisha kasi ya kuwafikia walengwa na kuangalia maendeleo yao kama Wazanzibari wengine pamoja na kuimarisha uhusiano wa kikanda kwa kushiriki vikao na makongamano mbali mbali ambayo yanafanywa na nchi wanachama.

## 2.2 OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Baraza la Mapinduzi (BLM) limeundwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Kifungu cha 43(1) cha Katiba kinaeleza kuwa “Kutakuwa na Baraza la Mapinduzi ambalo litajumuisha Rais, Makamu

wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais, Mawaziri pamoja na Wajumbe wengine kama Rais atakavyoona inafaa". Kuundwa kwa Baraza hilo kunaenda sambamba na kuanzishwa kwa Afisi ya Baraza la Mapinduzi inayoratibu kazi za BLM. Afisi hii inaongozwa na kusimamiwa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi ambaye pia ni Katibu Mkuu Kiongozi na huteuliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 49 cha Katiba na Kifungu cha 14 cha Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya 2011. Vifungu hivyo, vinaeleza majukumu ya Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Ofisi ya BLM inatekeleza majukumu yafuatayo:

*(a)* Kuandaa mikutano ya Baraza la Mapinduzi na kutunza taarifa za mikutano.

*(b)* Kuchambua nyaraka zitazowasilishwa Baraza la Mapinduzi na Kamati zake.

*(c)* Kuwasilisha maamuzi na maelekezo kwa taasisi za utumishi wa umma zinazohusika.

*(d)* Kutoa msaada wa kufanya utafiti kwa Baraza la Mapinduzi katika mambo yanayongoja au yanayotarajiwa kuwasilishwa katika Baraza hili.

*(e)* Kutekeleza majukumu mengine yoyote kama Katibu Mkuu Kiongozi atakavyoona inafaa ikiwemo kuendesha programu za kujenga uwezo kwa viongozi wa ngazi za juu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kamati imeridhishwa na kazi zinazofanywa na Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kwa kuzingatia mustakabali mzuri wa nchi yetu.

**Mafanikio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Afisi ya BLM**

Kupitia utekelezaji wa Programu Kuu ya Uratibu wa Utumishi na Uendeshaji wa Afisi ya Baraza la Mapinduzi Zanzibar, afisi imefanikiwa katika mambo yafuatayo: -

(i) Afisi imeimarisha miundombinu ya Ofisi, majengo pamoja na mazingira yake ikiwa pamoja na kujenga tenti katika lango kuu la kuingilia katika ukumbi wa Makatibu Wakuu. Sambamba na hili, Ofisi imekifanyia matengenezo kisima chake hali iliyoondoa usumbufu na kupunguza gharama za ununuzi wa maji kwa ajili ya matumizi ya Ofisi.

(ii) Afisi ya BLM imeimarisha huduma za mawasiliano na utekelezaji wa kazi za kila siku kwa kununua vifaa vya kuandikia, vifaa vya samani, kufanya malipo ya huduma za posta, kulipa likizo na muda wa ziada kwa watumishi wake na kufanya matengenezo ya gari.

(iii) Afisi imewajengea uwezo wa kiutumishi wafanyakazi wake na kuwaendeleza kielimu kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

## 2.3 TAASISI YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZANZIBAR

Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa Zanzibar imeundwa na inafanya kazi chini ya Sheria Nam. 3 ya Mwaka 2008, ambayo imepewa majukumu ya msingi ya Taasisi hii ni kutunza na kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu kama urithi wa taifa. Vile vile, kusimamia kumbukumbu na nyaraka zote zinazozalishwa na kuhifadhiwa katika wizara, taasisi na mashirika ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na taasisi zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilizopo Zanzibar.

**Mafanikio ya Taasisi ya Nyaraka**

(i) Kamati inapenda kutoa pongezi za dhati kwa Taasisi ya Nyaraka kwa namna wanavyochapa kazi, ambapo kwa upande wa Pemba wastani wa nyaraka 245 zimefanyiwa uhaulishaji.
(ii) Taasisi imefanya ukaguzi kwa Wizara ya Kilimo Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa lengo la kutoa ushauri na maelekezo juu ya usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka.
(iii) Afisi pia, imetoa mafunzo kwa Maafisa Wadhamini, Waratibu na Wakuu wote wa taasisi ambao Ofisi zao zipo Pemba. Mafunzo hayo yalihusu Usimamizi wa kumbukumbu na Nyaraka, Utunzaji wa siri na Uanzishwaji wa Sheria namba 8 ya mwaka 2008 ya Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu.
(iv) Taasisi imetoa huduma za kiutafiti kwa wanajamii 140 kwa kupatiwa nambari za utambuzi wa kuingilia skuli.
(v) Taasisi imefanya ukarabati na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kuanzisha chumba cha uhuwishaji kumbukumbu na nyaraka kisiwani Pemba.

**Changamoto za Taasisi ya Nyaraka Zanzibar**

Licha mafanikio ambayo yamepatikana katika kipindi hiki, Kamati imeweza kubaini changamoto ambazo kimsingi zinahitaji utatuzi kama ifuatavyo:

*(i)* Ufinyu wa nafasi za ofisi kwa watendaji wa taasisi ya nyaraka hali inayopelekea mazingira magumu ya kazi.
*(ii)* Kutokukamilika kwa taratibu za ununuzi wa nyumba zilizojirani na jengo jipya la Kilimani ambazo zitawezesha kuwepo kwa nafasi ya kutosha ya maegesho ya gari.

**Maagizo ya Kamati kwa Taasisi ya Nyaraka Zanzibar**

*(i)* Kamati inaipongeza Taasisi kwa kuweza kufanikisha suala zima la ununuzi wa makabati ya kuhifadhia Nyaraka na kuweka vipoza hewa

katika ghala la kuhifadhia nyaraka hizo, hata hivyo, kamati inashauri kutunza vifaa hivyo ili viweze kutumika kwa muda mrefu;

*(ii)* Kamati inaiagiza wizara kukamilisha kwa haraka mpango wake wa marekebisho ya Sheria namba 8 ya mwaka 2008 ili kwenda na wakati.

*(iii)* Taasisi izidishe mashirikiano na taasisi za umma na binafsi kwa lengo la kuimarisha mfumo wa kuhifadhia kumbukumbu na kutunza historia ya Zanzibar;

*(iv)* kuwajengea uwezo watendaji wake kwa lengo kuwa na wataalamu wa kutosha katika sekta hii pamoja na kuondosha changamoto za kitaalamu;

*(v)* kamati inaipongeza taasisi hii kwa hatua ya kuendeleza mpango wa ujenzi wa jengo jipya katika eneo la Kilimani. Hata hivyo, inashauriwa kufuatilia na kununua nyumba zilizopo katika eneo hilo kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya gari.

*(vi)* Kamati inashauri taasisi hii kutoa muongozo maalumu wa kuboresha uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka kwa taasisi za Serikali na binafsi.

## 2.4 AFISI YA USALAMA WA SERIKALI (GSO)

Afisi ya Usalama wa Serikali (GSO) inafanya kazi chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya mwaka 2011, kifungu 78(1) - (5) na Utaratibu wa Utendaji kazi wa GSO wa mwaka 1994. Kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 Afisi ililenga kuimarisha usalama katika maeneo muhimu, ikiwa ni pamoja na upekuzi wa waajiriwa wapya na Watumishi wa Serikali, Ukaguzi wa Majengo ya Serikali na kutoa mafunzo kwa watumishi wa Serikali kuhusu usalama na maadili.

### Mafanikio ya Afisi ya Usalama Zanzibar

Afisi ya usalama wa Serikali Zanzibar imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutekeleza majukumu yake makuu ambayo ni:

*(i)* Kufuatia upekuzi uliofanywa na afisi hii ambao umepelekea kupatikana kwa watumishi wenye tabia njema na wenye uzalendo wa kuitumikia nchi yao.

*(ii)* Kuimarika kwa usalama wa majengo kutokana na ukaguzi ambao umewezesha maboresho muhimu ya miundombinu ya usalama, kuongeza ufahamu wa umuhimu wa usalama, na kubaini viashiria hatarishi katika majengo ya Serikali.

*(iii)* Kuongeza uelewa wa usalama kwa watumishi kwa kutoa mafunzo ya usalama kwa watumishi wa Serikali ambayo yameongeza ufanisi katika utunzaji wa siri za Serikali na kuboresha huduma kwa wananchi.

**Changamoto zinazoikabili Afisi ya Usalama wa Serikali (GSO) Zanzibar**

Mbali ya kuwepo kwa mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, Afisi ya GSO inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Kutopatikana kwa taarifa za marekebisho yanayotokana na mapendekezo yanayotolewa na Afisi ya Usalama wa Serikali baada ukaguzi wa kiusalama wa majengo;

*(ii)* Kutotekelezwa kwa vitendo miongozo na mafunzo ya utunzaji na udhibiti wa siri za Serikali yanayotolewa na GSO katika utendaji wao wa kazi kwa baadhi ya taasisi.

*(iii)* Uwepo wa matumizi makubwa ya teknolojia ya habari na mawasiliano kunakopelekea uvujaji wa taarifa na uharibifu wa miundombinu ya Serikali kwa watu wenye nia mbaya.

**Maagizo ya Kamati kwa Afisi ya Usalama wa Serikali (GSO) Zanzibar**

*(i)* Kamati inaagiza Ofisi ya GSO kuongeza kasi ya kufuatilia utekelezaji wa ushauri uliyopendekezwa kila inapobidi ili kuhakikisha uimarishaji wa usalama wa majengo na miundombinu ya Serikali.

*(ii)* Kamati inashauri Ofisi ya Usalama Serikalini kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar kuhakikisha kanuni na taratibu za usalama za matumizi ya mitandao zinafuatwa ili kuondoa mianya ya uvujaji wa taarifa na uharibifu wa miundombinu ya serikali.

## 2.5 MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR

Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar imeanzishwa Mwaka 2024 kwa Sheria nambari moja (1) ya Mwaka 2024. Mamlaka ya Serikali Mtandao inaundwa na Idara Tatu, na Vitengo vitano (5). Kutokana na utaratibu wa Serikali wa kutekeleza majukumu yake kwa kutumia Bajeti inayotumia Programu (Programme Based Budget), Mamlaka ya Serikali Mtandao inatekeleza Programu Kuu mbili na Programu Ndogo Nne.

Programu hizi zimetokana na majukumu mahsusi ya Serikali Mtandao ambayo ni: -

*(i)* Kuandaa na kusimamia Sera, kanuni na Miongozo ya maendeleo na matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa umma,

*(ii)* Kuandaa Mipango ya Kitaifa ya maendeleo na matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa umma pamoja na kuratibu utekelezaji wa mipango hiyo,

*(iii)* Kuishauri Serikali katika matumizi bora ya TEHAMA katika uendeshaji na utoaji huduma za umma,

*(iv)* Kuendeleza matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma kwa ajili ya kuimarisha ufanisi na uthabiti wa utendaji kazi wa Serikali, utoaji huduma kwa umma pamoja na kupeana na kubadilishana taarifa baina ya taasisi za Serikali, Serikali na sekta binafsi pamoja na wananchi kwa ujumla,

*(v)* Kutoa miongozo na kufanya tathmini ya ubora wa mifumo ya TEHAMA katika Utumishi wa Umma na kuhakikisha kwamba ubora wa vifaa vya TEHAMA katika utumishi wa umma vinakuwa katika viwango vinavyokubalika na

(vi) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Usalama wa TEHAMA na muongozo wa matumizi yake katika utumishi wa umma.

**Mafanikio ya Mamlaka wa Serikali Mtandao Zanzibar**

Mamlaka imeweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa na hivyo kufanikiwa kuleta mchango mkubw akatika Nyanja za kimanedeleo. Baadhi ya mafanikio hayo ni kama ifuatavyo: -

*(i)* Kuanzishwa mfumo wa usajili wa watalaamu wa TEHAMA na rasilimali (ICT Register) ambao una lengo la kufanya tathmini kwa maafisa TEHAMA, vifaa na miradi ya TEHAMA inayosimamiwa na Serikali na taasisi za umma, jumla ya maafisa TEHAMA 395 walisajiliwa katika mfumo huo.

*(ii)* Mamlaka imefanikiwa kutengeneza mfumo wa kituo kimoja (One Stop Center) ambacho kinahusiana na uondoshaji na uingizaji wa shehena maeneo ya forodha ya Unguja na Pemba ili kuondosha urasimu na kurahisisha upatikanaji wa huduma za haraka Bandarini.

*(iii)* Mamlaka ya Serikali Mtandao imeanzisha Kituo cha kukabiliana na majanga kwa kuweza kuhifadhi Mifumo ya TEHAMA katika sehemu mbadala (Disaster Recovery Center).

*(iv)* Mamlaka imefanya Ukaguzi na Tathmini ya Mifumo ya TEHAMA katika Taasisi za Umma. Jumla ya mifumo kumi na mbili (12) imefanyiwa ukaguzi na Tathmini katika Taasisi za Umma.

*(v)* Mradi wa Mifumo ya Kielektroniki wa Afya jamii Pamoja na Uhifadhi wa Kumbukumbu za Wagonjwa (ZanEMR). Usimamizi wa miradi ya mifumo ya kielektroniki ya afya inaendelea kuimarishwa, ikiwa na lengo la kuhakikisha upatikanaji rahisi wa taarifa za wagonjwa.

**Changamoto za Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar**

*(i)* Uhaba wa watumishi wabobezi katika fani za teknolojia ya habari na mawasiliano.

*(ii)* Baadhi ya Taasisi zimekuwa na uzito katika kufuata na kutumia mifumo ya Mamlaka ya Serikali Mtandao hususan taasisi za kifedha.

*(iii)* Utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka hii yamekuwa yakiathiriwa na upatikanaji mdogo wa fedha za uendeshaji ambapo ndio rasilimali muhimu katika kufanikisha malengo yake.

**Maagizo ya Kamati kwa Mamlaka**

*(i)* Kamati inaishauri Serikali kuipa umuhimu ofisi kwa kuwapatia watumishi wabobezi katika fani za teknolojia ya habari na mawasiliano ili kupata ufanisi wa majukumu yake.

*(ii)* Kamati inashauri Serikali kuzichukulia hatua kali baadhi ya Taasisi ambazo hazifuati na hazitumii mifumo ya Mamlaka ya Serikali Mtandao hususan taasisi za kifedha.

*(iii)* Kamati inashauri Serikali kuwapatia fedha za kutosha kwa mujibu wa bajeti yake inayopangwa kila mwaka ili kwenda sambamba na mahitaji ya teknolojia ulimwenguni.

## 2.6 TAASISI YA AFISI YA RAIS, UFUATILIAJI NA USIMAMIZI WA UTENDAJI SERIKALINI - ZANZIBAR (ZPDB)

Taasisi hii ilianzishwa tarehe 02 Disemba, 2022 kwa lengo la kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa miradi ya vipaumbele ili kufikia maendeleo endelevu. Kwa dhamira ya kufanikisha kwa haraka na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake, Taasisi imekuwa

ikishirikiana na Wizara na Taasisi za Serikali zote mbili za Tanzania; Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri wa Muungano ya Tanzania (SMZ na SMT).

**Mafanikio ya Taasisi ya ZPDB**

*(i)* ZPDB kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) na Idara ya Habari Maelezo Zanzibar imeweza kuandaa na kuendesha vipindi maalum vya Viongozi wa Wizara na Taasisi za Serikali. Lengo la vipindi hivyo ni kueleza mafanikio ya Serikali katika kipindi cha miaka 61 tangu Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

*(ii)* Taasisi ya ZPDB kwa kushirikiana na Taasisi ya Tony Blair (TBI) imeweza kuisaidia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuandaa Mpango wa Mageuzi wa Utalii. Aidha, Taasisi ya ZPDB kwa kushirikiana na TBI imeipitia Sera ya Utalii Zanzibar ili kuweza kuendana na Mpango wa Mageuzi wa Utalii Duniani.

*(iii)* Taasisi ya ZPDB imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya Sekta ya Miundombinu ambapo Taasisi imesimamia ujenzi wa barabara mbali mbali zinazojengwa hapa nchini ambapo maendeleo ya miradi inaridhisha.

*(iv)* Taasisi ya ZPDB kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imeendelea kuratibu Mikataba ya Matokeo ya Miradi ya Kipaumbele (Priority Projects Results Agreements - PPRAs) kwa lengo la kutoa mafunzo kwa taasisi zinzotekeleza miradi ya kimkakati ikiwemo Wizara ya Elimu na wizara ya Afya Zanzibar.

*(v)* Katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Taasisi imekamilisha tathmini ya utekelezaji wa Mikataba ya Sekta Binafsi (Outsourcing) ya Mamlaka ya Bandari, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Maabara

ya Upimaji wa Afya Kazini (ZANMEDICAL). Taasisi inaendelea kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya tathmini hiyo.

**Maagizo ya Kamati kwa ZPDB:**

*(i)* Kamati inashauri taasisi hii kuzidisha kasi ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya kimkakati ili kusaidia Serikali kufanikisha malengo yake.

*(ii)* Kamati inashauri ZPDB izidishe kasi ya kuwapatia mafunzo watendaji wake kwa lengo la kupata wataalamu katika fani mbali mbali kwani kazi wanazofanya zinahitaji wataalamu wabobezi ambao wana uzoefu wakutosha.

*(iii)* Kamati inashauri taasisi hii kuongeza mashirikiano na mashirika ya umma katika kutekeleza majukumu yake ya usimamizi wa miradi ya maendeleo husuan miradi ya kimkakati ambayo itaifanya Zanzibar kukua kiuchumi.

## 2.7 AFISI KUU - PEMBA

Afisi ya Rais Ikulu - Pemba ni miongoni mwa afisi ziliopo chini ya Afisi ya Rais Ikulu - Zanzibar. Afisi hii inajukumu kubwa la kusimamia na kuratibu kazi zote za Afisi ya Rais Ikulu kwa upande wa Pemba kwa kushirikiana kwa karibu na Afisi kuu iliopo Zanzibar.

**Mafanikio ya Afisi Kuu – Pemba**

*(i)* Afisi imeweza kufanya ufuatiliaji wa shughuli mbali mbali zinazotekelezwa na Afisi ya Rais – Ikulu pamoja na kufuatilia miradi ya maendeleo ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa mujibu wa mikataba na inakamilika kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa ili kuleta manufaa na tija kwa jamii na Taifa.

*(ii)* Ofisi imeandaa na kurusha hewani vipindi vya radio, TV na mitandao ya kijamii ili kutoa elimu kwa jamii kuhusu utekelezaji wa

Miradi inayofanywa na Serikali ya awamu ya nane pamoja na faida zake kwa jamii.

*(iii)*Ofisi inaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake, ambapo kwa kupindi cha robo ya pili (Oktoba - Disemba) jumla ya watumishi saba (7) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

*(iv)*Ofisi imeendelea na kuimarisha huduma kwa Ikulu ya Pagali na Mkoani, ikiwemo kufanya maboresho ya mfumo wa umeme na maji ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya umeme na maji inapatikana wakati wote.

**Maagizo ya Kamati kwa Afisi ya Rais Ikulu – Pemba**

Kwa kuwa afisi inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa jengo la ofisi ya kudumu; Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuanza mchakato wa ujenzi wa jengo la matumizi ya ofisi ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

## 3. OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Itakumbukwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iliyoanzishwa rasmi mwaka 2010 kufuatia marekebisho ya 11 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, iliyoruhusu kuwepo na kuanzishwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ibara ya 39 (5) ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 inaelekeza kuwepo kwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar ambaye atakuwa Mshauri Mkuu wa Rais katika kutekeleza kazi zake.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inashughulikia masuala mtambuka ya uhifadhi, usimamizi na utunzaji wa mazingira, masuala ya watu wenye ulemavu, masuala ya VVU na UKIMWI na masuala yanayohusu udhibiti wa dawa za kulevya. Aidha, Ofisi hii inasimamia na kuratibu Ofisi ya faragha ya

Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na masuala ya Sera, Mipango na Tafiti za Ofisi.

Muundo wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais unasimamiwa na taasisi zifuatazo:

*(a)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,
*(b)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi,
*(c)* Idara ya Faragha, 4. Idara ya Mazingira,
*(d)* Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira,
*(e)* Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu,
*(f)* Tume ya Taifa ya Ukimwi,
*(g)* Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na
*(h)* Afisi Kuu Pemba.

## 3.1 MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ZANZIBAR (ZEMA)

Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA) imeanzishwa chini ya kifungu cha 14 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ya mwaka 2015. Lengo Kuu la Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ni kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria, kanuni, miongozo na viwango vya mazingira kwa ajili ya kupunguza uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Aidha, Mamlaka ya ZEMA inasimamiwa na Bodi iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) na imepangiwa majukumu yake kwa mujibu wa kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, 2015.

**Mafanikio ya ZEMA**

a) Kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki kwa ajili ya kuondoa athari za kimazingira na kiafya zinatokana na mifuko ya plastiki.

b) Kudhitbiti uharibifu wa Mazingira unaotokana na uchimbaji na uchukuaji holela wa maliasili zisizorejesheka.
c) kupunguza uharibifu na uchafuzi wa mazingira kwenye jamii.
d) Kukuza uelewa na ushiriki wa jamii juu ya uhifadhi wa Mazingira uliowahamasisha upatikanaji wa vipindi vilivyokuwa havina malipo kutoka vituo husika.

**Changamoto ya Utekelezaji wa Mamlaka**

Changamoto kubwa ziliopo zinazohusiana na Sera, Sheria na mifumo ya kitaasisi katika Usimamizi wa mazingira, miongoni mwao ni kama zifuatavyo:

*(i)* Ufinyu wa jengo la ofisi ambalo linapelekea uhaba wa nafasi kwa wafanyakazi wa sekta ya Mazingira.

*(ii)* Upungufu wa gari pamoja na vitendea kazi kunapelekea kutofikiwa lengo la kufanya ufuatiliaji na operesheni mbali mbali za kimazingira.

**Maagizo ya Kamati**

Katika kuendeleza matumizi bora ya mazingira na uhifadhi wa mazingira katika jamii zetu suala la utoaji wa elimu linahitajika zaidi ili jamii zifahamu umuhimu wake katika maisha ya kila siku. Pamoja na hilo, Kamati pia inashauri yafuatayo:

*(i)* Kwa kuwa ZEMA tayari imefanikiwa kupimiwa kiwanja na inasubiri kukabidhiwa hati ya kiwanja kutoka Kamisheni ya Ardhi. Kamati inashauri kuanza kwa ujenzi huo haraka iwezekanavyo baada ya kukamilisha taratibu na Wakala wa Majengo kwa ajili ya kutayarishiwa ramani pamoja na makisio ya gharama za ujenzi kwa mujibu wa ramani hiyo (BoQ).

*(ii)* Kutokana na ZEMA kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango vigezo (specifications) kwa ajili ya kukamilisha taratibu za ununuzi wa gari ambayo kimsingi fedha zake zimeshaingizwa. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuharakisha ununuzi wa gari hiyo.

## 3.2 MAMLAKA YA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria nambari 8 ya mwaka 2021 kwa lengo la kudhibiti Usafirishaji, Usambazaji na Utumiaji wa Dawa za kulevya nchini.

**Mafanikio ya Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar**

Mamlaka ya Dawa za Kulevya imefanikiwa katika mambo yafuatayo:

*(i)* Kupata jengo kutoka Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo katika eneo la Pujini Wilaya ya Chake – Chake Pemba kwa ajili ya matumizi ya ofisi ya Mamlaka.

*(ii)* Kufanikiwa kuteketeza vielelezo vya dawa za kulevya aina mbalimbali kutoka Mahkamani na vituo vya Polisi Unguja na Pemba.

*(iii)* Kusambaratisha mtandao wa wahalifu wakubwa ambao walitumika kuingiza na kusambaza dawa za kulevya nchini.

*(iv)* Kamati inaipongeza Mamlaka kwa kufakiwa kupata kiwanja kwa ajili wa ujenzi wa Sober ya Wanawake katika eneo la Kangagani, Kisiwani Pemba.

**Changamoto za Mamlaka**

Mbali na mafanikio yaliyopatikana, kuna changamoto kadhaa zinazokabili mamlaka hii, miongoni mwao ni:

*(i)* Upungufu wa vitendea kazi vya Ofisi kama gari, pikipiki na vifaa vya kisasa vya uchunguzi.

*(ii)* Jamii kuwa na muhali wa kutoa taarifa za uhalifu wa dawa za kulevya katika maeneo yao.

*(iii)* Upungufu wa fedha za kugharamia operesheni za nchi kavu, baharini na utafiti wa tatizo la Dawa za Kulevya.

*(iv)* Uhaba wa wafanya kazi katika taaluma mbalimbali.

*(v)* Uwepo wa vijana wasio na ajira rasmi, hali inayopelekea kujiingiza katika uhalifu wa dawa za kulevya na uhalifu mwengine wa kupangwa.

*(vi)* Kutokuwa na sera na mikakati ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya katika taasisi za Serikali.

**Maagizo ya Kamati kwa Mamlaka**

Kutokana na changamoto hizo ambazo Mamlaka inakabiliana nazo katika mazingira mbali mbali, Kamati inashauri mambo yafuatayo:

*(i)* Kamati inaishauri Mamlaka kujenga mashirikiano zaidi na jamii ili kusaidia kupata taarifa za kudhibiti bandari bubu ambazo inasemekana kwa kiasi kikubwa zinatumika kupitishia dawa za kulevya kwa pwani ya Zanzibar.

*(ii)* Kamati inashauri Serikali kuanzisha idara maalumu ndani ya mahakama ambayo itashughulikia mashauri ya Dawa za Kulevya peke yake kama ilivyo kwa kesi za udhalilishaji ili kuwezesha mashauri hayo kwenda kwa haraka.

*(iii)* Kamati inaishauri Mamlaka kutoa elimu kwa jamii namna ya kujenga mazoea ya kuwaona waathirika wa Dawa za Kulevya kuwa ni watu wema na wenye kuaminika katika jamii baada ya kutoka vituo vya kurekebisha tabia.

*(iv)* Kamati inaigiza Mamlaka kuimarisha mifumo ya kukusanya taarifa za uhalifu wa dawa za kulevya kwa kuzishirikisha Sekta binafsi na Taasisi za kidini katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

*(v)* Kamati inaigiza Mamlaka kufanya tafiti mbali mbali ili kubaini mbinu mpya zinazotumika katika usambazaji, usafirishaji na uuzaji wa dawa za kulevya.

*(vi)* Kamati inaishauri Mamlaka kuendelea kufanya vikao vya pamoja kati ya Wizara ya Afya, Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi (ZFDA) na wadau wa sekta binafsi wanaoshughulika na dawa tiba zenye asili ya

kulevya juu ya kudhibiti na utoaji wa vibali na usimamizi wa dawa hizo.

## 3.3 TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Tume ya UKIMWI Zanzibar (ZAC) imeanzishwa Mwaka 2002 chini ya Sheria ya Tume ya UKIMWI Namb.3 ya mwaka 2002 kwa lengo la kuratibu muitiko wa Taifa wa UKIMWI; pamoja na mambo mengine kuhakikisha kwamba maambukizo ya Virusi vya UKIMWI yanadhibitiwa nchini mwetu. Aidha miongoni mwa majukumu ya msingi kwa taasisi hii ni kuhamasisha na kutetea masuala ya UKIMWI, kuweka miongozo, kutafuta rasilimali, kufuatilia na kutathmini muitiko wa Taifa wa UKIMWI.

**Mafanikio ya Tume ya UKIMWI**

*(i)* Watendaji wa taasisi mbali mbali wameona haja na umuhimu wa kutekeleza mipango ya UKIMWI ndani ya taasisi zao na katika miradi ya maendeleo ili kudhibiti maambukizi mapya ya VVU.

*(ii)* Kuwepo kwa mkakati unaosaidia kuwafikia kundi la vijana ambalo liko hatarini zaidi kupata maambukizi mapya.

*(iii)* Kufanyika mijadala ya vijana imesaidia kubuni programu zitakazosaidia kuwalinda na maambukizo ya VVU na kuimarisha upatikanaji wa huduma.

**Changamoto za Tume ya Ukimwi**

*(i)* Uhaba wa fedha katika mapambano dhidi ya kutokomeza janga la UKIMWI unaopelekea utegemezi kwa washirika wa maendeleo.

*(ii)* Unyanyapaa kwa Watu wenye kuishi na Virusi vya UKIMWI.

*(iii)* Uhaba wa fedha za ndani unapelekea kuacha kutekeleza shughuli nyingi za msingi kama kutanua wigo wa uratibu, kuwajengea uwezo wadau, ufuatiliaji, tathmini na utafiti na utetezi na programu za jamii.

**Maagizo ya Kamati**

Kama ilivyo kwa maradhi mengine katika jamii jinsi Serikali kwa kushirikiana na washirika mbali mbali wanavyopambana kupunguza au kuyatokomeza kabisa, maradhi ya UKIMWI na VVU pia yanapaswa kuangaliwa kwa hatua madhubuti bila ya kuyachukulia kama maradhi ya kawaida katika jamii. Hivyo, kutokana na Kamati kubaini kupungua kwa mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI katika jamii, Kamati inashauri mambo yafuatayo:

*(i)* Kamati inashauri Serikali kuongeza bajeti ya fedha kwa Tume ya UKIMWI ili kusaidia kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI ili kuacha kutegemea wahisani wa maendeleo.

*(ii)* Kamati haikufurahishwa na kasi ya upatikanaji wa dawa za watoto wanaoishi na virusi vya Ukimwi kutokana na kupatikana kwa asilimia ndogo sana, hivyo inashauri juhudi za lazima kuchukuliwa ili dawa hizo ziweze kupatikana kwa wingi na kwa wakati.

*(iii)* Kamati inaiagiza Tume kutoa elimu zaidi kwa vijana katika sehemu za fukwe juu ya namna bora ya kujiepusha na janga la maradhi ya UKIMWI.

*(iv)* Kama ilivyo kwa maradhi mengine katika jamii jinsi Serikali kwa kushirikiana na washirika mbali mbali wanavyopambana kupunguza au kuyatokomeza kabisa, kamati inashauri Serikali kuchukua hatua madhubuti ya kupambana na janga la UKIMWI na VVU bila ya kuyachukulia kama maradhi ya kawaida katika jamii.

## 3.4 BARAZA LA TAIFA LA WATU WENYE ULEMAVU

Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar limeundwa Chini ya Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa) Namba 8 ya Mwaka 2022. Baraza linafanya kazi kwa nia ya kuishauri Serikali juu ya maslahi yote ya watu wenye ulemavu kwa kuhakikisha wanasimamia na kufuatilia masuala ya elimu mjumuisho katika jamii ili watu wenye ulemavu waweze kupata elimu kama watu wengine.

**Mafanikio ya Baraza la Watu wenye Ulemavu**

*(i)* Kwa mwaka 2024/ 2025 Baraza limekamilisha shughuli ya maadhimisho ya Watu wenye Ulemavu Kitaifa ambayo kilele chake kimefanyika Kisiwani Pemba.

*(ii)* Kukamilisha kazi ya kuandaa mfumo wa kuhifadhi taarifa za watu Wenye Ulemavu ambao upo tayari kwa hatua za matumizi ya usajili wa Watu wenye Ulemavu;

*(iii)* Kuendelea kuwapatia vifaa saidizi watu wenye ulemavu ambapo wastani wa vifaa 105 vimetolewa kwa vipindi tofauti, na

*(iv)* Kuendelea kuwajengea uwezo na uelewa watu wenye ulemavu ambapo jumla ya watu 20 wamelipiwa gaharama za masomo katika ngazi ya Cheti na Astashahada.

**Changamoto za Baraza la Watu Wenye Ulemavu**

*(i)* Baraza linakabiliwa na uchakavu wa vyombo vya usafiri na vitendea kazi vya ofisi.

*(ii)* Uelewa mdogo wa jamii kuhusu thamani na nafasi ya watu wenye ulemavu.

*(iii)* Kuwepo kwa kundi kubwa la watu wenye ulemavu ambao wanashindwa kupata mkopo kulingana na masharti magumu yaliyowekwa kutokana na ulemavu wao. Kundi hilo linajumuisha vikundi vya watu 79 na mtu mmoja mmoja 82 wenye ulemavu wa uoni, viungo, uziwi na ualbino.

**Maagizo ya Kamati kwa Baraza la Watu Wenye Ulemavu**

Katika kuhakikisha jamii ya watu wenye ulemavu inasaidiwa na kupewa mashirikiano mema katika nchi yetu, hatunabudi kuhakikisha jamii hii inapatiwa fedha na nyenzo za kutosha katika kupambania maisha na maslahi yao. Kwa mantiki hiyo, kamati inashauri mambo yafuatayo: -

*(i)* Kwa kuwa zipo taasisi zenye kutoa mikopo ya kifedha kwa ajili vikundi vya watu wenye ulemavu, Kamati inashauri Serikali kuzielekeza taasisi hizo kuregeza masharti ya mikopo kwa watu wenye ulemavu ili kuweza kutoa mikopo kwa mtu mmoja mmoja kulingana na aina ya ulemavu alionao kwasababu ni vigumu katika nchi yetu kupata kikundi cha watu 10 au zaidi wenye ulemavu wa aina moja katika eneo moja ambao watakua na aina moja ya ulemavu.

*(ii)* Kamati inaliomba Baraza kuendelea kutoa elimu kwa umma juu haki za watu wenye ulemavu sambamba na kuishajihisha jamii kuwathamini na kutowabagua katika shughuli mbali mbali za kijamii pamoja na fursa zinazojitokeza.

*(iii)* Kamati inashauri Serikali kusaidia nguvu za Baraza kwa kuwapatia vyombo vya usafiri ambavyo vitawasaidia katika majukumu yao ya kila siku.

*(iv)* Kamati inaigiza Serikali kuimarisha mabaraza katika ngazi ya Wilaya kwa ajili ya kuimarsiha huduma za jamii.

## 3.5 AFISI KUU PEMBA

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba kwa mwaka 2024/2025 inaendelea kuchukua juhudi mbalimbali katika kufanikisha shughuli zake pamoja na mipango mbalimbali ya Serikali. Juhudi hizo zimetoa mafanikio kadhaa ikiwemo Kuwapatia wananchi mitungi ya gesi kwa ajili ya

kushajihisha matumizi ya nishati mbadala,. Miongoni mwa Shehia zilizopatiwa vifaa hivyo ni pamoja na Shehia ya Kisiwa Panza ambapo jumla ya mitungi 789 ilitolewa kwa wanakijiji.

Sambamba na hili, Ofisi imeweza kukamilisha ujenzi wa matuta mawili yaliyojengwa katika eneo shehia ya Mkungu - Sipwese yenye urefu wa Mita 400.
Kuanza kwa ujenzi wa ukuta wa kuzuia Maji ya chumvi yasiingie katika mashamba ya wananchi katika Shehia ya Kisiwa Panza ambapo ujenzi huo umefikia 45%.

Lengo la kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi sambamba na matumizi safi ya nishati mbadala ofisi inaendelea kuhamasisha jamii juu ya mpango wa Serikali katika kulinda, kuhifadhi na kupanda miti ili kutimiza malengo ya kuirithisha Zanzibar ya kijani kupitia mpango wa kuifanya Zanzibar ya Kijani.

Sambamba na hilo, ofisi inaendelea kuelimisha jamii juu ya kuwa na tabia njema kwa kuacha tabia hatarishi ya kujiingiza katika makundi yaliyoathirika na dawa za kulevya, VVU pamoja na kuepuka vitendo vya udhalilishaji kwa jamii juu ya watu wenye ulemavu kwa kuzingatia miongozo na sheria zetu.

## 4. OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi imeanzishwa mwaka *2010* kutokana na mabadiliko ya *kumi na moja (11)* ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984* toleo la *2010*. Jukumu la jumla la Ofisi hii ni kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na masuala ya Muungano kwa upande wa Zanzibar.

Sambamba na hayo, Majukumu mahususi ya Ofisi hii ni pamoja na kutoa huduma bora kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais; kujenga uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa; kuandaa na kuratibu sherehe na maadhimisho ya kitaifa; kuratibu masuala ya muungano; kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Tanzania Bara. Vilevile Ofisi inaratibu na kusimamia shughuli za Baraza la Wawakilishi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi inaundwa na Idara zifuatazo:

*(i)* Idara ya Huduma za Makamu wa Pili wa Rais.
*(ii)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
*(iii)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
*(iv)* Idara ya Maafa.
*(v)* Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa.
*(vi)* Idara ya Kuratibu Shughuli za Serikali.
*(vii)* Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ.
*(viii)* Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba.

Vile vile, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi inasimamia Taasisi zinazojitegemea zifuatazo:

*(i)* Baraza la Wawakilishi la Zanzibar (BLW).
*(ii)* Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

## 4.1 BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ni chombo cha uwakilishi wa wananchi na kilichoanzishwa chini ya kifungu cha 63 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, lenye jukumu la kutunga sheria, uwakilishi wa wananchi na usimamizi wa Serikali , kustawisha demokrasia na uwakilishi wa watu wa Zanzibar, Kukuza na Kudumisha Demokrasia halisi ya Kibunge katika Zanzibar ambayo itawajengea uwezo wananchi wa kushiriki katika shughuli za Kidemokrasia ya Kibunge na nyenginezo kwa ajili ya kufikia maendeleo endelevu na Utawala Bora.

Kama yalivyo mabunge mengine duniani, Baraza la Wawakilishi linatekeleza majukumu yake ya msingi ya Kutunga Sheria, Kusimamia Serikali na Kuwawakilisha wananchi. Majukumu yake ya msingi yametajwa katika kifungu cha 88 cha Katiba ya Zanzibar kama ifuatavyo:

(a) kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitaji kuwepo kwa sheria hiyo;
(b) kujadili shughuli za kila Wizara wakati wa kikao cha mwaka wa Bajeti katika Baraza la Wawakilishi;
(c) kuuliza masuala mbali mbali kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi;
(d) kuidhinisha na kusimamia mipango ya maendeleo ya Serikali katika njia ile ile ambayo Bajeti ya mwaka inaidhinishwa.

**Changamoto za Baraza la Wawakilishi Zanzibar**

Katika utekelezaji wa shughuli za Baraza zipo changamoto mbali mbali ambazo zinapunguza ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za Afisi. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:

*(i)* Kufuatia kuidhinishwa kwa Muundo mpya wa Afisi ambao umepelekea kuongezeka kwa Idara, Vitengo, Divisheni na Ofisi kumesababisha kuongezeka kwa majukumu huku kukiwa na uhaba wa watumishi. Hata hivyo, kuna upatikanaji mdogo wa watumishi kupitia utaratibu wa maombi ya watumishi uliowekwa na Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma.

*(ii)* ufinyu wa kumbi za mikutano ya Kamati kutokana na nafasi ndogo ya jengo la Baraza. Aidha, utekelezaji wa Muundo Mpya umesababisha kuongeza uhaba wa nafasi, kwani unahitaji ongezeko kubwa la watumishi. Hata hivyo, hatua tayari zimeshachukuliwa za matayarisho ya ujenzi wa jengo jipya litakalojumuisha kumbi za kutosheleza kwa kazi za Kamati na Baraza.

*(iii)* Uhaba wa vyombo vya usafiri unaathiri shughuli za Kamati pamoja na kazi za kila siku za Afisi ambalo limepelekea kuazima gari kutoka taasisi nyengine au kukodi gari za binafsi. Kwa hivi sasa Afisi imepatiwa gari mbili kwa ajili ya kazi za Kamati ambazo hazitoshi.

*(iv)* Bajeti iliyopo ni ndogo kuweza kuwajengea uwezo Wajumbe na watumishi hususani katika uchambuzi wa bajeti, Miswada ya Sheria na taarifa za kifedha. Ufinyu wa bajeti unachangiwa na ukomo(ceiling) unaopangiwa Afisi ya Baraza ambao kwa kawaida hauakisi mahitaji yote yanayohitajika kwa mwaka husika.

*(v)* Afisi ya Baraza bado haijaanza kutumia njia za kisasa katika shughuli za Baraza ikiwemo “video conference equipment”, “smart board” na “digital recoder” ambazo zinasaidia kufanya kazi kwa ufanisi kwa kupunguza gharama na muda wa kufanya kazi kutokana na ukosefu wa nyenzo za kisasa za kufanyia kazi.

**Maagizo kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar.**

*(i)* Kamati inashauri afisi ya Baraza kuharakisha taratibu za Mzabuni na Mjenzi wa jengo jipya ili kuondoa changamoto ya ufinyu wa nafasi uliokuwepo na kuweka nafasi za ziada kwa ajili ya ongezeko la watumishi, vitendea kazi na huduma nyengine mbali mbali.

*(ii)* Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kuipatia gari mbili tu kwa matumizi ya Kamati na gari mbili kwa matumizi ya viongozi (Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika). Hata hivyo, Kamati inaisisitiza Serikali kufuatilia gari za ziada kwa matumizi ya Baraza na Afisi ya Baraza.

*(iii)* Kamati inaishauri Serikali kuwaongezea bajeti ili iweze kufanya ununuzi wa vifaa na mafunzo ili kuongeza ufanisi katika utumiaji wa vifaa vya kisasa hasa ikizingatiwa kuwa mabunge mengi hivi sasa yanafanyakazi zake kwa njia za kisasa.

## 4.2 TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imeundwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu cha 119(1). Majukumu ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, yameelezwa katika Katiba hiyo, Sheria ya Uchaguzi Namba 4 ya mwaka 2018, Sheria ya kuanzishwa kwa Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya mwaka 2017, Sheria ya Kura ya Maoni ya mwaka 2010 pamoja na Sheria nyenginezo na kanuni zake.

Aidha, katika kutekeleza majukumu ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imekuwa ikifanya shughuli mbali mbali ikiwemo, kusimamia na kuendesha mwenendo mzima wa Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar, Kusimamia, kukuza na kuratibu elimu ya Wapiga Kura; Kuandaa, kutayarisha, kuhifadhi na kuendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; Kufanya mapitio ya mipaka, idadi na majina ya Majimbo ya Uchaguzi na kuendesha Kura ya Maoni Zanzibar.

**Mafanikio ya Tume ya Uchaguzi:**

Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imefanikiwa kupata mafanikio yafuatayo:

*(i)* Kuimarika kwa ushirikiano kati ya Tume ya uchaguzi, taasisi mbali mbali, jamii inayoizunguka na wadau kwa ujumla. Vile vile, Kuongezeka kwa idadi ya wananchi wanaofatilia mitandao yetu ya kijamii, ambapo hadi sasa Tume ina wafuatiliaji (subscribers) 1225 kutoka 1139 na watazamaji (views) 91362.

*(ii)* Afisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar, inaendelea kutekeleza mradi wa kimaendeleo wa ujenzi wa jengo jipya na la kisasa la Afisi kuu ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar linalojengwa Maisara ambalo litaweza kumudu shughuli zake zote ikiwemo Shughuli zote za kuendesha Uchaguzi Mkuu badala ya kwenda kukodi ukumbi kwa ajili ya kutangaza matokeo, Studio kwa ajili ya kurikodi vipindi vyote vinavyosimamiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzaibar.

*(iii)* Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imefanikiwa kushiriki katika Maonesho ya Sita (6) ya Kilimo yaliofanyika katika viwanja vya Dole, Kizimbani Mkoa wa Mjini Magharibi ambapo huduma mbali mbali kwa wadau wa uchaguzi zilitolewa katika eneo la maonyesho.

**Changamoto za Tume ya Uchaguzi**

Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inakabiliana na changamoto zifuatazo:

*(i)* Uhaba wa maghala ya kuhifadhia vifaa vya Uchaguzi.

*(ii)* Uwepo wa majengo ya Afisi za Wilaya ambazo haziendani na hadhi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

*(iii)* Urasimu wa upatikanaji wa maeneo ambayo Tume imeomba kwa ajili ya ujenzi wa Afisi.Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imekuwa ikipata usumbufu katika kupatiwa maeneo ya ujenzi ya Afisi za

wilaya ambazo zitaendana na utendaji kazi zake. Urasimu huo umejitokeza kwa Wilaya ya Kaskazini B na Magharibi B hadi hii leo Tume ya Uchaguzi haijapata barua ya kupewa eneo kwa ajili ya ujezi wa Afisi hizo za Wilaya.

*(iv)* Mradi wa kimaendeleo kuwa nyuma ya muda uliopangwa kwa muda wa siku 10. Changamoto hii imetokana na kuwepo kwa mvua kubwa katika miezi ya Machi na Aprili 2024. Hali hii imesababisha kuchelewa kwa baadhi ya kazi katika ujenzi huo ambazo hazitofanyika vizuri wakati wa mvua kubwa. Kazi zenyewe ni uwekaji sawa kwa ardhi, kuweka zege katika ardhi ya chini, na kujenga msingi wa jengo. Hali hii impelekea kutofanyika baadhi ya kazi kwa muda uliopangwa.

**Maagizo ya Kamati kwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar**

*(i)* Kamati inaipongeza Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa kupata mradi wa maendeleo ya ujenzi wa Jengo jipya la kisasa ambalo litakuwa na nafasi ya kutosha ikiwemo ghala la kuhifadhia vifaa vya Uchaguzi. Hata hivyo, kamati inaishauri Tume kuanza kuandaa mikakati ya ununuzi wa vifaa vya Ofisi ili jingo litakapokamilika liweze kutumika mara moja.

*(ii)* Kamati pia imeridhishwa na hatua za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, katika mpango wake wa kujenga ofisi 10 za Wilaya ambazo zitaendana na hadhi ya Tume. Hasa kufuatia kupata viwanja na maeneo kwa Wilaya ya Kaskazini "A", Micheweni na Chake Chake, hata hivyo, kwa kuwa tayari viwanja hivyo vimeshapimwa kamati inashauri kuongeza hatua za kutafuta hatimiliki za maeneo hayo ili ujenzi huo uweze kuanza kwa haraka.

*(iii)* Aidha, Kamati inataka Tume kuzidisha kasi ya kuwasiliana na Taasisi zinazomiliki maeneo ambayo hayajapatiwa hati ili wapatiwe ridhaa ya maandishi itakayoonesha umiliki wa maeneo hayo licha ya kutoa barua za awali katika kufuatilia mchakato huo.

## 4.3 KAMISHENI YA KUKABILIANA NA MAAFA

Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa ni miongoni mwa Taasisi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ambayo imeanzishwa chini ya Sheria ya Kukabiliana na Maafa Nambari 1/2015. Kwa mujibu wa Sheria hii, Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa ndio taasisi yenye jukumu la kuainisha, kuimarisha na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya kukabiliana na maafa hapa Zanzibar.

**Changamoto za Kamisheni**

*(i)* Uhaba wa fedha ukilinganisha na mahitaji ya kazi za kukabiliana na Maafa ambapo mahitaji mengi hujitokeza nje ya mpango kazi;

*(ii)* Ongezeko la matukio ya majanga hasa majanga ya moto na mafuriko hali inayopelekea uhaba wa misaada ya kibinadamu kwa waathirika wa majanga hayo;

*(iii)* Uhaba wa wafanyakazi katika baadhi ya sehemu/vitengo vya Kamisheni na taaluma zinazoendana na masuala ya kukabiliana na maaafa; na

*(iv)* Uhaba wa vifaa vya kisasa vinavyotumika kwenye uokozi.

*(v)* Kutokufanyika kwa vikapo vya kamati za maafa za wilaya ambapo kwa mwaka huu ni wilaya moja tu ya Magjaribi ‘A’ ambayo imefanya vikao hivyo.

*(vi)* Kuwepo kwa ongezeko kubwa la majanga ya moto nchini.

**Maagizo ya kamisheni ya Maafa**

*(i)* Kamati inashauri kuanzisha mfuko maalumu utakaosaidia wakati kutokea maafa katika jamii ili kuepusha changaoto yan fedha wakati wa maafa.

*(ii)* Kamati inashauri Kamisheni kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya kujikinga na maafa pamoja na kuzidisha kasi ya kutoa tahadhari inapotokea viashiria vya maafa nchini.

*(iii)* Kamati inaishauri Kamisheni kutoa miongozo na ushauri kwa taasisi zinazosimamia mipango miji ili kusaidia kuepusha ujenzi holela ambao haufuati taratibu za kujikinga na maafa.

*(iv)* Mwisho, Kamati inaiasa jamii kujikinga na maradhi ya mripuko kwa kuweka mazingira safi na salama hususan katika vipindi vya mvua zamasika zinazokaribia kunyesha.

## 4.4 IDARA YA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA

Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa imeanzishwa mwaka 2010 ikiwa na jukumu la kuratibu na kusimamia Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na shughuli za Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa. Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa yanayoratibiwa na Idara hii ni Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar pamoja na ushiriki wa Viongozi na wananchi wa Zanzibar katika Sherehe za Uhuru wa Tanzania Bara.

Aidha, kwa upande wa shughuli za Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Idara inaratibu Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa, Maadhimisho ya Siku ya Kumbukumbu ya Siku ya Karume pamoja na shughuli nyengine kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa Namba 5 ya Mwaka 2019.

Kamati imeridhishwa na Utekelezaji wa kazi za Idara hii na inapenda kuchukua nafasi ya kuipongeza kwa dhati kabisa kwa kuweza kufanikisha maadhimisho ya Sherehe za miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Changamoto za Idara ya Sherehe na maadhimisho ya Kitaifa**

*(i)* Uchakavu mkubwa wa maduka yanayomilikiwa na Idara

ambayo yapo Mwanakwerekwe.

*(ii)* Mbali na ukarabati ulofanyika wa jengo la Idara bado ipo changamoto ya uhaba wa ofisi kulingana na idadi ya watendaji wa Idara.

*(iii)* Ukosefu wa Gari kwa ajili ya shughuli za kawaida za Ofisi.

*(iv)* Ubovu wa miundombinu ya barabara zinazoelekea katika baadhi ya makabujri ya waasisi wa mapinduzi katika vipindi vya mvua.

**Maagizo ya Kamati**

*(i)* Kamati inaishauri Serikali kuongeza nguvu katika Idara kwa kuwapatia fedha za kutosha katika uendeshaji wa ofisi.

*(ii)* Kamati inashauri Idara hii kupatiwa vifaa vya kisasa na wataalamu ambao watahusika katika matumizi ya vifaa hivyo.

*(iii)*Kamati inashauri Idara baada ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa barabara ya flyover Mwanakwerekwe waanze ujenzi wa jengo jipya la kibiashara ambalo litatumika kama chanzo cha mapato.

*(iv)*Kamati inashauri Serikali kuzijnega barabara zinazoelekea katika makaburi ya waasisi hususan barabara inayelekea katikakaburi la Marehemu mzee Abdallah Said Natepe.

## 4.5 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini ni Mpango wa Kitaifa ambao unatekelezwa kwa lengo la kuziongezea kaya za walengwa kipato, fursa na kuboresha upatikanaji wa mahitaji muhimu kama chakula, malazi na mahitaji ya huduma ya elimu na afya kwa watoto wa kaya za walengwa. Aidha, utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini unakwenda sambamba na Mikakati mbali mbali ya Serikali zetu katika kuhakikisha wananchi wanaendelea kutekeleza shughuli zao za kujiongezea kipato husika pamoja na kukuza uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mpango huu unaendelea kusisitiza katika kuhakikisha kaya za walengwa wenye uwezo wa kufanyakazi zishiriki kufanya kufanyakazi kupitia Miradi ya Kutoa Ajira za Muda kwa Walengwa pamoja na Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu katika sekta ya afya na elimu. Vile vile, Mpango unaendele kuwahamasisha wanakaya kuimarisha rasilimali watu (Watoto) kwa kuhakikisha wanapelekwa vituo vya afya (kliniki) na kuhudhuria skuli.

**Mafanikio ya Utekelezaji wa Programu Kuu**

Kwa ujumla Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kwa upande wa Zanzibar umeendelea kutekelezwa kwa mafanikio makubwa kwa kaya za Walengwa na jamii yote katika shehia zetu. Miongoni mwa mafanikio hayo ni:-

*(i)* Kuweza kutekeleza shughuli zote zilizopangwa kwa kipindi hiki cha utekelezaji.

*(ii)* Kuendelea na utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi katika sekta ya Afya na Elimu kwa shehia za Upenja na ambapo mradi wa Dahalia Kizimkazi Dimbani umekamilika.

*(iii)* Kaya zilizopatiwa ruzuku za Uzalishaji zimeendelea kutekeleza miradi yao kwa lengo la kuongeza vipato vya kaya husika.

*(iv)* Asilimia 99 ya Watoto wa Walengwa wameweza kutimiza masharti ya Elimu na Afya hivyo kuziwezesha kaya husika kupata ruzuku zinazohusiana na masharti ya elimu na afya.

*(v)* Mpango unawasaidia walengwa kupata mahitaji ya msingi yakiwemo chakula, vifa vya skuli kwa watoto wao.

*(vi)* Walengwa wameweza kujikwamua kwa shughuli za kujiwekea akiba na kuanzisha miradi ya kiuchumi ambayo inawasaidia kuongeza kipato cha kaya.

*(vii)* Walengwa wamepata ujuzi kupitia utekelezaji wa miradi ya kutoa ajira za muda na kutumia ujuzi huo katika kutatua changamoto za maeneo yao.

*(viii)* Kuboresha miundombinu ya huduma za kijamii zikiwemo huduma za afya na elimu. Mpango umewezesha ujenzi wa kituo cha afya kinyikani.

**Changamoto za Utekelezaji wa Programu**

Baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kwa Awamu ya Kwanza ni: -

*(i)* Idadi ndogo ya wananchi wanaojitokeza katika ujenzi wa miradi ya miundombinu maalumu inasababisha miradi hiyo kupungua kasi ya utekelezaji.

*(ii)* Baadhi ya walengwa kutohudhuria katika vituo vya malipo inapelekea kukosa taarifa muhimu na baadae kusimamishwa katika Mpango.

**Maagizo ya Kamati kwa Idara ya Uratib katika Mradi wa TASAF**

Katika utekelezaji wa mradi wa TASAF kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini, Kamati inashauri mambo yafuatayo: -

*(i)* Kamati inazipongeza Serikali zetu mbili ambazo ni SMZ na SMT kwa namna zinavyoshirikiana kuendesha mradi huu ambao umekuwa na maslahi makubwa kwa wananchi wetu. Shukran za pekee ziende kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Samia Suluhu Hassan na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Hussein Ali Mwinyi pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa TASAF ndugu Shedrack Mzirai kwa namna wanavyoendesha mradi huu kwa mafanikio makubwa.

*(ii)* Kwa kuwa awamu ya tatu ya mradi imekamilika na maandalizi kwa ajili ya awamu nyengine ya mradi yanaendelea; kamati inaomba wananchi kuwa watulivu na makini katika kuendeleza miradi yao midogo midogo ambayo waliibua kipindi kilichomalizika ili kutafakari miradi mipya ambayo itatekelezwa katika awamu mpya inayokuja.

*(iii)* Kamati inaishauri Idara ya uratibu kuzidisha kasi ya uchapaji kazi kwa mashirikiano makubwa inayoyapata kutoka Tanzania Bara na hivyo kufanya mradi huu kuwa maarufu na muhimu zaidi kwa wananchi.

*(iv)* Kamati pia inashauri Serikali zote mbili kuweka mazingira mazuri ya kupatikana kwa mradi wa awamu ya nne wa TASAF ili kuendelea kusaidia wananchi wetu.

## 4.6 OFISI YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ DODOMA

Ofisi hii ilianzishwa mwaka 1980 chini ya iliyokuwa Wizara ya Mipango na baadae kuhamishiwa Wizara ya Fedha na Mipango mwaka 1988 baada ya Wizara hizo mbili (2) kuunganishwa. Ofisi iliendelea kufanya kazi zake chini ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo hadi mwaka 2013 ilipohamishiwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kamati katika ufatiliaji wa kazi za Ofisi ya Uratibu imefurahishwa sana na namna inavyofanya kazi za kuzifikia kaya maskini pamoja na miradi ambayo wanayoisimamia.

**Mafanikio ya Ofisi ya Uratib**

*(i)* Kukamilisha na kuwasilisha taarifa ya miaka minne ya SMZ kuhusu Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020;

*(ii)* Kuanzisha Mfumo wa kielektroniki wa Kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali;

*(iii)* Kuratibu na Kuandaa Kikao cha Masuala ya Muungano kupitia Kamati ya Uchumi, Fedha na Biashara;

*(iv)* Kukamilisha Rasimu ya Awali ya Andiko la Kitabu cha Ripoti ya Tathmini ya Hali ya Siasa na Utendaji wa Serikali, Zanzibar;

*(v)* Kukamilisha Rasimu ya Awali ya taarifa ya Miaka miwili (2020 – 2022) ya Utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo;

*(vi)* Kukamilisha Rasimu ya Awali ya Andiko la Kitabu cha Hoja za Muungano zilizopatiwa Ufumbuzi; na

*(vii)* Kuendelea kusimamia Utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini.

**Changamoto za Ofisi ya Uratib wa Shughuli za SMZ Dodoma**

Katika utekelezaji wa shughuli zake, Ofisi inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Ukosefu wa usafiri kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji za Ofisi pamoja na wageni/viongozi wa Serikali;
*(ii)* Ubovu wa miundombinu ya majengo ya Ofisi (Dar es Salaam na Dodoma);
*(iii)* Kutokuwepo kwa ulinzi wa uhakika katika majengo ya Ofisi;
*(iv)* Uhaba wa watendaji hasa wenye kada maalum zinazolingana na majukumu ya Ofisi;
*(v)* Ushirikiano hafifu kwa baadhi ya taasisi katika kuratibu shughuli baina ya SMZ na SMT.

**Maagizo ya Kamati kwa Ofisi ya Uratib**

*(i)* Kamati inashauri Serikali kuongeza nguvu ya utendaji kwa Ofisi ya Uratib Dodoma kwa lengo la kuwapatia rasilimali zinazohitajika ikiwemo gari kwa ajili ya usafiri na watendaji ambao watakua msaada mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii.
*(ii)* Kamati inashauri taasisi za Zanzibar na Wazanzibari wanaoishi Tanzania Bara kuitumia Ofisi hii kwa lengo la kupata msaada wa kitaalamu lakini pia kukamilisha harakati za kiofisi zinazohitaji utekelezaji wa Zanzibar kwa upande wa Bara.

## 4.7 OFISI YA AFISA MDHAMINI PEMBA.

Lengo la jumla la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kuratibu shughuli za Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa upande wa Pemba. Aidha, malengo na mipango ya Ofisi imezingatia Dira ya Maendeleo ya 2050 na Mpango wa

Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP), Malengo ya Milenia (SDGs), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) ya mwaka 2020-2025, Maagizo ya Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa pamoja na Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Kwa mwaka 2024/2025 Ofisi kuu Pemba imetekeleza yafuatayo:**

*(i)* Kuratibu huduma za makaazi na shughuli za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais, Pemba;
*(ii)* Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba;
*(iii)* Kuratibu ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Pemba.
*(iv)* Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi sita
*(v)* Kuimarisha kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa Programu na miradi ya maendeleo iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba;
*(vi)* Kuratibu na kufuatilia shughuli za Serikali kwa upande wa Pemba
*(vii)* Kuratibu shughuli za kukabiliana na maafa Pemba;
*(viii)* Kuratibu masuala ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa.
*(ix)* Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa upande wa Pemba.

## 5. OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora inasimamia masuala ya Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Ofisi hii ina jumla ya Idara na Taasisi 11 zinazosimamiwa na Katibu Mkuu na Taasisi 01 inayopokea Ruzuku kutoka Serikalini. Idara na Taasisi hizo ni kama zifuatavyo:

*(a)* Idara ya Utumishi na Uendeshaji,

*(b)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,
*(c)* Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi,
*(d)* Wakala wa Serikali Mtandao,
*(e)* Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma,
*(f)* Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu,
*(g)* Idara ya Msaada wa Kisheria,
*(h)* Idara ya Utawala Bora,
*(i)* Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar,
*(j)* Ofisi ya Waqfu na Mali ya Amana,
*(k)* Afisi Kuu Pemba.

Aidha, Chuo cha Utumishi wa Umma *(IPA)* kinapokea ruzuku kutoka Serikalini ili kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

Vile vile, Wizara hii inasimamia Taasisi zinazojitegemea zifuatazo:

*(a)* Mahkama Kuu,
*(b)* Afisi ya Mwanasheria Mkuu (AGC),
*(c)* Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP),
*(d)* Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
*(e)* Tume ya Kurekebisha Sheria,
*(f)* Kamisheni ya Utumishi wa Umma,
*(g)* Tume ya Utumishi Serikalini,
*(h)* Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA).

Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imegawika katika sekta kuu tatu (3) ambazo ni Sekta ya Sheria, Sekta ya Uratibu wa Utumishi wa Umma na Sekta ya Utawala Bora.
*Sekta ya Sheria* inahusisha Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa haki, Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria, Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai, Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria na Programu ya Usimamizi wa Masuala ya dini. Programu

hizi zinatekelezwa kupitia Mahkama Kuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Tume ya Kurekebisha Sheria, Ofisi ya Mufti, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na Idara ya Msaada wa Kisheria.

## 5.1 MAHAKAMA KUU

Mahakama Kuu Zanzibar ina jukumu la kutafsiri sheria, kusikiliza kesi na kutoa uamuzi kufuatana na sheria za nchi. Vile vile, Mahakama ina jukumu la kusikiliza na kutoa uamuzi wa kesi zote zinazohusiana na masuala ya jinai na madai.

Kamati imeridhishwa na utendaji wa Mahakama ikiwemo Mahakama ya Kadhi Zanzibar kutokana na juhudi zake za kutoa uelewa kwa jamii kuhusu upatikanaji wa haki katika jamii kupitia vipindi vya Ijue Mahakama vinavyorushwa na Shirika la Utangazaji la ZBC sambamba na kutoa taaluma kwa jamii juu ya namna ya kuzifikia na kuweza kupata huduma katika Mahkama za Kadhi

Kwa Upande wa Kukuza mashirikiano na kuimarisha mahusiano kamati inaipongeza Mahkama kwa kuongeza ufanisi katika utendaji wa pamoja na kuhakikisha mashauri yanasikilizwa kwa wakati na kutolewa maamuzi kwa uweledi zaidi kwa mujibu wa sheria zilizowekwa.

**Mafanikio ya Mahakama Kuu**

*(i)* Mahakama imefanikiwa kufanya vikao vya msukumo wa kesi vilivyosaidia kutatua changamoto mbali mbali na kuhakikisha mafanikio yanapatikana.

*(ii)* Kumekuwepo na uwajibikaji kwa mahakimu uliosaidia umalizwaji wa kesi kwa haraka, hususani kesi za udhalilishaji, kwani malalamiko yanakua mengi iwapo kesi hizi zinapokaa muda mrefu bila kumalizika kwa haraka.

*(iii)* Wafanyakazi wa kitengo cha Tehama wamekua wakiendesha mafunzo kwa Mahakimu na wafanyakazi wa kada zote ili kupata kujua baadadhi ya kozi ambazo huzitumia katika shughuli za kazi zao.

*(iv)* kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa kada ya udereva pamoja na kada ya masjala yaliofanyika Iringa na Arusha.

*(v)* Kuendelea kwa utekelezaji wa ujenzi wa majengo ya Mahkama za Mikoa na Wilaya kwa kwa hatua za ukamilishaji wa majengo hayo, hivyo tutapata fursa ya kufanya kazi katika mazingira Rafiki na usalama sambamba Kuanza kwa ujenzi wa Mahkama Jumuishi iliopo Mabaoni Wilaya ya Chake – Chake, Pemba.

*(vi)* Ushirikiano wa Serikali na wadau unaopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Mahkama ya Zanzibar.

*(vii)* Uanzishwaji wa Kitengo cha Kumbukumbu ya Uhifadhi wa Majalada yaliyomalizika, hii imesaidia kwa kiasi kikubwa suala la utunzaji wa majalada ambayo yamemalizika na kurahisisha uwekaji wa kumbukumbu mbali mbali kulingana na miaka yake.

**Mafanikio ya Mahkama ya Kadhi:**

Mahkama ya Kadhi Zanzibar ikiendelea kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na;

*(i)* Kutangazwa rasmi kuanza kutumika Sheria mpya ya Mahkama za Kadhi, Nam. 8 ya 2023;

*(ii)* Uteuzi wa idadi ya ziada ya Ulamaa wa Mahkama Kuu kwa lengo kuondoa mrundikano wa kesi rufaa pia kuharakisha usikilizaji wa rufaa mpya za Mahkama ya Kadhi katika ngazi ya Mahkama Kuu;

*(iii)* Kutangazwa rasmi kuanza kutumika Kanuni za Mahkama za Kadhi (Mwenendo na Taratibu) za 2024, kanuni ambazo zinakwenda kutafsiri na kurahisisha utekelezaji wa Sheria ya

Mahkama za Kadhi, Nam. 8 ya 2023 katika uendeshaji wa mashauri;

*(iv)* Uteuzi wa Kadhi wa ziada katika ngazi ya Mahkama ya Kadhi ya Rufaa;

*(v)* Uteuzi wa Makadhi watano wa Mahkama za Kadhi za Mkoa, kwenda kuanzisha ngazi mpya ya Mahkama za Kadhi Zanzibar kwa mujibu ya Sheria mpya ya Mahkama za Kadhi;

*(vi)* Kuanzisha Kamati ya Kusukuma mbele Mashauri katika Mahkama za Kadhi; na

*(vii)* Kuwalipia wafanyakazi wawili kwenda kuongeza taalumu katika ngazi ya Shahada ya Sheria na Sharia.

**Changamoto za Mahkama Zanzibar**

Mbali ya kuwepo kwa mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, Mahkama inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Uhaba wa vyombo vya usafiri katika utekelezaji wa majukumu ya Mahakama hususan kisiwani Pemba ambapo gari moja iliyopo hutumiwa na viongozi wote wa mahakama wanaofika kisiwani Pemba.

*(ii)* Ufinyu wa bajeti unapelekea changamoto za utekelezaji kwa baadhi ya shughuli za Mahkama na hivyo kupelekea mahakama kuwa na ongezeko la madeni.

*(iii)* Uhaba wa wachapaji ambapo unapelekea kuchelewa kutoka kwa mienendo ya kesi.

**Changamoto za Mahkama Zanzibar**

Licha ya kuwepo kwa mafanikio, Mahkama ya Kadhi imekuwa ikikabiliana na changamoto za hapa na pale ambazo kimsingi zimekuwa

ni fursa za kuzifanyia kazi katika kuhakikisha malengo yanafanikiwa. Miongoni mwa changamoto nzito ni pamoja na:

*(i)* Uchache wa Makadhi pamoja na wasaidizi wa Makadhi kulinganisha na wingi wa mashauri na zaidi baada ya kuanza kutumika kwa Sheria mpya na kuanzishwa kwa ngazi ya Mahkama ya Kadhi ya Mkoa; na

*(ii)* Ukosefu wa usafiri wa gari kwa Naibu Kadhi Mkuu pamoja na Kadhi wa Rufaa Pemba.

**Maagizo ya Kamati kwa Mahakama**

*(i)* Kamati inashauri Mahakama kuongeza juhudi katika kusikiliza mashauri ya kesi kwa wakati na kuwapatia wananchi mienendo ya kesi zao ndani ya muda mfupi.

*(ii)* Kamati inashauri Serikali kuandaa utaratibu maalumu ya kutumikia adhabu jamii kwa watoto ambao wapo chini ya miaka 17 na watu wazima wenye vifungo vya chini ya mwaka mmoja. Aidha, kamati inaishauri Mahakama kutummia adhabu mbadala kwa makosa madogo madogo kama wizi wa mazao kuliko kutoa adhabu ya kifungo kwani kunaongeza idadi kubwa ya wafungwa na gharama za uendeshai katika magereza.

*(iii)* Kamati inaipongeza mahakama kuu kwa kuanzisha miradi ya ujenzi wa Mahakama za Mikoa na Wilaya ambapo zimeshafikia asilimia 85 kukamilika kwake.

*(iv)* Aidha, kamati inashauri Ofisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora kusimamia na kufuatilia kwa karibu ujenzi wa Mahakama Jumuishi inayojengwa Mfikiwa Wilaya ya Chake – Chake ili kukamilika kwa wakati na kuondoa changamoto za mahakama ya Chake – Chake ambayo kwa imeshazidiwa na matumizi.

*(v)* Mwisho, kamati inaishauri mahakama kuzidisha kasi ya mafunzo kwa watumishi wake kwa lengo la kuongeza ufanisi katika masuala mazima ya utendaji wa mahakama.

Kwa upande wa Mahkama za Kadhi Kamati inaagiza yafuatayo:

*(i)* Kamati inaipongeza Mahakama ya Kadhi kwa kuanza kutumia Sheria mpya na kuanzishwa kwa ngazi ya Mahkama ya Kadhi ya Mkoa. Hata Hivyo kamati inaihauri Serikali Kuajiri Uchache wa Makadhi pamoja na wasaidizi wa Makadhi ili kuondosha uhaba uliopo wataosaidia kumaliza mashauri kwa wakati.

*(ii)* Kamati inaiomba Serikali kulitafutia ufumbuzi tatizo la wa usafiri wa gari kwa Naibu Kadhi Mkuu pamoja na Kadhi wa Rufaa Pemba ili kuimarisha ufatiliaji wa majukumu katika ngai za wakubwa.

## 5.2 AFISI YA MWANASHERIA MKUU

Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 ndio Mshauri Mkuu wa Serikali kwa mambo yote ya Kisheria.

Kamati imeridhishwa na utendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa jitahada zake za kusimamia na kuendeleza majukumu yake ya na shughuli mbalimbali za kisheria ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri wa kisheria kwa Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali, Uandishi wa Miswada ya Sheria, Kusimamia Kesi na Mashauri ya madai kwa niaba ya Serikali, Kuandaa Hati za Nyaraka za Kisheria, Kusimamia Mikataba yote ambayo Serikali ni sehemu ya Mikataba hiyo na kufanya mambo mengine ya Kisheria kwa niaba ya Serikali.

**Mafanikio ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu**

*(i)* Kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali waliopo Afisi ya Pemba kwa lengo la kuisaidia Serikali kwa masuala mbali mbali ya kisheria;

*(ii)* Afisi imeweza kuisaidia jamii/wananchi katika kuwapatia elimu na kutatua changamoto mbali mbali za kisheria; na

*(iii)* Kusaidia kujenga mashirikiano baina ya taasisi za Serikali na Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika utekelezaji wa majukumu ya Afisi.

**Changamoto zinazoikabili Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Zanzibar**

Mbali ya kuwepo kwa mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, Afisi ya Mwanasheria Mkuu inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Ucheleweshaji wa taarifa zinazoombwa na Afisi kutoka taasisi zinazolalamikiwa hali inayopelekea uchelewaji wa kutoa majibu kwa walalamikaji.

*(ii)* Kukosekana kwa usafiri wa Gari Afisi ya Mwanasheria Mkuu Pemba ambao kwa sasa wanatumia honda hali ambayo sio salama kwa mawakili wanapokwenda Mahakamani.

*(iii)* Kwa upande wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Pemba ni kukosa mashirikiano katika upatikanaji wa taarifa juu ya malalamiko yanayopelekwa Afisini, jambo linalopelekea kutomalizika kwa malalamiko na kufunguliwa kwa kesi zisizokuwa na tija kwa Serikali.

**Maagizo ya Kamati kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu**

*(i)* Kamati inaziomba Taasisi ambazo zinalalamikiwa kuharakisha majibu ya walalamikaji ili kuwarahisishia Afisi ya Mwanasheria kumaliza mashauri yao kwa wakati.

*(ii)* Kamati inashauri Afisi ya Mwanasheria kuliangalia suala la usafiri kwa upande wa Pemba ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

## 5.3 AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka inaendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 56A cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 (kufuatia Marekebisho ya nane yaliyofanywa Mwaka 2002) na kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria Nambari 2 ya Mwaka 2010 (Sheria ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar)

Sambamba na hayo, Kamati imeridhishwa na utendaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kutokana na **mafanikio** makubwa yalipatikana yakiwemo:

*(i)* Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kupitia Mradi wa kupambana na makosa makubwa ya kupanga (Serious Organised Crime – SOC) iliendesha mafunzo maalumu kwa Waendesha Mashtaka na taasisi nyengine za haki jinai yanayohusiana na ushahidi wa kielektroniki katika kuthibitisha makosa ya Rushwa, uhujumu uchumi na utakatishaji wa fedha haramu.

*(ii)* Afisi ilifanya kikao cha pamoja na wakuu wa Upelelezi wa Mikoa pamoja na wakuu wa Usalama Barabarani wa Mikoa na Wilaya, Mamlaka ya Usafiri na usalama barabarani.

*(iii)* Kufanya mkutano wa robo mwaka wa kukutana na wadau wa haki jinai unaojumuisha wakuu wa Taasisi zinazohusiana na usimamizi wa haki jinai wakiwemo Mahkama, Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Madawa ya Kulevya, Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi, Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkemia Mkuu na Chuo cha Mafunzo.

*(iv)* Kuendelea kupunguza muda wa kukaa majalada ya uchunguzi Afisini kutoka siku 14 hadi siku mbili tu.

*(v)* Kuendelea na utaratibu wa kukutana na Mahakimu kabla na baada ya kuanza usikilizaji wa mashauri mahakamani kila siku.

*(vi)* Kuendelea na utaratibu wa kukaa na mashahidi siku moja kabla ya kusikilizwa kesi Mahakamani ili kurahisisha usikilizwaji wa kesi.

*(vii)* Kufanya mafunzo ya kuwajengea uwezo Wanasheria.

*(viii)* Kufanya mafunzo kuhusu Sheria na Kanuni za Utumishi kwa wafanyakazi wote.

*(ix)* Kuimarika kwa mashirikiano kati ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mamlaka za upelelezi zikiwemo Polisi, ZAECA na Uhamiaji pamoja na wadau wote wa haki jinai.

*(x)* Kukutana na Wakuu wa Vitengo na Divisheni katika kukumbushana uwajibikaji kazi wa kila siku.

*(xi)* Afisi imefanikiwa kukodi jengo kwa ajili ya Afisi ya Mkoa Kaskazini.

*(xii)* Kukamilisha utayarishaji wa Michoro kwa ajili ya ujenzi wa Afisi za Mikoa Kaskazini na Kusini.

**Changamoto za Afisi ya Mkurugenzi wa Mashataka Zanzibar (DPP):**

Pamoja na kuwepo kwa mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, Afisi ya DPP

inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Afisi inakabiliwa na Uhaba wa watendaji wakiwemo (waendesha Mashtaka, Mtakwimu, IT)

*(ii)* Uchache wa vitendea kazi ikiwemo vyombo vya usafiri.

*(iii)* Kuchelewa kupatikana kwa baadhi ya maslahi ya wafanyakazi kwa wakuu wa Vitengo na Divisheni kulingana na muundo wa Afisi uliopitishwa.

*(iv)* Mashahidi wenye umri kati ya miaka 15 hadi 17 kwenye makosa ya udhalilishaji wanawake Kukataa kutoa ushahidi kwa mtindo mpya wa kutowatambua washtakiwa wakiwa Mahakamani.

*(v)* Upatikanaji wa fedha za uendeshaji wa Ofisi (OC) usioendana na mahitaji ya Mpangokazi.

**Maagizo ya Kamati kwa ofisi ya DPP**

*(i)* Kamati inashauri Wizara kuliingia kati tatizo la uhaba wa watendaji kwani limekuwa la muda mrefu kwa kuwapa kibali cha uajiri utaosaidia utekelezaji wa majukumu ya Afisi kuliko lile la kuazima wanasheria wa taasisi nyengine.

*(ii)* Kamati inashauri Afisi kuongeza bidii ya kutenga fedha katika bajeti yake kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi.

*(iii)* Kamati pia inaishauri Serikali kufuatilia kwa ukaribu tatizo la usafiri na kulipatia ufumbuzi kwa kadri hali inavyoruhusu;

*(iv)* Kamati inaishauri Serikali kuifanyia mapitia Sheria ya Ushahidi ambayo itawabana wale wote wanaokataa kutoa ushahidi.

*(v)* Kamati inashauri kulitafutia ufumbuzi tatizo la maslahi ya wakuu wa vitengo hasa Mkuu wa chuo ili kuwapa nguvu ya utendaji kazi.

## 5.4 SKULI YA SHERIA ZANZIBAR

Skuli ya Sheria Zanzibar imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria namba 13 ya mwaka 2019.

**Mafanikio ya Skuli ya Sheria**

*(i)* Jumla ya waombaji 44 wamefanikiwa kuomba kujiunga na Skuli ya Sheria. Kati ya hao, 34 ni waombaji kwa ngazi ya mawakili na 10 kwa ngazi ya mavakili ambao wanatarajiwa kuanza masomo yao tarehe 20 Januari, 2025;

*(ii)* Skuli ya Sheria imefanikiwa kuaza masomo kwa Kundi la Kwanza kwa wanafunzi 15 wa ngazi ya Vakili. Wanafunzi hao, watapatiwa masomo ya darasani kwa muda miezi mitatu (3);

*(iii)* Skuli ya Sheria imefanikiwa kufanya mitihani ya kupima ufahamu binafsi (ICA) pamoja na Mitihani ya (OPE 1) kwa wanafunzi 15 wa kundi la Kwanza (First Cohort) la Vakili kwa mwaka wa masomo 2024 – 2025.

*(iv)* Pia, Skuli ya Sheria imefanikiwa kufanya mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi 27 wa Kundi la Tatu. Mafunzi hayo yalifanyika katika Taasisi mbali mbali za Serikali ikiwemo Mahkama Kuu ya Zanzibar, Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na Sekta Binafsi.

**Changamoto za Skuli ya Sheria Zanzibar:**

Pamoja na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa, Skuli ya Sheria imekabiliwa na changamoto zifuatazo;

*(i)* Ukosefu wa Jengo la Kufundishia.

*(ii)* Ukosefu wa vitabu vya Maktaba Pamoja na kwamba Skuli inaendela na ufundishaji wa masomo kwa mwaka wa masomo 2024, Skuli imekabiliwa na tatizo la kutokuwepo Maktaba inayojitosheleza kwa wanafunzi waliopo masomoni.

*(iii)* Skuli imechukua hatua za awali kuanzisha Maktaba ya Skuli iliyopo katika jengo la Ofisi za Kamisheni ya Utumishi Mwanakwerekwe licha ya kwamba Maktaba hiyo ndogo haina vitabu vya kutosha.

*(iv)* Ukosefu wa Jengo la kudumu la Ofisi za skuli ambapo kwa kipindi husika Skuli ya Sheria inatumia Jengo la kukodi Michezani

**Maagizo ya Kamati kwa Skuli ya Sheria Zanzibar**

*(i)* Kamati inaishauri Serikali kuipatia Skuli majengo yake ya kudumu ambayo yatasaidia kufikia malengo ya Skuli licha ya harakati hizi kuanza lakini bado juhudi za makusudi zinahitajika ili kufikia malengo kwa wakati;

*(ii)* Skuli ifanye jitihada ya kuweka maktaba yenye vitabu vya kutosha kwa ajili ya wanafunzi ilikuwarahisishia katika masomo yao na kwa kutumia Maktaba ya Mtandao (E- learning);

*(iii)* Kamati inaishauri Serikali Skuli ifuatilie kikamilifu suala la usafiri na kutatua changamoto hii kwa wakati;

## 5.5 IDARA YA KATIBA NA MSAADA WA KISHERIA

Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria ilianzishwa rasmi mwaka 2019 kwa mujibu wa Sheria ya Msaada wa Kisheria Namba 13 ya 2018 na imepewa mamlaka ya kuratibu, kuendeshana kusimamia utoaji wa msaada wa kisheria, Zanzibar.

**Mafanikio ya Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria.**

katika kutekeleza majukumu yake Idara imefanikiwa kujenga Uwelewa juu ya upatikanaji wa msaada umeengezeka hasusan katika maeneo ya vijijini pamoja na Mashirikiano kwa taasisi za Serikali na binafsi katika masuala ya msaada wa kisheria yameengezeka.

**Changamoto za Idara**

*(i)* Ukosefu wa Mawakili wa kusimamia kesi za kujitolea (pro bono cases) hasa katika ngazi ya rufaa.

*(ii)* kuwepo kwa baadhi ya mapungufu katika mfumo wa usajili kwa watoa huduma za msaada wakisheria unaopelekea kukosekana kwa baadhi ya taarifa na mfumo kutokufanya kazi uzuri.

*(iii)* Muamko mdogo wa wananchi katika kuhudhuria mikutano ya jamii hususan wanaume.

**Maagizo ya Kamati kwa Idara**

*(i)* idara imeandaa Kanuni ya Malipo ya Wakili na Vakili kwa kushughulikia changamoto hii, hata hivyo, kwa sasa Mahkama haina bajeti ya kuwalipa Mawakili hao.

*(ii)* Idara kwa kushirikiana na Kitengo cha TEHAMA cha Wizara ipo katika kuufanyia marekebisho mfumo wa usajili kwa lengo la kuuboresha kwa kuingiza taarifa muhimu ambapo hapo awali hazikuwemo.

*(iii)* Wizara kwa kushirikiana na Taasisi za Watoa huduma za msaada wa kisheria inaendelea kuhamasisha wananchi kuhudhuria mikutano ya jamii inayohusu masuala mbali mbali ya msaada wa kisheria

## 5.6 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA ZANZIBAR

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imeanzishwa kwa Sheria nambari 2 ya mwaka 2007 ikiwa na majukumu ya kusimamia na kuendesha Mali za Wakfu na Amana, kuendesha Mirathi ya marehemu Waislamu, pamoja na kuratibu shughuli za Hijja na suala zima la ukusanyaji na ugawaji wa Zakka, Sadaka na Misaada ya Kheri. Kimuundo Kamisheni ya Wakfu inaundwa na Bodi ya Uongozi, Katibu Mtendaji, Idara nne na Divisheni sita.

**Mafanikio ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana:**

*(i)* Kamisheni ya Wakfu imefanikiwa kuzikagua nyumba 11 inazozisimamia. Nyumba 9 za wakfu na 2 za amana. Pia imefanikiwa kuzikagua shamba 12 za wakfu.

*(ii)* Aidha, Ofisi yetu ilitakiwa kukusanya jumla ya Tsh 10,229,250 ikiwa ni mapato ya urithi (0.25%), na kufanikiwa kukusanya jumla ya Tshs 5,417,985.74 sawa na asilimia 53 ambazo huchangiwa katika mfuko Mkuu wa Serikali na tayari zimeshawasilishwa Wizara ya Fedha.

*(iii)*Ofisi imefanikiwa kufanya mikutano miwili inayohusu elimu ya zakka kwa wafanyabiashara wa Wilaya ya Chake Chake na Wete. Pia kwa kushirikiana na Jumuiya ya Taasisi za Hijja Zanzibar (UTAHIZA) elimu ya ibada ya Hijja, Zakka na Mirathi ilitolewa katika Msikiti wa Miembeni Chake Chake, Machomanne Chake Chake, Chanjamjawiri na Ole Kianga pamoja na makongamano yaliyofanyika katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Wete, Skuli ya Konde, Skuli ya Madungu na ukumbi wa Umoja ni Nguvu Mkoani.

**Changamoto za Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar**

Sambamba na mafanikio yaliyopatikana katika Ofisi hii, bado Kamisheni inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Baadhi ya kesi za mirathi kuchukua muda mrefu kumalizika ambapo hii inasababishwa na warathi wenyewe.

*(ii)* Licha ya Elimu ambayo inaendelea kutolewa, bado baadhi ya wanajamii kuwa na uelewa mdogo juu ya kuitumia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana katika masuala ya mirathi, wakfu, zakka na Hijja.

*(iii)* Jamii kutorithi kwa wakati au kutorithi kabisa kinyume na maamrisho ya Dini yetu ya Kiislamu ambapo hupelekea migogoro mingi ya mirathi katika jamii,

*(iv)* Familia nyingi kushindwa kuitumia Ofisi hii kwa lengo la kufanya mirathi kisheria na mambo mengine yanayohusiaka;

*(v)* Kutokufanyiwa marekebisho Sheria ya Kamisheni ya Wakfu kwa muda sasa ambapo mabadiliko mengi ya kiutendaji yanahitajika.

**Maagizo ya Kamati kwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.**

*(i)* Hatua ambazo zinachukuliwa ni kutoa elimu kwa jamii ambazo zina migogoro kabla ya kufanya Mirathi.

*(ii)* Kamisheni izidishe bidii katika kutoa elimu ya mirathi kwa jamii ili iweze kurithiwa kwa wakati,

*(iii)* Kamati inahimiza kuajiri vijana wa kutosha wakiwemo wataalamu wa mirathi na ili kuwawezesha kutoka hatua waliyosasa na kwenda hatua nyengine ya kiuzalishaji baada ya kupata wataalamu wa kiuchumi kutoka Serikalini,

*(iv)* Kamati inaiomba Seriali kuharakisha marekebisho ya Sheria ambayo yamechukua muda mreefu sasa ili iweze kukidhi haja ya masuala yote ya mirathi na mambo mengine.

## 5.7 OFISI YA MUFTI MKUU ZANZIBAR

Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar kwa mwaka 2024/2025, imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kutoa fatwa za masuala mbalimbali, kutatua migogoro, kutoa miongozo ya kidini kwa wananchi, kuratibu na kusimamia vikao vya Kamati ya Kitaifa ya kuthibitisha kuandama kwa Mwezi, kufanya ziara katika misikiti na Madrasa, kutoa mafunzo ya

maadili ya ndoa kwa wananchi, mafunzo ya ualimu kwa walimu wa Madrasa mafunzo kwa wasimamizi wa ndoa na kutoa ithibati kwa waliosilimu.

**Mafanikio ya Ofisi ya Mufti Mkuu**

*(i)* Kukamilisha ujenzi wa jengo la Mufti kwa Upande wa Unguja uliopelekea kuondosha tatizo la ufinyu wa nafasi.

*(ii)* Kuendelea kutoa elimu kwa kutumia vyombo vya habari.

*(iii)* Kuimarika kwa mashirikiano baina ya Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na taasisi mbalimbali za kidini.

**Changamoto za Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar**

Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Ofisi inakabiliwa na tatizo la Uhaba wa samani za Ofisi pamoja na vitendea kazi kama vile Kompyuta, Fotokopi, Printa nk.

*(ii)* Uwepo wa migogoro ya misikiti na Madrasa.

*(iii)* Ufinyu wa nafasi za kufanyia kazi kwa Ofisi ya Mufti Mkuu Pemba.

**Maagizo ya Kamati kwa Ofisi ya Mufti Mkuu**:

*(i)* Kamati inaipongeza Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar kwa kufanikisha ujenzi wa jengo liliopo Mazizini. Hata hivyo kamati inaishauri kuitunza tunu hiyo ya jengo sambamba na kuendelea na utaratibu wa kuwajengea watendaji wa Ofisi ya Pemba jengo ninaloendana na hadhi yake.

*(ii)* Kamati inaipongeza Ofisi ya Mufti kwa jitihada zake za kupunguza migogoro ya misikiti na Madrasa hata hivyo, inaisisitiza isichoke kutoa elimu juu ya athari za migogoro inayoendelea ambayo bado haijapatiwa ufumbuzi wake.

*(iii)*Kamati inaishauri Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar isichoke kuchukua hatua na kutoa miongozo ya kidini wakati wote wanapoona inafaa kufanya hivyo.

*(iv)*Kamati inashauri kuharakisha suala la migogoro mbali mbali ambayo inaletwa kwao ili iweze kumalizika kwa muda mfupi.

*(v)* Kamati inaelekeza Ofisi ya Mufti kuongeza vipindi vya kuelimisha jamii juu ya masuala mbali mbali ya dini na kupitia hutba za sala za ijumaa wanazoziandaa.

*(vi)* Kuomba kuongezewa fedha za matumizi ya kawaida (OC) kwa ajili ya kununua samani za Ofisi.

*(vii)* Ofisi imeshapata hati ya kiwanje kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi na kwa sasa imo katika hatua ya kuandaa mchoro.

## 5.8 TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Tume ya Utumishi Serikalini ni chombo kinachojitegemea kilichoanzishwa na Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 chini ya kifungu 117 Toleo la 2010 na kifungu 33 cha Sheria ya Utumishi wa Umma nambari 2 ya mwaka 2011. Tume kwa ujumla ina jukumu la kusimamia Utumishi katika Serikali kwa uadilifu na kufuata misingi ya Utawala Bora.

### Changamoto za Tume ya Utumishi Serikalini

Ofisi ya Tume ya Utumishi Serikalini inakabiliwa na changamoto ikiwemo: -

*(i)*Ukosefu wa jengo la ofisi ya kudumu jambo ambalo linaifanya Taasisi hii kuwa ya kuhamahama mwaka hadi mwaka na hivyo kupelekea usumbufu mkubwa kwa watendaji wake na wananchi wanaohudumiwa.

*(ii)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri katika utekejelezaji wa shughuli za Tume.

*(iii)* Uhaba wa fedha za matumizi mengineyo (OC) jambo ambalo linaifanya Tume kushindwa kutekeleza kwa ukamilifu baadhi ya mipango yake ikiwemo kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika taasisi za umma.

**Maagizo ya Kamati kwa Tume ya Utumishi Serikalini**

*(i)* Kamati inaishauri uongozi wa ofisi kuendelea na jitihada za utafutaji wa ofisi ya kudumu kwa Tume ili kumaliza kabisa changamoto hii kama ilivyo kwa taasisi nyengine za umma.

*(ii)* Kamati inashauri wizara kusimamia upatikanaji wa vyombo vya usafiri kwa Tume ili kusaidia utekelezaji wa majukumu yake ufanisi zaidi.

*(iii)* Kamati inaishsauri Srikali kujitahidi kuingiza fedha za matumizi kwa wakati kwa namna wanavyoomba katika kufanikisha majukumu yao.

## 5.9 CHUO CHA UTAWALA WA UMMA (IPA)

Chuo cha Utawala wa Umma Zanzibar kimeanzishwa kwa Sheria Nambari 1 ya Mwaka 2007 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2022 kikiwa na lengo na majukumu ya msingi ya kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Umma na binafsi, kufanya tafiti na kutoa huduma ya ushauri elekezi.

**Mafanikio ya Chuo cha Utawala wa Umma.**

*(i)* kuendelea kutembelea taasisi mbalimbali za Serikali juu ya kushajihisha uwepo wa fursa kadhaa za mafunzo ya watumishi Chuoni.

*(ii)* Kufanya Tafiti katika Utumishi wa Umma na kubaini mapungufu na mahitaji yaliyopo katika Utumishi na kuandaa programu za Mafunzo ya kujenga uwezo ili kuondoa mapungufu na mahitaji katika Sekta za Umma.

*(iii)* Kutoa huduma za itifaki na maandalizi ya mikutano kwa Taasisi mbalimbali.

*(iv)* Kutoa huduma ya Ushauri elekezi katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kupata Rasilimali watu wenye sifa na kuimarisha utoaji wa huduma bora nchini.

*(v)* Kundelea Kutoa Mafunzo ya Shahada ya kwanza kutokana na mahitaji ya kiutumishi

**Changamoto za Chuo cha Utumishi wa Umma (IPA)**

Licha ya mafanikio ambayo Chuo kimeyafikia kwa mwaka huu, lakini bado zipo changamoto ambazo zinahitaji mikakati maalumu ya kuweza kuzitatua. Miongoni mwao nikama zifuatazo:

*(i)*Ufinyu wa nafasi za kufanyia kazi na ukosefu wa madarasa ya kufundishia kwa upande wa kampasi ya Pemba.

*(ii)* Kuwepo kwa Idadi ndogo ya watumishi wanaohudhuria katika mafunzo ya kujenga uwezo, elekezi na wastaafu watarajiwa.

*(iii)*Uwepo wa madeni ambayo chuo inayadai kupitia taasisi za umma zenye kupatiwa mafunzo ya awali kwa watumishi wao wapya.

**Maagizo ya Kamati kwa Chuo cha Utumishi wa Umma (IPA)**

*(i)*Kamati inakishauri Chuo kuongeza jitihada za kuomba mradi wa ujenzi wa jengo jipya lenye kukidhi mahitaji ya Utawala kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

*(ii)* Kamati inaushauri uongozi wa chuo kuongeza jitihada za kupita katika taasisi mbali mbali za umma na binafsi kwa lengo la kushajihisha upatikanaji wa fursa mbalimbali za mafunzo kwa watumishi wa Umma.

*(iii)*Pia, chuo kiendelee kufuatilia taasisi za umma ambazo inadai ili kuweza kufanya mrejesho wa fedha zinazotakiwa kulipa.

## 5.10 KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Kamisheni ya Utumishi wa Umma imeanzishwa kutokana na matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984, Ibara ya 116, Toleo la mwaka 2010. Ibara hiyo imeitambua Kamisheni kuwa ni chombo cha juu kwa Tume zote za Utumishi na kuipa jukumu la kusimamia na kuratibu masuala yote ya Utumishi wa Umma wa Zanzibar. Aidha, kazi uwezo na majukumu ya Kamisheni yamefafanuliwa zaidi na Sheria ya Utumishi wa Umma Nambari 2 ya Mwaka 2011.

Majukumu ya Kamisheni Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Nambari 2 ya mwaka 2011 Kumshauri Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa BLM kuhusu mambo yote ya Utumishi wa Umma, yakiwemo: -

*(i)* Uteuzi wa viongozi na watendaji wakuu;
*(ii)* Miundo ya Taasisi za Umma;
*(iii)* Kuanzishwa, kuondoa, kuunganishwa Taasisi za Umma au kupanga Wizara;

**Changamoto za Kamisheni ya Utumishi wa Umma**

Pamoja na mafanikio makubwa ambayo yamepatikana katika utekelezaji wa shughuli za Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo: -

*(i)* Kamisheni inakabiliana na changamoto ya kuimarisha Utumishi wa Umma ili kuwa na tija kwa kutoa huduma bora na mabadiliko ya fikra na utamaduni wa watumishi.
*(ii)* Ukosefu wa fedha za matumizi mengineyo na hivyo kupelekea Kamisheni kushindwa kutekeleza mipango yake kwa wakati.

**Maagizo ya Kamati kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma**

*(i)* Maslahi ya watendaji wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma yaboreshwe ili kwenda sambamba na majukumu wanayoyatekeleza.

*(ii)* Katika kujenga Utumishi ulio bora na wenye tija kwa wananchi, watendaji wa Serikali na Mashirika yasio ya Kiserikali ni lazima yakubaliane na miundo ya kiutumishi iliyopo ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

*(iii)* Kamati inaishauri Kamisheni kuzifuatilia kwa kina Tume za Utumishi ili kuhakikisha zinatenda haki na zinawasimamia watumishi katika kutimiza wajibu wao kwa jamii.

*(iv)* Kamisheni ihakikishe inaidhinisha miundo ya taasisi ambazo zina sababu za msingi kufanya mabadiliko na sio kufanya mabadiliko kwa kufuata utashi wa wakuu wa taasisi au kuangalia upande mmoja wa maslahi ya taasisi husika.

*(v)* Aidha, Kamati inaigiaza Kamisheni kufuatilia kikamilifu Taasisi zote ambazo zimeshaidhinishiwa miundo mipya na kuona utekelezaji wake. Hata hivyo, ni vyema ukawepo mpango maalumu wa ukaguzi kwa kila mwaka kwa taasisi zote za umma.

## 5.11 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR (ZAECA)

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ni Taasisi ya Serikali iliyo huru na inayojitegemea, iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4(1) cha Sheria nambari 5 ya mwaka 2023, yenye Makao Makuu yake Unguja na Ofisi mbili (2) za Mikoa zilizopo Pemba. Mamlaka hii ina majukumu mbali mbali kama yalivyoelezwa chini ya kifungu cha 5(1) Sheria nambari 5 ya mwaka 2023.

Katika utekelezaji majukumu hayo yamegawika katika misingi mikuu mitatu ambayo ni: -

*(i)* Kutoa elimu kwa jamii juu ya kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi.
*(ii)* Kufanya udhibiti juu ya matendo yote yanayoashiria kuwepo kwa mianya ya rushwa na uhujumu wa uchumi.
*(iii)* Kufanya uchunguzi juu ya tuhuma mbali mbali zinazohusiana na viashiria vya rushwa na uhujumu uchumi.

**Mafanikio ya ZAECA**

*(i)* Ofisi za ZAECA Mikoa ya Pemba imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kukuza uelewa kwa wananchi kwa kutoa elimu jambo ambalo limepelekea wananchi wengi kutoa na kuripoti taarifa za vitendo vya rushwa vinavyotokea katika jamii zetu,

*(ii)* Pia Mamlaka imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuongeza mashirikiano na Taasisi za Serikali na binafsi jambo ambalo linapelekea Mamlaka kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa zaidi.

**Changamoto zinazoikabili ZAECA**

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana bado zipo changamoto mbalimbali katika mapambano dhidi ya rushwa. Miongoni mwa changamoto hizo ni: -

*(i)* Uhaba wa vitendea kazi ikiwemo vifaa vya uchunguzi, n.k.

*(ii)* Uhaba wa wataalamu.

*(iii)* Muhali kwa wananchi katika kutoa taarifa zinazohusiana na rushwa na uhujumu wa uchumi.

**Maagizo ya Kamati**

Kamati inaipongeza Mamlaka katika mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi ambapo juhudi kubwa zinahitajika kwa Serikali na sekta binafsi kushirikiana pamoja kutokomeza adui huu katika nchi yetu. Sambamba na hayo, kamati yetu inashauri mambo yafuatayo: -

*(i)* Jamii kuacha muhali wa kuwahifadhi watu wenye nia ovu ya kuhujkumu uchumi wetu na kuendeleza wimbi la rushwa kwa jamii iliyowazunguka.

*(ii)* Serikali ifanye utaratibu wa kuipatia mamlaka hii vifaa vya kisasa vya uchunguzi ambavyo vinawezesha kutambua mbinu za uhujumu uchumi zinazotumika nchini.

*(iii)* Wizara iandae mpango maalumu wa kuwaombea mamlaka hii wataalamu ambao watasaidia kufikia malengo yake, na

*(iv)* Mwisho, Kamati inaishauri wizara kusimamia na kuiwezesha Mamlaka hii kupata fedha za matumizi mengineyo ambayao ndio chanzo cha maendeleo yao.

## 5.12 TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Tume ya Maadili) ni Taasisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 4 ya Mwaka 2015 na imepewa mamlaka ya kusimamia maadili ya viongozi wa umma. Mamlaka hayo yanajumuisha kupokea, kusajili na kuhakiki Tamko la Rasilimali na Madeni kutoka kwa Viongozi wa Umma, kufanya uchunguzi na kushughulikia malalamiko, tuhuma au madai kuhusu uvunjwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kutoa elimu kwa umma na viongozi kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili.

**Mafanikio ya Tume ya Maadili**

*(i)* Kufanya uhakiki wa Taarifa za mali na madeni ya Viongozi wa Umma.
*(ii)* Kuendelea na mfumo wa Kielektroniki wa usajili wa taarifa za mali na Madeni ya viongozi wa Umma.
*(iii)* Kuandaa na kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili kwa mwaka 2023/2024.
*(iv)* Kupokea na kufanya uchunguzi wa tuhuma na malalamiko ya ukiukwaji wa sheria ya maadili ya viongozi wa umma.
*(v)* Kujenga uelewa kwa viongozi wa Umma na wananchi kuhusu maadili ya viongozi wa umma kwa Unguja na Pemba.

**Changamoto zinazoikabili Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kamati wakati wa ufatiliaji wa utekelezaji wa kazi za imegundua bado zipo changamoto ambazo zinahitaji mikakati maalumu ya kuweza kuzitatua. Miongoni mwao nikama zifuatazo:

*(i)* Uelewa mdogo kwa baadhi ya viongozi wa umma na wananchi juu ya majukumu na utendaji kazi wa Tume.
*(ii)* Katika jukumu la uhakiki wa taarifa za viongozi, tumegundua kuna baadhi ya viongozi hawana hati za umiliki wa mali zao ambazo wanazimiliki.
*(iii)* upungufu wa baadhi ya vitendea kazi na vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Tume ikiwemo jukumu la utoaji wa elimu kwa wananchi, uchunguzi, usajili na uhakiki wa taarifa za viongozi. Vitendea kazi na vifaa hivyo ni pamoja na gari, kompyuta na vifaa vya usikilizaji wa mashauri ya malalamiko.

**Maagizo ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

*(i)* Kamati inaitaka Tume kuendelea na hatua za utoaji wa elimu ya maadili kwa viongozi na wananchi.

*(ii)* Kamati pia, inaitaka Tume kuendelea kuwahimiza viongozi kufanya usajili mali zao kwa wakati bila ya kushurutishwa kwa mujibu wa sheria.

*(iii)* Vile vile, Kamati inaishauri Tume kuendelea na hatua za utafutaji wa vitendea kazi ambavyo ni muhimu katika kutekeleza majukumu yao.

## 5.13 OFISI KUU – PEMBA

Jukumu la msingi la Ofisi kuu ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba, katika kusimamia hilo, Ofisi imefanikiwa kuratibu vikao 2, kati hivyo kikao 1 kimezungumzia "Kanuni za Utumishi wa Umma kwa Watumishi Wanaohamishiwa Kikazi Nje ya Utumishi wa Umma" le ngo la kikao hicho ni kupokea maoni na kuichangia rasimu mpya kulingana na mahitaji ya wakati wa sasa. Kikao hicho kimehudhuriwa na Kamati ya Kanuni na Sheria ndogo ndogo za Baraza la Wawakilishi Zanzibar pamoja na watendaji wa Taasisi za SMZ Pemba. Kikao chengine kilihusu uhakiki wa taarifa za Mfumo wa Rasilimaliwatu na malipo, lengo la uhakiki huo ni kuangalia usahihi wa taarifa za watumishi kabla ya kuanza kutumika kwa mfumo huo ambao unategemewa kuanza kutumika hivi karibuni. Washiriki wa zoezi hilo ni maafisa utumishi wa Wizara na Taasisi zote za SMZ Pemba.

Ofisi imefanya kazi ya kutoa elimu na maelekezo ya kiutumishi kwa watumishi wapya imefanyika, miongoni mwa watumishi waliopatiwa elimu hiyo ni watumishi wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana pamoja na watumishi wa Ofisi ya Muft Mkuu Pemba. Uhakiki wa Rasilimali watu kwa kuzingatia Muundo wa Wizara ya Afya umefanyika. Lengo la uhakiki huo ni kujua mahitaji halisi ya watumishi na kuweza kushauri kupangwa watumishi wa Wizara hio kwa mujibu wa kada zao. Ofisi imefanikiwa kufanya kikao na

watumishi wa OR/KSUUB kwa upande wa Ofisi Kuu Pemba, lengo ni kukumbushana kusimamia na kutekeleza majukumu yetu ya kazi, miongoni mwa mada ambazo zimezungumzwa ni pamoja na nidhamu na uwajibikaji, kuzisoma na kuzifahamu Kanuni na Sheria za Utumishi ili kuweza kutoa huduma bora kwa jamii.

## 6. OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ina jukumu la kusimamia Sera, Sheria na Kanuni za Ofisi ili kuhakikisha kuwa inaweka mazingira mazuri ya kutoa huduma za kijamii na kiuchumi sambamba na kuimarisha ulinzi na usalama kwa wananchi na wageni wanaoingia na kutoka Zanzibar. Aidha, Ofisi hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli zinazotekelezwa na Taasisi zisizo za Kiserikali (NGO's) ambazo zinasaidia kupunguza umasikini na kukuza uchumi wa wananchi.

Dira ya Ofisi hii ni kuwa Taasisi imara katika kusimamia amani, usalama, usajili wa wakaazi na upatikanaji wa huduma karibu na wananchi.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inaundwa na Idara zifuatazo zilizo chini Katibu Mkuu:

*(a)* Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa.
*(b)* Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ.
*(c)* Tume ya Utumushi wa Idara Maalum za SMZ.
*(d)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
*(e)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
*(f)* Ofisi Kuu Pemba.

Aidha, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inasimamia Taasisi 11 zinazojitegemea zifuatazo: -

*(a)* Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU),
*(b)* Chuo cha Mafunzo (MF),
*(c)* Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM),
*(d)* Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU),
*(e)* Kikosi cha Valantia (KVZ),
*(f)* Ofisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi,
*(g)* Ofisi ya Mkoa wa Kusini Unguja,
*(h)* Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja,
*(i)* Ofisi ya Mkoa wa Kusini Pemba,
*(j)* Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Pemba,
*(k)* Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar.

Katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi hiki Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Kamati imefanikiwa kuzitembelea na kukagua utekelezaji wa kazi za taasisi mbali mbali zilizochini ya Ofisi hii.

Hivyo basi, kwa kutumia Kanuni ya za Baraza la Wawakilishi (Toleo la mwaka 2024), miongozo ya sera na matoleo mbali mbali ya Serikali pamoja na Ilani ya CCM ya 2020 – 2025, Kamati imeweza kutembelea na kukagua utekelezaji wa bajeti na miradi ya maendeleo kwa taasisi zifuatazo:

## 6.1 JESHI LA KUJENGA UCHUMI *(JKU)* ZANZIBAR

Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar *(JKU)* ni miongoni mwa Idara maalumu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizo chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ. JKU imeanzishwa kupitia Ibara ya *121(1)* ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984* na Sheria Nam. *6* ya mwaka *2003*. Kwa mujibu wa Sheria,

JKU imepewa jukumu la kutoa mafunzo kwa vijana katika nyanja za uzalishaji wa kilimo, mifugo na uvuvi. Sambamba na kuwafunza vijana ufundi, kazi za amali na uzalendo kwa ajili ya kuwafanya waweze kujitegemea, kuitumikia na kuijenga nchi.

Aidha, Kamati imeridhishwa na utendaji wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kwenye ngazi ya Utawala na Uendeshaji, wanavyolitumikia Jeshi hili sambamba na kuwajenga vijana katika misingi iliyobora na ya ukakamavu kwa maslahi ya taifa. Idara pia, imeweza kuimarisha makaazi bora kwa askari wake na vijana waliopo makambini pamoja na kuimarisha maslahi yao kwa ujumla.

**Changamoto za Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) Zanzibar**

Katika utekelezaji wa kazi za JKU Zanzibar na kutimiza malengo yaliyoainishwa katika bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025, Kamati imebaini kuwa zipo baadhi ya changamoto zinazokifanya kikosi hiki kufikia malengo yake kwa hatua isiyo ya kuridhisha. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo: -

*(i)* Ukosefu wa miundombinu ya uzalishaji katika mashamba na viwanda vya JKU, hali ambayo inayotokana na JKU kutumia mashine zilizopitwa na wakati katika uzalishaji wake wa mazao na samani.

*(ii)* Kuwepo kwa uhaba wa wataalamu wa fani mbalimbali ikiwemo, kilimo mifugo, uvuvi, afya, uhandisi na usanifu wa majengo.

*(iii)* Kamati inasikitishwa na uwepo wa tatizo la uhaba wa vyombo vya usafiri pamoja na vitendea kazi.

*(iv)* Muamko mdogo wa vijana wanaojiandikisha kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria hali inayoashiria taifa kuja kukosa nguvu kazi iliyolelewa kimaadili na kiuzalendo.

**Maagizo ya Kamati kwa JKU Zanzibar**

*(i)* Kamati inaipongeza Idara ya JKU kwa namna walivyoweza kuleta matokeo mazuri ya vijana wetu waliomaliza kidato cha nne sambamba na kuendeleza elimu ya kidatu cha tano na sita katika skuli yao ya Mtoni. Kamati inaishauri JKU kulipa kipaumbele wa kuanzisha Skuli hiyohiyo kwa upande wa Pemba na Kaskazini Unguja ili vijana waendelee kupata ukakamavu na elimu iliyo bora.

*(ii)* Kamati inashauri JKU kuendelea na juhudi za kuimarisha miundombinu katika vikosi na kambi za kila zoni ili kuongeza uwezo wa kusajili na kuhudumia vijana ipasavyo.

*(iii)* Kamati pia, inashauri JKU kuimarisha miundombinu ya uzalishaji mali kwa kujenga "green house", kuchimba visima vya umwagiliaji katika makambi na kuzipatia kambi pembejeo na zana za uzalishaji ikiwemo matrekta na mbegu bora za mazao mbalimbali ambazo watazifanyia utafiti ili ziweze kuleta matokeo mazuri.

*(iv)* Kamati inaitaka Idara kuendelea kununua na kufanya matengenezo ya vyombo vya usafiri kwa kuvipatia vipuri na matengenezo ya kawaida. Ipo haja ya Serikali kuviangalia vikosi vyetu kwa upande wa usafiri ili waweze kurahisisha shughuli zao za kila siku.

*(v)* Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kupitia ngazi za masheha kuwashajihisha vijana kuwa na muamko wa kujiunga na JKU ili kupata taifa lililo bora na kupunguza vijana wasio na kazi za kufanya mitaani.

*(vi)* Kamati inashauri JKU kujenga majengo mapya na ya kisasa katika makao makuu ya Saateni.

## 6.2 WAKALA WA ULINZI WA JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Wakala wa Ulinzi JKU umeanzisha rasmi chini ya Sheria nam. 2 ya mwaka 2015 ukiwa na lengo la kusimamia na kuimarisha huduma za ulinzi katika maeneo ya uwekezaji na utalii ili kukuza uchumi wanchi pamoja na kuhakikisha na kurahisisha upatikanaji wa huduma za ulinzi wa uhakika na ulio bora.

Kamati imeridhishwa na kazi wanazofanya Wakala wa Ulinzi wa JKU yenye Makao Makuu yake Saateni kwa wanavyoendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa majengo ya viongozi wetu pamoja na taasisi binafsi ambazo huhitaji huduma bora za Wakala. Kufanya doria na kutoa mafunzo yenye ushauri wa kiulinzi na kiusalama kwa wamiliki wa taasisi za utalii. Kutoa miongozo mbalimbali ya kiulinzi kwa niaba ya Serikali pamoja na kutoa maelekezo kuhusiana na vijana na mitambo ya kiusalama. Kamati inawataka kutochoka kutimiza wajibu wao ili hali ya usalama nchini izidi kuimarika.

**Changamoto za Wakala wa Ulinzi wa JKU Zanzibar**

Katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku Wakala inakabiliwa na changamoto ndogo ndogo ambazo Kamati imezibaini na zinafaa kutatuliwa. Changamoto zenyewe ni kama zifuatavyo:

*(i)* Uwepo wa Madeni yatokanayo na makusanyo ya huduma ya ulinzi kwa Taasisi hii ambapo wengi wa wapewa huduma wamekuwa wagumu katika kufanya malipo ya huduma ya ulinzi kwa wakati kwa kisingizio cha kukosa ruzuku au kupata ruzuku kidogo ukilinganisha na mahitaji ya taasisi zao, hili linapelekea kukwamisha jitihada za kiutendaji za wakala katika kufikia malengo waliojiwekea yaliyosababishwa na madeni ya taasisi za Serikali kwani hadi kamati inapokea taarifa hii Wakala imekuwa ikidai TZS 2, 072,218,000 kwa taasisi mbali mbali.

*(ii)* Kushindwa kuwasilisha fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kutotimiza kiwango walichopangiwa ambacho ni kikubwa kuliko uwezo wa mapato yao.

*(iii)* Ufinyu wa Ofisi kutokana na eneo wanalotumia hivi sasa ni dogo kulingana na mahitaji ya kazi za Wakala wa Ulinzi.

*(iv)* Uchakavu wa vitendea kazi hasa gari na Sare ambazo ndio nyenzo muhimu za Wakala katika uendeshaji wa shughuli zao za ulinzi.

*(v)* Upungufu wa nguvu kazi ya waajiriwa;

*(vi)* Ulipaji mdogo unaotokana na bei elekezi ya vituo vya Serikali.

**Maagizo ya Kamati kwa Wakala wa Ulinzi**

*(i)* Kamati inasikitishwa na uwepo wa madeni makubwa kama ni malipo ya Wakala hivyo inashauri Serikali kutafuta njia mbadala za kuyapunguza madeni hayo kupitia Wizara ya fedha katika fedha za Ruzuku ambazo hupelekwa katika wizara. hivyo, Kamati inazitaka taasisi zote zinazodaiwa kutoa kipaumbele kwa kulipa madeni yake kwa wakati ili kurahisisha utoaji wa huduma katika maeneo yao.

*(ii)* Kamati inashauri Serikali kufanya marekebisho ya bei elekezi iliyowekwa kwa taasisi za umma zinazolindwa na wakala zitazokwenda sambamba na ulipaji wa kima cha chini cha mishahara.

*(iii)* Kamati inaishauri Serikali kuwapatia ajira ya kudumu vijana waliojitolea kwenye kazi za ulinzi ndani ya JKU ili kuweza kulinda vituo vingi vyenye tija na kuepuka kulipa jumla ya TZS 254,760,000 kwa mwezi ambapo jumla ya TZS 3,057,120,000/ kwa mwaka ikiwa ni posho la wasaidizi.

*(iv)* Kamati inaishauri Serikali kuwapatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la Wakala ambayo itaendana na mahitaji ya kazi zao.

## 6.3 CHUO CHA MAFUNZO (MF) ZANZIBAR

Idara ya Chuo cha Mafunzo ni miongoni mwa Idara tano maalum za Serekali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984 na inaongozwa na Sheria Nambari 1 ya mwaka 1980 pamoja na Sheria Nambari 3 ya marekebisho ya mwaka 2007. Idara inatekeleza majukumu yake chini ya (OR) Tawala za Mikoa Serekali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Idara ya Chuo cha Mafunzo inatekeleza programu kuu mbili ambazo ni Programu kuu ya Urekebishaji Tabia kwa Wanafunzi na Programu kuu ya Utawala na Uendeshaji. Kupitia programu hizo, Chuo cha Mafunzo kimeweza kufanikisha malengo yake kwa kutekeleza shuhghuli ambazo zimepangwa kwa mwaka huu ikiwemo kuwapatia wanafunzi utaalamu katika fani za ushoni, kilimo, ujenzi, fundi uwashi, fundi seremala, fundi gereji, ufugaji na utunzaji wa bustani.

Kwa upande wa shughuli za maendeleo, Idara imefanikiwa kununua vifaa vya TEHAMA na kukamilisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu Unguja. Aidha, idara imeendelea na ujenzi wa hanga la askari Bumbwini na kuanza ujenzi wa nyumba 9 za familia 18 katika kambi ya Hanyegwa Mchana.

Kamati baada ya kupata fursa ya kutembelea kambi mbali mbali za Vyuo vya Mafunzo Unguja na Pemba na kuweza kujionea namna bora wanavyoweza kuyakabili majukumu yao ya kuwapokea, kuwalinda pamoja na kuwarekebisha wale wote walioikosea jamii na kupelekwa Chuo cha Mafunzo kwa mujibu wa Sheria ili wanaporudi katika jamii wawe raia wema inakri kuridhishwa na utendaji kazi wa Idara hii.

**Changamoto za Chuo cha Mafunzo Zanzibar**

Pamoja na mafanikio mazuri yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, Chuo cha Mafunzo Zanzibar kimekabiliwa na Changamoto zifuatazo:

*(i)* Idara inakabiliwa na upungufu wa miundo mbinu ya umwagiliaji maji katika kambi zake mbalimbali na kusababisha mazao kutoimarika vyema katika maeneo hayo.
*(ii)* Tatizo la Mabadiliko ya hali ya tabia ya nchi huathiri sana sekta ya kilimo na mifugo.

*(iii)* Upungufu wa wataalamu wa kilimo wataopelekea kuendeleza uzalishaji mzuri na wenye tija kwa Shuo.

*(iv)* Gharama kubwa inayotumika katika kilimo cha miwa kutokana na njia wanazozitumia katika uzalishaji.

*(v)* Uhaba wa gari kwa ajili ya kutolea huduma kambi mbali mbali za Chuo unaathiri ufanisi wa kazi.

*(vi)* Uhaba wa fedha za kuendeleza mradi wa ufugaji wa kuu umepelekea Kutokukamilika kwa mradi wa ufugaji wa kuku katika kambi ya Hanyegwa Mchana ambao ulikuwa chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

**Maagizo ya Kamati kwa Chuo cha Mafunzo**

Katika kukabiliana na changamoto hizo Kamati inashauri yafuatayo:

*(i)* Kamati inashauri Chuo cha Mafunzo kufanya mradi wa kilimo cha miwa kwa gharama zake wenyewe kuanzia hatua za mwanzo hadi mavuno na kuuza kama bidhaa yake bila kushirikisha wawekezaji.

*(ii)* Kamati inashauri Chuo kukamilisha kwa haraka mradi wa ufugaji kuku katika kambi ya Hanyegwa mchana baada ya kukamilika ujenzi wa mabanda. Aidha, kamati inashauri wizara kusimamia uendelezaji wa mradi huu kwa kuwaombea fedha za mradi Serikalini.

*(iii)* Kamati inaishauri Serikali kupitia taasisi za haki jinai kukaa pamoja na kufikiria namna bora ya kutekeleza hukumu ya adhabu ya kuitumikia jamii badala ya kesi ndogo ndogo kuhukumiwa kifungo gerezani na kuisababishia Serikali gharama kubwa katika kutoa huduma kwa wanafunzi.

## 6.4 KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimeanzishwa chini ya Sheria nambari 1 ya mwaka 2003 ambapo kina majukumu ya kulinda

usalama wa bahari ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, kuzuia njia zote zinazoweza kutumika kupitishia magendo, kusaidia vyombo vya abiria na kufanya uokozi baharini pamoja na kushirikiana na Jeshi la Wananchi pale itakapotakiwa kufanya hivyo katika kuilinda Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mafanikio ya Kikosi cha KMKM Zanzibar**

*(i)* Kupitia programu kuu ya ulinzi na uokozi baharini kikosi kimefanikiwa kufanya doria mbali mbali ambazo zimepelekea kuokoa na kukamata mali kadhaa ambazo zilikusudiwa kusafirishwa kwa njia ya magendo. kwa mwaka 2024 kikosi kiliokoa zaidi ya shilingi milioni 215,424,000/- kama thamani ya mali zilizokuwa zikisafirishwa nje ya nchi.

*(ii)* Katika programu ya utawala na uendeshaji wa KMKM, kikosi kimeweka mazingira safi ya kazi na ustawi wa askari wake kwa kuboresha huduma za chakula, vifaa vya ofisi na kulipa stahiki za wapiganaji kwa wakati.

*(iii)* kupitia programu hii, Kikosi kimefanikiwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu jumla ya wapiganaji 74 katika vyuo vya ndani na nje ya nchi kwa lengo kuboresha uwezo wao wa kiutendaji katika fani za ubaharia, ufundi, afya na utawala.

*(iv)* Kikosi kimefanikiwa kusimamia na kutoa huduma za afya kwa askari na raia wanaoishi karibu na kambi kwa kuwapatia huduma za matibabu na ushauri katika masuala ya kiafya ambapo Hospitali ya Kibweni pekee imehudumia zaidi ya wapiganaji na wananchi 16,400 ndani ya kipindi cha muda mfupi.

*(v)* Kwa upande wa miradi ya maendeleo, Kikosi kimefanikiwa kutekeleza miradi mikuu miwili ambayo ni mradi wa ujenzi na ukarabati wa kambi na nyumba za KMKM, na mradi wa Uzamiaji na uokozi. Utekelezaji wa miradi hii kwa sasa ipo katika hatua za utekelezaji.

**Changamoto za Kikosi cha KMKM Zanzibar**

Licha ya mafanikio mbali mbali ambayo Kamati imeyaona pamoja na mikakati ambayo inatumika katika utekelezaji wa majukumu yao, KMKM hata hivyo imekabiliwa na changamoto zifutazo:

*(i)* Uhaba wa fedha za kuanzisha miradi ya kimaendeleo na uendelezaji wa miradi ambayo imeanzishwa kama vile mradi wa ujenzi na ukarabati wa nyumba na ununuzi wa samani na vifaa tiba.

*(ii)* Uhaba wa vyombo vya usafiri kwa kambi za zote Unguja na Pemba unarudisha nyuma ufanisi wa kazi za kikosi.

*(iii)* Uhaba wa fedha za matumizi mengineyo (OC) tatizo ambalo linapelekea baadhi ya mipango ya kikosi kushindwa kutekelezeka.

**Maagizo ya Kamati kwa KMKM**

*(i)* Kamati inakiagiza kikosi kuzidisha bidii katika operesheni za baharini na nchi kavu ili kukabiliana na wafanyabiashara haramu za magendo.

*(ii)* Kamati inakishauri kikosi kuendeleza miradi yake ambayo imesimama kutokana na matatizo mbali mbali ikiwemo ukosefu wa fedha na wataalamu.

*(iii)* Kamati inakitaka kikosi kusimamia na kuanzisha ujenzi mpya wa kituo cha afya katika kambi ya Tundauwa kwa kuwa kituo kilichopo sasa hakifai na hakiendani na wakati.

*(iv)* Kamati pia, inakishauri Kikosi kujenga kituo cha mafuta cha kibiashara ili kujiongezea vyanzo vya mapato.

*(v)* Kamati inaishauri Serikali kuandaa mkakati maalum wa kuwapatia fedha za matumizi na ruzuku kwa ajili ya kuendesha miradi yake iliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

## 6.5 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU)

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi *(KZU)* kimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria nambari 7 ya mwaka *1999* na kina jukumu la kusimamia shughuli zote za uzimaji moto na uokozi wa maisha na mali za watu, kusimamia na kuhakikisha kuwa huduma za zimamoto kwenye Viwanja vya Ndege na Bandarini zinakwenda sambamba kulingana na masharti ya Kitaifa na Kimataifa.

**Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa shughuli za Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, Zanzibar**

*(i)* Kikosi kimeendelea kutoa elimu ya tahadhari ya majanga ya moto inayotolewa kwa Wananchi, Taasisi za Serikali na za watu binafsi, ambapo elimu ya utumiaji wa mitungi ya kuzimia moto katika taasisi 21 za serikali na binafsi zimefikiwa.

*(ii)* Kikosi kimewawezesha wapiganaji 150 kupata mafunzo ya uongozi wa kati (Senior NCO's Course), wapiganaji 300 wamemaliza mafunzo ya refresher na wengine 62 wanaendelea na mafunzo katika kada mbali mbali.

*(iii)* Kikosi kimeendeleza ushirikiano kwa Taasisi za Serikali na za watu binafsi kwa kufanya ukaguzi wa vifaa vya kujikinga na moto na kuwaelekeza namna ya matumizi bora ya vifaa hivyo.

*(iv)* Kikosi kimekamilisha ujenzi wa vituo viwili na kuanza kufanya kazi. Vituo hivyo ni Tasini Mkanyageni kwa upande wa Pemba na Kiwengwa kwa upande wa Unguja.

*(v)* Kikosi kimeimarisha usalama wa viwanja vya ndege kwa kuhudumia ndege kubwa na ndege ndogo katika kiwanja cha Abeid Amani Karume International Airport (AAKIA), Karume Airport (KA) na Nungwi Airport kwa wakati wa kuruka, kutua na kutia mafuta. Pia, huduma kama hizo za utiaji wa mafuta na ushushaji wa abiria na mizigo zimetolewa katika bandari za Zanzibar.

*(vi)* Kikosi kimeendelea kufanya doria katika ukanda wa bahari kwa lengo la kuimarisha usalama wa wananchi wanaotumia Bahari kama sehemu yao ya kujipatia kipato.

**Changamoto za Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar**

Licha ya mafanikio mazuri ya kikosi hiki bado kuna changamoto kadhaa zinazowakabili ambazo zimekuwa ni endelevu kutokana na hali inavyokwenda siku hadi siku, miongoni mwa changamoto hizo ni hizi zifuatazo:

*(i)* Uchakavu wa gari za kutolea huduma pamoja na ujazo mdogo wa maji wa gari hizo kulinganisha na ukubwa wa matukio ya moto hasa ya mahoteli na majengo ya umma.

*(ii)* Uhaba wa gari za kutolea huduma za uokozi na uzimaji moto katika makaazi ya watu.

*(iii)* Uhaba wa vyanzo vya maji na miundombinu ya maji isiyo rafiki kwa kazi za uokozi.

*(iv)* Tatizo la ujenzi holela usiofuata mipango miji katika nchi yetu inapelekea zoezi la uokozi kuwa kugumu kutokana na kushindwa kuyafikia kwa baadhi ya maeneo ya raia.

**Maagizo ya Kamati**

*(i)* Kamati inaishauri Serikali kukamilisha hatua za mkataba wa usambazaji wa vifaa vya uokozi na uzimaji moto kwa njia ya mkopo nafuu kutoka Serikali ya Austria.

*(ii)* Kamati inaiomba Serikali kukamilisha taratibu za ununuzi wa gari za uzimiaji moto na uokozi kwa kuwa taratibu za kumpata Mzabuni zimeshakamilika.

*(iii)* Kamati inakiagiza kikosi kuandaa na kusimamia mpango maalumu wa kuainisha sehemu ambazo zinahitaji kuwekwa “fire hydrants” pamoja

na kutoa taaluma kwa wakandarasi wote wanaojenga au kusimamia majengo ya umma na binafsi.

*(iv)* Kamati pia inakiashauri Kikosi kwa kushirikiana na Kamisheni ya Maafa kufanya tafiti za kina juu ya majanga ya moto yanayotokea kila siku katika jamii.

## 6.6 KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ)

Kikosi cha Valantia Zanzibar *(KVZ)* kimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria nambari *5* ya mwaka *2004*. Majukumu ya msingi ya KVZ ni kusimamia amani na utulivu nchini, kupambana na janga lolote litakaloikumba jamii, kulinda viongozi na mali za Serikali pamoja na kufanya kazi za kijeshi kwa madhumuni ya kuzuia hali inayohatarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu pamoja na kufanya kazi kibiashara kwa lengo la kujiongezea kipato.

Kikosi cha Valantia Zanzibar kinatekeleza majukumu yake kupitia programu kuu mbili ambazo ni Programu kuu ya Ulinzi wa Nchi, Raia na Mali zao, na Programu kuu ya Utawala na Uendeshaji. Aidha, kikosi kinatekeleza programu moja ndogo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kufanya shughuli zake za maendeleo.

Kwa kipindi cha mwaka 2024/2025 kikosi kimefanikiwa kwa asilimia kubwa kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi kwa kufanya doria mbali mbali mijini na ng'ambo ya mji kwa lengo la kuhakikisha usalama umeimarika.

Kwa upande wa miradi ya maendeleo kikosi kimefanikiwa kukamimlisha ujenzi wa kituo cha mafuta katika eneo la Makao makuu Mtoni. Pia, kinaendelea na ujenzi wa hospitali katika makao makuu Mtoni, ujenzi wa kituo cha afya Muyuni na Ndugukitu Pemba, ujenzi

wa mabanda ya kufugia kuku Muyuni, ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Kambi, ujenzi wa hanga jipya la kulala askari na ukarabati wa hanga kongwe katika kambi ya Ndugukitu Pemba.

**Changamoto za Kikosi Cha Valantia Zanzibar**

Kikosi cha Valantia Zanzibar kinakabiliwa na changamoto ndogo ndogo ambazo katika utekelezaji wa majukumu yake imekuwa zikirudisha nyuma mipango yao. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:

*(i)* Kamati imebaini upatikanaji mdogo wa fedha katika kutekelezaji wa miradi ya maendeleo na uhaba wa fedha za matumizi mengineyo.
*(ii)* Ukosefu wa vituo vya afya na huduma za uhakika kwenye makambi ukiachia Makao Makuu ambayo huduma za afya ndipo pekee hupatikana kwa uhakika na zenye ubora.
*(iii)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri kuanzia makao makuu na kambi nyengine mbali mbali za KVZ Unguja na Pemba.
*(iv)* Ubovu wa miundombinu ya barabara za kuingilia makambini.
*(v)* Kutokamilika kwa mradi kufugia kuku katika kambi ya Muyuni.

**Maagizo ya Kamati Kwa KVZ**

*(i)* Kamati inashauri kikosi kuzidisha kasi ya kufanya doria za ulinzi hususan katika maeneo yenye makundi ya kihalifu ambayo yanahatarisha usalama wa jamii.
*(ii)* Kamati inaishauri Wizara kusimamia na kufuatilia upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo ya kikosi ili kukamilisha miradi hiyo kwa mujibu wa bajeti yake ya maendeleo.
*(iii)* Kamati inashauri Kikosi kuzidisha juhudi za ujenzi wa vituo vya afya kwa zile kambi ambazo fedha zake zimeshapatikana.

*(iv)* Kamati inakishauri kikosi kuzidisha weledi wa kazi zake sambamba na kuitumia sheria yake katika kuibua na kutekeleza miradi mingi ya maendeleo.

*(v)* Kamati inaiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwamboea hati ya umiliki wa eneo la kambi ya Kisakasaka eneo ambalo linamikiwa na Jeshi la Wananchi Tanzania.

## 6.7 OFISI YA MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Mkoa wa Mjini Magharibi ni miongoni mwa Mikoa mitano ya Zanzibar ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Ibara ya 2(a) na Sheria Nambari 08/2018 Sheria ya Tawala za Mikoa. Kiutawala Mkoa wa Mjini Magharibi ni mkusanyiko wa Wilaya tatu; (Mjini, Magharibi 'A' na Magharibi 'B') na Shehia 121 ukiwa na jukumu la kusimamia na kutekeleza Sera, Sheria, Mipango na Miongozo ya Serikali.

Kwa mujibu wa takwimu za awali za sensa ya watu na makaazi ya mwaka 2022 Mkoa wa Mjini Magharibi una idadi ya watu wapatao laki nane, tisiini na tatu elfu mia moja na sitini na tisa (893,169) ambapo ni sawa na asilimia 47.3 ya wakaazi wote wa Zanzibar.

Hivyo, tumeona kuwa Mkoa huu ndio wenye idadi kubwa zaidi ya watu na matumizi ya rasilimali na miundombinu ni makubwa zaidi ukilinganisha na mikoa mengine ya Zanzibar.

**Kwa msingi huo, Kamati imeridhika na utekelezaji wa majukumu yake kutokana na mafanikio yafuatayo:**

*(i)* Kuimarika kwa Ulinzi na Usalama wa wananchi na wageni wanaoishi ndani ya Mkoa huu.

*(ii)* kufuatilia na kusimamia miradi ya maendeleo ambayo ndio msingi wa utekelezaji wa Ilani ya CCM na hivyo, kupitia maadhimisho ya miaka 61 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar Mkoa ulitoa jumla ya miradi 57 ya maendeleo ambayo miongoni mwake ipo iliyofunguliwa na mengine kuwekewa mawe ya msingi.

*(iii)* kufuatilia na kusimamia matukio ya udhalilishaji ambayo yamekuwa yakiripotiwa katika Ofisi ya Mkoa siku hadi siku.

*(iv)* Mkoa pia, umeshughulikia malalamiko ya migogoro ya ardhi ambapo kwa kipindi cha miezi 6 jumla ya malalamiko 27 yalisikilizwa na kupatiwa usuluhishi.

*(v)* Kuratibu ustawi wa wazee na watu wenye ulemavu ambapo wastani wa wazee 497 walifikiwa na kupatiwa msaada. Kwa upande wa watu wenye ulemavu jumla ya watu 9 walipatiwa vifaa kama vile viti vya marugudumu mawili, magongo na fimbo nyeupe.

## 6.8 BARAZA LA JIJI LA ZANZIBAR

Baraza la Jiji la Zanzibar lilianzishwa mwaka 2019 chini ya kifungu cha 18 cha Sheria Nambari 7 ya Mwaka 2014. Majukumu ya msingi ya Baraza la Jiji yameainishwa katika kifungu cha 19(a) mpaka (h) cha Sheria hiyo.

Baraza la Jiji limefanikiwa kuendesha programu za kujenga uwezo kwa waheshimiwa Madiwani na watendaji katika fani tofauti ikiwemo mafunzo ya uongozi, mafunzo ya udereva na teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT).

Baraza limezamiria kuanzisha miradi ya kiuchumi na kimaendeleo kwa kuendeleza mradi wa "Youth Climate Change" kwa kuwashirikisha vijana wabunifu kupitia mradi mkubwa wa "Youth Climate Action Fund" chini ya udhamini wa "Bloomberg Centre for Public Innovation".

Matarajio ya mradi huu ni kusaidia usafi wa jiji la Zanzibar na upandaji wa miti kwa lengo la kuimarisha mazingira ya mji na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**Changamoto zinazolikabili Baraza la Jiji la Zanzibar**

Ofisi ya Baraza la Jiji inaendelea kukabiliwa na baadhi ya changamoto katika utekelezaji wa kazi zake za kila siku, miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:

*(i)* Muingiliano wa majukumu kati ya Jiji na Manispaa za Mkoa wa Mjini Magharibi.
*(ii)* Ukosefu wa jengo la kudumu la Baraza kwa ajili ya Ofisi.
*(iii)* Uchakavu wa uhaba wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya kazi za ufuatiliaji za baraza la Jiji.
*(iv)* Kuchelewa kuingiziwa fedha za bajeti (OC).
*(v)* Kuchelewa kuidhinishiwa muundo wa Baraza la Jiji
*(vi)* Uhaba wa watumishi wenye ujuzi wa fani mbali mbali.

**Maagizo ya Kamati**

Kwa kuwa Kamati imebaini changamoto mbalimbali ambazo kimsingi zinarudisha nyuma maendeleo ya Jiji la Zanzibar tumeona ipo haja ya kupendekeza hatua ambazo zitaweza kusaidia kutatua changamoto hizo, miongoni mwa hatua hizo ni kama ifuatavyo:

*(i)* Kamati inashauri Baraza kupitia maandiko ya miradi kubuni na kuibua vyanzo vya mapato ambavyo vitawawezesha kupata udhamini na wawekezaji ikiwemo kukodisha sehemu za jengo kwa ajili ya matumizi ya ofisi, biashara, maegesho na usimamizi wa usafi wa jiji.
*(ii)* Kamati pia inaishauri Serikali kuwapatia vyombo vya usafiri Baraza la Jiji kwa ajili ya shughuli za Ofisi.

(iii) Kamati inalishauri Baraza liandae mpango maalumu utakaowawezesha kupata ofisi yake ya kudumu pamoja na kuwa na wataalamu ambao watasaidia kukuza maendeleo ya Jiji.
(iv) Kamati inashauri wizara kufuatilia Tume ya Utumishi Serikalini Muundo uliopendekezwa na Baraza la Jiji pamoja na mpango wa rasilimati watu wa Baraza ambao tayari umeshawasilishwa Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ili kufahamu hatua iliyofikiwa kwa utekelezaji.

## 6.9 BARAZA LA MANISPAA MJINI

Baraza la Manispaa Mjini limeanzishwa kwa Mujibu wa Sheria nambari 7 ya Mwaka 2014, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na linajukumu la kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo kutoa huduma za usafi wa mji na mazingira, kusimamia maeneo ya wazi pamoja kusimamia kutekeleza mpango mkuu wa mji, kusaidia wajasiriamali wadogo, kuweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara pamoja na kusimamia masuala mtambuka.

**Katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 Baraza la Manispaa ya Mjini limefanikiwa kuitekeleza mambo yafuatayo: -**

(i) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ambapo kwa kipindi cha robo ya pili ya oktoba – Disemba hali ya mapato haikuwa nzuri sana kutokana na kukusanya wastani wa asilimia 63% ya makusanyo yake.
(ii) Kuimarisha huduma za jamii na masuala mtambuka kwa kuimarisha huduma za usafi wa mazingira, kusimamia maeneo ya wazi ili kuufanya mji upendeze.
(iii) Kuweka mazingira bora ya wafanyabiashara wadogo na kuwawezesha wajasiriamali kiuchumi ambapo jumla ya vikundi 11 vilipatiwa mikopo.

*(iv)*Kusimamia shughuli za uendeshaji wa ofisi na rasilimali watu.

**Changamoto za Baraza la Manispaa Mjini**

Mbali na utekelezaji huo wa Baraza nilioutaja hapo juu, Baraza linakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Utayari bado ni mdogo kwa jamii katika kushirikiana na Manispaa juu ya masuala ya usafi.
*(ii)* Uwelewa mdogo wa wajasiriamali kujisajili na kupatiwa Vitambulisho.
*(iii)* Mwamko mdogo kwa jamii juu ya ulipaji wa ada na tozo mbali mbali za Manispaa jambo linalopelekea kushuka kwa mapato.

**Maagizo ya Kamati**

Kutokana na changamoto hizi ambazo Kamati imeziibua na kimsingi zinarudisha nyuma maendeleo ya Manispaa ya Mjini, Kamati inashauri na kupendekeza mambo yafuatayo:

*(i)* Kamati inaitaka Manispaa ya Mjini kuongeza programu za uhamasishaji jamii juu ya masuala ya usafi kupitia televisheni, redio, mikutano ya jamii pamoja na mikutano katika skuli.
*(ii)* Kamati inaisisitiza Manispaa kutia nguvu katika matumizi ya kanuni ya papo kwa papo ili kuweka nidhamu katika mji na kuongeza vyanzo vipya vya mapato.
*(iii)*Kamati inaliomba Baraza kuongeza juhudi za kufanya usafi kwa kushirikiana na jamii, wafanyabiashara, taasisi mbali mbali na vikundi vya usafi.
*(iv)*Kamati pia inasisitiza Baraza kuongeza juhudi katika kusimamia vyanzo vya mapato vilivyopo kwa kufanya operesheni mbali mbali kwa ajili ya wafanyabiashara na wananchi wanaokwepa kulipa ada na tozo kwa hiari pamoja na kuwasimamia wafanyakazi wanaohusika na ukusanyaji wa mapato.

*(v)* Kamati pia inashauri kuongeza juhudi za kutoa elimu na operesheni wa usajili na upatikanaji wa vitambulisho vya wajasiriamali wadogo.

*(vi)* Kamati inaligiaza Baraza kukamilisha mradi wa ujenzi wa soko la Kwahajitumbo na soko la Mombasa.

## 6.10 BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI "A"

Baraza la Manispaa Magharibi 'A' limeanzishwa kwa Mujibu wa Sheria nambari 7 ya Mwaka 2014, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na linajukumu la kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo kutoa huduma za usafi wa mji na mazingira, kukusanya mapato, kusimamia na kutekeleza mpango mkuu wa mji. Aidha, Kamati katika ziara zake mbali mbali imekuwa ikitembelea na kukagua miradi na kazi tofauti ambazo zimekuwa zikitekelezwa na Manispaa hii na kujionea mafanikio ya utekelezaji wake ukiwa wenye kuridhisha kwa kiasi chake. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:

*(i)* Baraza limefanikiwa kukamilisha soko la kwa kisasi ambalo linaendelea kutumika;

*(ii)* Kuimarisha usafi wa Mazingira;

*(iii)* Kusimamia na kuboresha mazingira ya wafanyabiashara wadogo wadogo;

*(iv)* Kusimamia na kufuatilia ujenzi wa soko la Chuini ili kuongeza vyanzo vipya vya mapato.

*(v)* Kusimamia ujenzi na kukamilisha ujenzi wa soko la Shuwari lililopo kwa kisasi na kuendelea na mradi ya ujenzi wa Kituo cha Daladala cha Mndo.

**Changamoto zinazolikabili Baraza la Mji Magaharibi 'A'**

Licha ya mafanikio ambayo Baraza limeyafikia kwa mwaka huu, lakini bado zipo changamoto ambazo zinahitaji mikakati maalumu ya kuweza kuzitatua. Miongoni mwao nikama zifuatazo:

*(i)* Mwamko mdogo wa jamii katika kushirikiana na Manispaa juu ya masuala ya usafi.
*(ii)* Utayari mdogo wa baadhi ya wafanyabiashara kulipa ada kwa hiari ikiwemo ada ya tozo.
*(iii)*Uhaba wa taarifa za uhakika kwa walipakodi waliosajiliwa;
*(iv)*Uhaba wa vitendea kazi vikiwemo gari ya taka na vifaa vya ofisini;
*(v)* Elimu ndogo kwa wananchi juu ya umuhimu wa uhifadhi wa mazingira ya mji na maeneo ya kibiashara.

**Maagizo ya Kamati**

*(i)* Baraza lizidishe kasi ya programu za usafi wa mazingira na kuielimisha jamii juu ya umuhimu wa kutunza mazingira na kuweka safi haiba ya mji.

*(ii)* Baraza lifanye operesheni za ukaguzi wa mara kwa mara ili kubaini wafanyabiashara na wananchi wanaokwepa kulipa kodi kwa hiari na waweze kuwachukulia hatua za kisheria.

*(iii)* Kamati pia inaliagiza Baraza kubuni vyanzo vipya vya mapato ili liweze kujiendesha katika shughuli zao za kila siku.

## 6.11 BARAZA LA MANISPAA YA MAGHARIBI "B"

Baraza la Manispaa Magharibi 'B' limeanzishwa kwa Mujibu wa Sheria nambari 7 ya Mwaka 2014, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na linajukumu la kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo kutoa huduma

za usafi wa mji na mazingira, kukusanya mapato, kusimamia na kutekeleza mpango mkuu wa mji.

**Mafanikio ya Baraza la Manispaa Magharibi "B"**

*(i)* Kusimamia ujenzi wa vituo vikubwa vya mabasi ambavyo taasisi itashirikiana na mfuko wa hifadhi ya jamii katika ujenzi huo.

*(ii)* Kuratibu na kusimamia utoaji wa mikopo kwa makundi maalum (wajasiriamali).

*(iii)* Kuimarisha shughuli za utendaji wa Ofisi ikiwemo kusimamia Maslahi na stahiki kwa watendaji na Waheshimiwa Madiwani.

*(iv)* Kukuza ustawi wa jamii na kupunguza umasikini kwa kuwafikishia miradi na shughuli za maendeleo wananchi.

**Changamoto za Baraza La Manispaa Magharibi 'B'**

Baraza la Manispaa Linakabiliwa na changamoto zifuatavyo:

*(i)* Kamati imebani katika Manispaa hii kuwa suala la uimarishaji wa usafi wa mji bado ni tatizo pamoja na kufanya Operesheni za kuondoa majaa yasiyo rasmi katika maeneo mbali mbali ya Manispaa magharibi 'B'.

*(ii)* Kamati pia, imebaini kuwepo kwa ujenzi holela katika Manispaa hii ambapo wananchi huruhusiwa kujenga bila kufuata mpango wa mji na hivyo kupelekea njia zilizowekwa kwa matumizi ya wananchi kuzibwa bila mpangilio.

*(iii)* Manispaa hii, pia inasuasua katika uanzishaji wa miradi mipya ya maendeleo ikiwemo Ujenzi wa Jengo la kibiashara (Mombasa kwa Mchina), Mradi wa Maegesho Mwanakwerekwe (Bwawa), Ujenzi wa Jengo la kibiashara na eneo la bustani Kiembe Samaki na uwekaji wa mabango mapya ya matangazo ya kielektroniki maeneo ya barabarani.

**Maagizo ya Kamati**

(i) Baraza lisimamie ipasavyo zoezi la usafi wa mji katika Manipaa hii pamoja na kuwachukulia hatua kali wale wote wanaokiuka miongozo, masharti ya afya na usafi wa mazinigra ya ndani na nje ya wafanyabiashara.

(ii) Baraza liachane na suala la muhali kwa wale wote wanaojenga bila kufata taratibu za mipango miji.

(iii) Baraza lijipange upya katika kasi ya kudai hatimiliki ili iweze kusimamia na kuendeleza miradi ya maendeleo ambayo maandio yake wameshayaandaa.

### 6.12 OFISI YA MKOA WA KUSINI UNGUJA

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, inatekeleza majukumu yake ya kazi kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Tawala za Mikoa Namba 8 ya Mwaka 2014 sambamba na kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Sheria Namba 7 ya Mwaka 2014:

Kwa mwaka 2024/2025 Mkoa wa Kusini Unguja ulipanga kutekeleza shughuli mbali mbali zikiwemo kuratibu na kusimamia shughuli za kiseka, kuratibu ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na mwenge wa Uhuru, kufanya vikao vya kamati ya ulinzi na usalama, kuratibu Mpango wa Kitaifa wa ukomeshaji wa Vitendo vya Udhalilishaji wanawake na watoto, kufanya kikao cha Baraza la Biashara la Mkoa, kutoa stahiki za Wafanyakazi na kuipatia Ofisi vitendea kazi.

**Mafanikio yaliyopatikana kwa Ofisi ya Mkoa wa Kusini Unguja.**

Katika utekelezaji wa majukumu ya Mkoa huu, mafanikio makubwa yamepatikana ikiwa ni pamoja na:

*(i)* Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za jamii katika Mkoa

*(ii)* Kuimarika kwa ulinzi na usalama pamoja na sekta za uchumi
*(iii)* Kuongezeka muamko kwa wananchi katika usajili vizazi kwa wakati.
*(iv)* Kuimarika kwa mashirikiano baina ya Ofisi ya Mkoa na wadau wengine.
*(v)* Kuanzishwa kwa mfumo wa mawasiliano ya kiofisi kwa njia ya kielektroniki ndani ya Ofisi.

**Changamoto za Mkoa wa Kusini Unguja**

Katika jitihada za kukuza uchumi wa nchi na kupunguza umasikini katika jamii, hatuna budi kukabiliana na changamoto ambazo zinatukwaza katika maendeleo yetu. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:

*(i)* Uingiaji mkubwa wa watu kutoka sehemu mbalimbali ambao kwa kiasi fulani unaathiri utamatuni wa asili.
*(ii)* Muamko mdogo wa wananchi katika suala la uhaulishaji ardhi;
*(iii)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri;
*(iv)* Uhaba wa fedha za matumizi mengineyo.

**Maagizo ya Kamati kwa Mkoa wa Kusini Unguja:**

Kamati kujenga mustakbali uliobora na wenye kuleta ufanisi wa mafanikio ya wananchi wetu, hatunabudi kuishauri Serikali ya Mkoa huu kukabiliana na changamoto hizi.

Aidha, Kamati inashauri kama ifuatavyo:

*(i)* Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa Mikoa juu ya kuwapatia vyombo vya usafiri ikiwemo kuingiza katika bajeti ya 2025/2026.

*(ii)* Kamati inashauri Mkoa uendeleze juhudi za kupambana wale wote wanaokwenda kinyume na utamaduni na silka za wazanzibari kwa kufanya ziara za mara kwa mara katika maeneo ya starehe na fukwe.

*(iii)*Mkoa ushirikiane na Wizara ya ardhi kutoa elimu katika jamii juu ya umuhimu wa uhaulishaji ardhi.

*(iv)*Kamati inaishauri Serikali kulitafutia ufumbuzi suala la fedha za matumizi mengineyo kwani imekua ni kilio cha Mkoa.

## 6.13 BARAZA LA MJI KATI

Baraza la Mji Kati ni miongoni mwa Serikali za Mitaa ambayo imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa Nam. 7 ya Mwaka 2014 na imekasimiwa majukumu yake kwa mujibu wa sheria hiyo. Kamati imefuatilia vya kutosha utekelezaji wa majukumu ya Baraza na kujionea jinsi wanavyojitahidi katika kufikia malengo waliyokusudia.

Ofisi ya Baraza la Mji Kati, kwa mwaka 2024/2025, imeweza kutekeleza Majukumu yake kupitia mambo makuu Manne (4) ikiwemo ukukusanyaji wa Mapato, Miradi ya Maendeleo, Usafi wa mazingira na uendeshaji wa shughuli za ofisi .

**Changamoto zinazolikabili Baraza la Mji Kati:**

Baraza la Mji Kati linakabiliwa zifauatazo: -

*(i)* Kukwama kwa malipo kunakosababisha na Mfumo wa ZANMUTM kuwa chini kutokana na kukatika umeme mara kwa mara.

*(ii)* Kuwepo kwa uhaba wa wafanyakazi wenye taaluma mbali mbali akiwemo Afisa mapato.

(iii) Tatizo la uchakavu na uhaba wa gari za kuzolea taka unaorudisha nyuma kufanya usafi wa Mji.
(iv) Kutopata fedha za gawio kwa wakati au ada kutoka Taasisi zinazohudumu katika wilaya ya Kati, kwa mfano idara ya misitu ambayo wanapokea wageni katika msitu wa Jozani.
(v) Kuchelewa kupata majibu kutoka taasisi za serikali pale Baraza linapoomba mashirikiano kwa mfano kuomba ruti mpya za gari.
(vi) Kuchelewa kupata hati miliki za maeneo ya Baraza na kuchelewa kupimiwa kwa maeneo mapya.

**Maagizo ya Kamati:**

Ili kuweza kufikia hatua ya mafanikio katika Baraza la Mji Kati na kufikia hatua iliyokusudiwa, Kamati inashauri mambo yafuatayo:

(i) Kamati inaishauri Serikali kuwapatia Baraza watumishi wenye weledi wa mapato kwa kutumia taaluma yao katika kubuni na kuendeleza vyanzo vya mapato.
(ii) Kamati inalishauri Baraza kusimamia usafi wa mazingira yake katika maeneo mbali mbali ikiwemo hoteli na makaazi ya watu.
(iii) Kamati inalitaka Baraza kuzidisha kasi ya ukusanyaji wa mapato pamoja na kusimamia mifumo yake ya mapato na kuwashajihisha wafanyabiashara kulipa tozo na ada kwa wakati.

## 6.14 HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA

Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja ni miongoni mwa taasisi za Serikali za Mitaa ambayo imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa, Namba 8 ya Mwaka 2014.

Katika utekelezaji wa majukumu ya Halmashauri hii, Kamati imeelezwa mafanikio yafuatayo:

*(i)* Kufungua rasmi kiwanja cha kufurahishia Watoto cha Paje katika kuadhimisha sherehe za miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

*(ii)* Kuendelea kufanya usafi wa mazingira ndani ya Wilaya ya Kusini kwa kuchukua taka katika baadhi ya Mahoteli ya Wilaya hiyo na kwenda kuzitupa katika jaa kubwa Kibele.

*(iii)* Kuimarisha na kuvuka malengo ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kwa kusimamia vyema vyanzo vya mapato na kuzidisha kasi ya ukusanyaji kwa wakati.

*(iv)* Kuuvuka malengo ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kwa kusimamia vyema vyanzo vya mapato na kuzidisha kasi ya ukusanyaji ambapo kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba 2024) imefikia asilimia 147 ya ukusanyaji mapato.

**Changamoto za Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja**

Mbali ya mafanikio hayo ambayo Halmashauri imefanikiwa kuyapata, bado Kamati imebaini changamoto kadhaa ambazo kimsingi zinafanana na Halmashauri nyengine za Zanzibar. Changamoto zenyewe ni kama zifuatazo:

*(i)* Uhaba wa vitendea kazi vya kisasa katika ukusanyaji wa mapato.

*(ii)* Uelewa mdogo wa wananchi katika ukusanyaji wa mapato na kulinda vyanzo vya mapato.

*(iii)* Uhaba wa vyombo vya usafiri kwa watendaji wa Halmashauri.

*(iv)* Uhaba wa watendaji wa Halmashauri hususan wataalamu wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha katika fani za miradi na mapato.

*(v)* Uwepo wa tatizo la wizi wa mifugo, ukosefu wa malisho na elimu ndogo ya ufugaji wa kibiashara kwa wakulima.

**Maagizo ya Kamati kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja**

*(i)* Kamati imeridhishwa na kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa kiwanja cha kufurahiushia watoto Paje kwani kitapunguza masafa ya watoto kufuata huduma hizo Mkoa wa Mjini Magharibi.

*(ii)* Kamati inashauri Halmashauri kuzidisha kasi ya usajili wa wajasiriamali ili kupata takwimu zao halisi na kuwafikia katika shughuli mbali mbali.

*(iii)* Kamati inaigiza Halmashauri kuzidisha kasi ya kufanya usafi katika maeneo yake ya kitalii na kuboresha maeneo yote ambayo yanatumika kwa biashara. Aidha, Halmashauri inaweza kutafuta vikundi vya vijana na kuwatumia kwa ajili ya kufanya usafi wa maeneo yake.

*(iv)* Kamati inashauri Halmashauri kuongeza mikakati zaidi juu ya ukusanyaji wa mapato, kuimarisha makusanyo na matumizi bora ya fedha na uendelezaji wa vyanzo vya mapato.

*(v)* Kamati inaishauri Halmashauri kuzidisha usafi katika maeneo ya kitalii na kusimamia shughuli zote zinazofanyika katika maeneo yao.

*(vi)* Kamati inaigiza Halmashauri kutafuta wawekezaji wazalendo ambao watafanya kazi za ukusanyaji taka mahoteli na kuachana na kampuni ambazo hazitekelezi maagizo ya mkataba.

*(vii)* Kamati inaishauri Halmashauri kufuatilia deni wanaloidai kampuni ya usafi iliyoshindwa kufanya kazi kwa mujibu wa mkataba na hivyo kukimbia bila ya kurejesha fedha ambazo walitakiwa kulipa kwa mujibu wa mkataba.

## 6.15 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Mkoa wa Kaskazini Unguja ni miongoni mwa Mikoa mitano ya Zanzibar ambao umeanzishwa chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa, nambari *8* ya mwaka *2014* ikiwa na jukumu la kuratibu shughuli za maendeleo ndani ya Mkoa, Utawala, Usimamizi na uendeshaji wa Serikali za Mitaa kama yalivyotajwa katika kifungu Nam. 12(3)(a)(i), pamoja na kusimamia Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinazoongozwa na Sheria ya Serikali za Mitaa Nam. 7 ya mwaka 2014.

Mkoa wa Kaskazini Unguja unajumla ya Wilaya mbili; Wilaya ya Kaskazini "A" na Wilaya ya Kaskazini "B" pamoja na Halmashauri za Mabaraza ya Miji; Baraza la Manispaa Kaskazini "A" na Baraza la Mji Kaskazini "B".

## 6.16 BARAZA LA MANISPAA KASKAZINI "A"

Baraza la Manispaa Kaskazini "A" Unguja ni moja ya Mabaraza mawili yaliyomo katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na linalotekeleza kazi zake kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo Zanzibar 2020 – 2050, ilani ya Chama cha Mapinduzi na Mpango Mkakati wa Baraza la Manispaa Kaskazini "A" 2019 -2024 pamoja na maelekezo ya Viongozi wa juu.

Baraza la Manispaa Kaskazini "A" limepata mafanikio mbali mbali kutokana na utekelezaji wake na usimamizi madhubuti ya fedha za bajeti. Miongoni mwa mafanikio yake ni kama ifuatavyo:

*(i)* Kufanya usafi kwa kushirikiana na Mawakala wa Baraza la Manispaa katika maeneo ya Biashara ya jamii.
*(ii)* Kuweza kumalizia ujenzi na kuzindua soko la Mkwajuni kwa hatua ya Awali.
*(iii)* Kuongezeka kwa kiwango cha ukusanyaji wa Mapato;

**Changamoto za Baraza La Manispaa Kaskazini "A" Unguja**

Baraza la Mji Kaskazini 'A' Unguja, linakabiliwa na changamoto tofauti ambazo zinarudisha nyuma maendeleo yao, miongoni mwa changamoto hizo:

*(i)* Upungufu wa watumishi wa kudumu hasa katika maeneo ya ukusanyaji Mapato na Usafi;

*(ii)* Ucheleweshaji wa marejesho ya mgao wa fedha zinazotokana na Mali asili;

*(iii)* Mkanganyiko wa sheria na kanuni katika ukusanyaji wa tozo mfano leseni za nyumba za kulala wageni.

*(iv)* Kampuni zinazopewa jukumu la ukusanyaji wa taka kutofuata matakwa ya mikataba wanayopatiwa na hivyo kushindwa kufanya malipo kwa wakati na kusababisha hasara kwa Manispaa.

*(v)* Kamati inasikitishwa na kuwepo kwa deni kubwa kutoka moja ya kampuni zinazofanya usafishaji katika Manispaa hali inayopelekea mji kutokuwa na hali ya kuridhisha.

**Maagizo ya Kamati**

Kutokana na changamoto hizo ambazo tumezibainisha Kamati bado inaendelea kushauri yafuatayo:

*(i)* Baraza lishirikishe vikundi viweze kusimamia usafi katika ngazi za shehia;

*(ii)* Kamati inalishauri Baraza liendelee na jitihada za kutafuta wawekezaji katika maeneo mbalimbali ikiwemo miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa kiwanja cha kisasa cha kufurahishia Watoto Nungwi, Nyumba za makaazi Matemwe,

Maegesho ya kisasa mkokotoni, nyumba za bei nafuu Mtowapwani na ujenzi wa jumba la kibiashara;

*(iii)* Kamati inashauri kuimarisha na kuibua vyanzo vipya vya mapato ikiwemo chanzo cha ushuru wa huduma na Tozo.

*(iv)* Kamati inashauri Baraza kukaa pamoja na wawekezaji wa kampuni za usafi kwa lengo la kutafuta suluhu ya kudumu kwenye mikataba yao na endapo watakataa kufanya hivyo, basi Baraza litafute wawekezaji wengine wazalendo wenye kufuata matakwa ya Baraza.

*(v)* Kamati inaagiza kampuni ya usafi yenye deni la Baraza la Manispaa kulipa deni hilo kwa haraka na kwa kufuata makubaliano ya mkataba waliofunga na Manispaa hiyo.

## 6.17 BARAZA LA MJI KASKAZINI "B"

Baraza la Mji Kaskazini "B" Unguja ni moja ya Mabaraza mawili yaliyomo katika Mkoa wa Kaskazini Unguja yalioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Miji Sheria namba 7 mwaka 2014 kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa.

Katika utekelezaji wa malengo ya Baraza kwa mwaka 2024/2025 Kamati imeridhishwa na juhudi za uongozi wa Baraza kwa ajili ya kuimarisha maendeleo yake.

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni haya yafuatayo:

*(i)* Kuendelea kutoa huduma bora kwa jamii, ikiwemo kuwapatia taaluma wananchi juu ya usafi wa mazingira na ulipaji wa ada kwa hiari.

*(ii)* Baraza kuendelea kusajili wajasiriamali wadogo wadogo kwa lengo la kuboresha maendeleo yao.

**Changamoto Za Baraza La Mji Kaskazini "B"**

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, pia zipo changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa shughuli za Baraza, miongoni mwa changamoto hizo ni kama ifuatavyo:

a) Ufinyu wa miradi ya maendeleo yenye tija kwa Baraza.
b) Kamati imebaini Baraza linakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha za matumizi ya (OC). Hii inapelekea kukosekana kwa baadhi ya huduma muhimu za ofisi na kupelekea ugumu wa utekelezaji wa kazi za kila siku,
c) vile vile, kuchelewa kwa fedha za marejesho kutoka mali zisizorejesheka.
d) kuekewa kima kidogo cha bajeti kulingana na uhalisia wa huduma nyingi inazozisimamia na kuziratibu katika jamii.

**Maagizo ya Kamati**

Katika kukabiliana na changamoto hizo juhudi na mikakati mbalimbali inahitajika ili kuona changamoto hizo zinapatiwa ufumbuzi katika hatua kwa hatua. Hivyo, basi Kamati inashauri mambo yafuatavyo:

*(a)* kamati inaishauri Serikali kutafuta miradi ya vitega uchumi ambayo itasaidia kukuza maendeleo yake.
*(b)* Baraza liendelee kutoa elimu juu ya ulipaji kodi kwa hiari.
*(c)* Kamati inashauri Serikali kulisaidia Baraza la Mji Kaskazni B kwa kuwapatia fedha za marejesho ya mali zisizorejesheka kwa wakati.
*(d)* Baraza liandae na liweke kipaumbele kwa watumishi wake katika kupata elimu ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa wataalamu.

## 6.18 OFISI YA MKOA WA KUSINI PEMBA

Mkoa wa Kusini Pemba umeanzishwa chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa, nambari *8* ya mwaka *2014* na inatekeleza shughuli zake za Kuratibu na Kusimamia Shughuli za Serikali Katika Ngazi ya Mkoa, Wilaya na Shehia zake, Kusimamia Utawala na Uendeshaji wa Ofisi na Kusimamia Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

**Mkoa unaendelea kupata mafanikio makubwa, miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-**

*(i)* Kuimarika kwa hali ya amani, ulinzi na usalama katika maeneo yote ya Mkoa hali inayopelekea wananchi kufanya shughuli zao za kijamii na kiuchumi kwa utulivu mkubwa.

*(ii)* Kupungua kwa idadi ya migogoro ya ardhi unaotokana na kasi ya utendaji wa kamati ambayo hutoa elimu ya uhaulishaji wa ardhi kwa wananchi.

*(iii)* Wananchi kutumia vyema Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana juu ya mirathi.

*(iv)* Mkoa unaendelea kupambana dhini ya matukio ya udhalilishaji wa wanawake na Watoto ambapo matukio mbali mbali yamepatiwa ufumbuzi Mahakamani.

**Changamoto zinazoukabili Mkoa wa Kusini Pemba:**

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku bado kuna changamoto ambazo Kamati imezibaini na zinafaa kuchukuliwa hatua. Changamoto zenyewe ni kama zifuatavyo:

*(i)* Kuongezeka kwa uingiaji na utumiaji wa dawa za kulevya mijini na vijijini.

*(ii)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri katika Ofisi za Mikoa na Wilaya.

*(iii)* Athari za mabadiliko ya tabianchi kwa wakulima na wajasiriamali.

*(iv)* Uwepo wa tabia mbaya za wizi wa mazao na mifugo kwa baadhi ya maeneo.

*(v)* Tatizo la baadhi ya wananchi kutolipa kodi kwa hiari pamoja na kutotoa risiti za mashine.

**Maagizo ya Kamati**

*(i)* Kamati inaishauri Serikali kuongeza udhibiti wa uingiaji na utumiaji wa dawa za kulevya.

*(ii)* Kamati inashauri watendaji wa Mkoa kuzidisha kasi ya utendaji ili kumsaidia Mkuu wa Mkoa kwa kutoa huduma bora katika jamii.

*(iii)* Kamati pia, inashauri Mkoa kutoa elimu ya mara kwa mara kwa wananchi juu ya kulipa kodi kwa hiari.

*(iv)* Kamati inauagiza Mkoa kuchukua hatua za makusudi kwa kuwafuatilia na kupambana na watu wenye tabia ya wizi wa mazao na mifugo.

## 6.19 BARAZA LA MANISPAA CHAKE CHAKE

Baraza la Mji la Chake – Chake ni moja ya Mabaraza mawili yaliyomo katika Mkoa wa Kusini na inaendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku kupitia malengo makuu ya kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya Mji wa Chake Chake, Kukusanya mapato, kuanzisha na kuendeleza miradi ya maendeleo ya wananchi.

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni haya yafuatayo:

*(i)* Kuongezeka kwa kasi ya ukusanyaji wa mapato na kuongeza vyanzo vipya vya mapato katika maeneo ya mjini ikiwemo bustani ya Mwanamashungi;

*(ii)* Kuimarika kwa huduma za uendeshaji na Kuwajengea uwezo wafanyakazi;
*(iii)* Kuimarika kwa usafi wa mazingira katika maeneo ya Miji na vijijini;
*(iv)* Kuyawezesha makundi maalum kujiimarisha kiuchumi;
*(v)* Kuendelea kwa ujenzi wa soko la samaki na matunda la Machomane; na
*(vi)* Kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa soko la wajasiriamali Michakaini.

**Changamoto zinazolikabili Baraza La Mji Chake – Chake:**

Pamoja na kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato na kukuwa kwa hali ya usafi wa Mji kwa kuzifikia Shehia nyingi zaidi bado Ofisi ya Baraza la Mji Chake – Chake inakabiliwa na changamoto kadhaa katika utekelezaji wa majukumu yake. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatavyo: -

*(i)* Uhaba wa gari ya kubebea taka na kunyonyea maji taka.
*(ii)* Uhaba wa watendaji wataalamu katika baadhi ya idara.
*(iii)* Uelewa na utayari mdogo wa jamii kwenye ulipaji wa kodi.

**Maagizo Kamati**

*(a)* Kamati inaagiza Baraza kusimamia kikamilifu miradi yake ya maendeleo kwa lengo kulinda rasilimali za Serikali na wananchi.
*(b)* Kamati inashauri Baraza kufanya juhudi za makusudi kutafuta mtaalamu atayeboresha mfumo wa mashine za ukusanyaji wa mapato ili kuzuia mianya ya upoteaji wa mapato. Aidha, ni vyema kama Baraza litakuwa na mtaalamu ambaye atatumika kufanya marekebisho kila atakapohitajika.
*(c)* Kamati inalitaka Baraza pia, lijikite katika usafi wa mji, na kutoa huduma kwa jamii kwani hizo ndio kazi kuu za Mabaraza kwa

mujibu wa Sheria. Kamati inaliagiza Baraza la Manispaa kuajiri kampuni za kizalendo katika ukusanyaji wa taka majumbani.

*(d)* Kamati inashauri Baraza liendelee kutoa elimu kwa wafanya biashara kutoa risiti na kudai risiti katika biashara zao.

*(e)* Kamati inaliagiza kujenga eneo la maegesho ya magari na bustani katika soko la Michakaini.

*(f)* Kamati inalitaka Baraza kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vyake licha ya changamoto zinazojitokeza wakati wa uendeshaji wa zoezi hili.

## 6.20 BARAZA LA MJI MKOANI – PEMBA

Baraza la Mji Mkoani ni moja ya Mabaraza yaliyomo katika Mkoa wa Kusini Pemba lilioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Miji Sheria namba 7 mwaka 2014 kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa. Katika utekelezaji wa malengo ya Baraza kwa mwaka 2024/2025, Kamati yetu imeridhika na malengo ya Baraza kwa ajili ya kuimarisha maendeleo yake.

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni haya yafuatayo:

*(i)* Baraza kupitia makusanyo yake ya ndani liliendelea kufanya malipo ya ujenzi wa Soko la Mtambile na uwekaji wa kifusi katika Stendi ya kipitacho.

*(ii)* Baraza liliendelea kuendeleza na kusimamia miradi ya maendeleo ya wananchi na Wajasiriamali kupitia fedha za mapato ya ndani pamoja na mifuko ya Majimbo

*(iii)* Baraza limefanikiwa kufanya zoezi la usafi wa mazingira, ikiwa ni pamoja na kufanya Operesheni maalum ya usafi wa miji kwa ukataji majani, kuhamisha majaa yasiyo rasmi katika jamii, sambamba na kufanya usafi wa pamoja kwa Wilaya nzima.

**Changamoto zinazoikabili Baraza La Mji Mkoani**

Licha ya Baraza kufanikiwa katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku kwa ufanisi na uwazi zaidi lakini bado kuna changamoto mbali mbali zinazolikabili ili kufikia malengo ya shughuli zao kwa asilimia mia moja, miongoni mwa Changamoto hizo ni pamoja na:

*(i)* Uhaba wa gari za kubebea taka na kunyonyea maji taka ndio kikwazo kikubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza.
*(ii)* Uhaba wa wataalamu katika baadhi ya idara.
*(iii)* Upungufu wa fedha za matumizi mengineyo ukilinganisha na mahitaji yaliyopo;
*(iv)* Kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato katika vyanzo mbali mbali vya mapato;
*(v)* Ufinyu wa Ofisi ukilinganisha na wafanyakazi waliopo ambapo hulazimika kila chumba kutumiwa na wafanyakazi zaidi ya wawili;

**Maagizo ya Kamati**

*(i)* Kamati inalipongeza Baraza kwa kuimarisha usafi wa mji na kuwa katika hali nzuri. Hata hivyo, juhudi zaidi zinahitajika kwa lengo la kuwa mfano bora kwa mabaraza mengine.
*(ii)* Kamati inakiagiza Baraza kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ili kuimarisha miradi yake.
*(iii)* Kamati inalitaka Baraza kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza ufanisi wa makusanyo.
*(iv)* Ili kukabiliana na changamoto ya ufinyu wa Ofisi, Kamati inashauri Baraza kutumia jengo la ofisi kwa kazi maalum na kazi nyengine zifanywe nje ya ofisi kama ni ‘outreach programs’.

## 6.21 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Mkoa wa Kaskazini Pemba, ni moja kati ya Mikoa Mitano ya Zanzibar, Kijiografia Mkoa una ukubwa wa kilomita za mraba 574 km2 (222 sqm). Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa upande wa Kusini umepakana na Mkoa wa Kusini Pemba na kwa upande wa Kaskazini, Mashariki na Magharibi umepakana na Bahari ya Hindi.

Mkoa wa Kaskazini Pemba umeunganishwa na Wilaya Mbili (2), Wilaya ya Wete na Wilaya ya Micheweni pamoja na Wilaya ndogo ya Kojani.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Mkoa wa Kaskazini Pemba umefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

*(i)* Kuimarisha hali ya ulinzi na usalama wa Mkoa.

*(ii)* Kuimarika kwa kampeni ya mapambano dhidi ya udhalilishaji na ukatili ndani ya Mkoa.

*(iii)* Kuimarika kwa utoaji wa huduma za afya katika jamii.

*(iv)* Mkoa umejitahidi katika kusimamia mifumo ya elimu ili kwenda sambamba na sera ya taifa.

**Changamoto za Mkoa wa Kaskazini Pemba**

Mkoa huu katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo:

*(a)* Ufinyu wa nafasi za ofisi kulingana na idadi ya wafanyakazi.
*(b)* Ufinyu wa Bajeti kutokana na mahitaji ya ofisi.
*(c)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri.

*(d)* Kuwepo kwa kesi za wizi wa mifugo na mazao katika maeneo mbali mbali ya Mkoa.

**Maoni na ushauri wa Kamati**

*(i)* Kamati inauagiza Mkoa kuzidisha kasi ya kuzisimamia Halmashauri zake kwa lengo la kuongeza kasi ya mapato na usafi wa miji.

*(ii)* Kuhusu suala la bajeti, Kamati inaitaka Ofisi kufanya maombi kwa kufuata utaratibu maalumu wa maombi na kuyawasilisha katika wizara husika ili kupata nyongeza ya bajeti.

*(iii)* Kamati pia, inaishauri Serikali kuongeza fedha za matumizi maalum (Political Votes) kutokana na kiwango kidogo kilichopo ambacho kinaleta changamoto kwa waheshimiwa Wakuu wa Mikoa.

*(iv)* Mkoa uongeze kasi ya kusimamia na kufuatilia vitendo vya wizi wa mifugo na mazao ya wananchi.

## 6.22 BARAZA LA MJI WETE

Baraza la Mji Wete ni miongoni mwa Mamlaka mbili za Serikali za Mitaa zilizomo ndani ya Mkoa wa Kaskazini Pemba. Baraza hili limeundwa kwa jumla ya wadi kumi zenye madiwani kumi na tisa (19), kati yao madiwani kumi (10) ni wakuchaguliwa ni wananchi na tisa (9) ni wa kuteuliwa na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

Mafanikio yaliyofikiwa na Baraza la Mji Wete ni kama yafuatayo:

(i) Baraza la Mji Wete limefanikiwa kuboresha usafi wa miji, kukusanya Tani 1,620 za taka, sawa na asilimia 90% ya makadirio na kuzipeleka jaa kuu la Magombani katika Shehia ya mzambaru takao.

(ii) Baraza limefanikiwa kufanya ukaguzi wa Nyumba 170 katika shehia za mbalimbali ambapo jula ya nyumba 100 hazikua katika hali nzuri.

(iii) Baraza katika Uwezeshaji wa Makundi Maalum lilifanikiwa kukusanya Shilingi 3,183,916/= Makusanyo yake ya ndani na kuzipeleka katika Mfuko wa Wizara ya Uwezeshaji Wananchi kiuchumi kwa ajili ya kuwasaidia Wajasiriamali na Watu wenye Mahitaji Maalum wakiwemo, Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

(iv) Baraza la Mji wete kwenye Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo linaendelea kusimamia ujenzi wa Soko la Matunda na Mboga mboga katika eneo la Mzambarau Takao ambalo litasaidia upatikanaji wa huduma kwa wananchi na kuboresha mazingira ya biashara kwa jamii.

**Changamoto za Baraza la Mji Wete**

Afisi ya Baraza la Mji Wete inakabiliwa na changamoto kadhaa katika utekelezaji wa majukumu yake, miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:

*(i)* Uchakavu na ubovu wa gari la kuzolea taka.

*(ii)* Kutokuingiziwa fedha za Makusanyo kwa wakati, Mfano fedha za Maliasili zisizorejesheka

*(iii)* Uhaba na uchakavu wa Vitendea kazi ikiwemo gari za Ufuatiliaji wa kazi na shughuli nyengine za kiofisi.

**Maagizo ya Kamati**

*(i)* Kamati inaliagiza Baraza kufatilia maelekezo waliyotoa ya kuziweka Nyumba walizozifanyia ukaguzi katika hali ya Usafi ikiwemo kufanya maboresho pamoja na kupatiwa Elimu ya Afya**.**

*(ii)* Kamati inalitaka Baraza la Mji Wete kuandaa mpango maalumu utakaowawezesha kupata vyombo vya usafiri na gari za kuzolea taka ikiwa ni pamoja na kuwatumia wataalamu katika kuandaa miradi ya kimaendeleo kupitia nchi Wahisani na Taasisi za Fedha;

*(iii)* Kamati inashauri Baraza kuendelea kutoa elimu ya ulipaji kodi kwa wananchi ili kuzidisha kasi ya ukusanyaji wa mapato.

*(iv)* Kamati inaliomba Baraza kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vyake ili kusaidia ongezeko la miradi ya maendeleo.

*(v)* Kamati inaliagiza Baraza kutosita kuwapatia vitambulisho wajasiriamali ambao tayari wamesajiliwa kwa madhumuni ya kuwafanya wawe huru katika kazi zao.

*(vi)* Kamati pia inalitaka Baraza kubuni vyema vyanzo vya mapato na kujikita kutumia mashine za ukusanyaji mapato. Kwani Kufanya hivyo kutapelekea Barara hilo kuimarika na kutokuwa tegemezi kwa kiasi kikubwa.

## 6.23 HALMASHAURI WILAYA YA MICHEWENI

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ni miongoni mwa mamlaka 11 za Serikali za Mitaa Zanzibar na ni moja kati ya Mamlaka mbili za Serikali za Mitaa zilizomo ndani ya mkoa wa Kaskazini Pemba. Halmashauri hii imeundwa kwa Wadi nane (8) zenye Madiwani nane (8) wa kuchaguliwa, Madiwani watatu (3) wa viti maalum na Madiwani watano (5) wa kuteuliwa na Mhe, Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa hapa Zanzibar.

Aidha, Wilaya imegawika katika kanda mbili kimaumbile, Kanda ya Mashariki, ambayo ardhi yake ni ya mawe na kanda ya Magharibi ambayo ardhi yake ni yenye rutuba nzuri kwa kilimo.

Katika utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa 2024/2025 Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imefanikiwa katika mambo yafuatayo:

(i) Wilaya na shehia zake kuendelea kuwa salama, amani na utulivu na kuweza kupungua kwa vitendo vya dawa za Kulevya.
(ii) Wilaya imefanikiwa kupunguza matukio ya udhalilishaji kwa kiwango kikubwa ukilinganisha na kipindi kilichopita.

(iii) Kuongezeka kwa uwajibikaji kwa watendaji katika kutoa huduma bora.

**Changamoto zinazoikabili Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni**

Katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Halmashauri inakabiliwa na Ukosefu wa Vifaa vya usafi kama vile gari za kubebea taka hali inayosababisha shughuli za uzowaji taka kutokufanyika kwa wakati.

*(ii)* Uhaba wa Wafanyakazi jambo ambalo huzorotesha utekelezaji wa kazi ya Halmashauri.

*(iii)* Wafanyabiashara waliowengi hawatumii mashine za risiti na hivyo kushindwa kutoa risiti kwa mujibu wa utaratibu uliopo.

*(iv)* Kumekuwa na Mwamko mdogo wa wananchi katika kulipa ada na tozo.

*(v)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri vinavyorudisha nyuma shughuli za ufuatiliaji katika halmashauri.

**Maagizo ya Kamati kwa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni**

*(i)* Kwa kuwa halmashauri imewasilisha changamoto ya ukosefu wa vifaa vya usafi kupitia Mradi wa Big Z na imeahidiwa kupatiwa Magari ya kubebea taka Kamati inaishauri Halmashauri kufuatilia maombi hayo ili vifaa hivyo viweze kupatikana kwa haraka.

*(ii)* Kamati pia, inaridhishwa na ujenzi wa kituo cha Daladala cha Konde na inaagiza ujenzi huu ukamilika kwa wakati ili kuongeza vyanzo vya mapato.

*(iii)* Kamati inaitaka Halmashauri kuendelea kuwasajili wajasiriamali na kuwapatia vitambulisho kwa lengo la kufahamu mahitaji yao.

*(iv)* Kamati inashauri Halmashauri kuendelea kutoa elimu ya ulipaji kodi kwa wananchi ili kuzidisha kasi ya ukusanyaji wa mapato.

*(v)* Kamati inaiagiza Halmashauri kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vyake ili kusaidia ongezeko la miradi ya maendeleo.

*(vi)* Kamati inaitaka Halmashauri kuongeza juhudi za utumiaji wa mashine za ukusanyaji mapato na kutumia vyema vyanzo vya mapato ambavyo wanavipata.

## 6.24 AFISI YA MRAJIS WA JUMUIYA ZISIZO ZA KISERIKALI (NGOs) ZANZIBAR

Afisi ya Mrajis wa Jumuiya zisizo za Kiserikali Zanzibar katika kutekeleza majukumu yake ya kazi ya Usajili, Uratibu na kuzisimamia Jumuiya Zisizo za Kiserikali (NGO's) inaendesha majukumu yake kwa kufuata Sera ya Jumuiya zisizo za Kiserikali ya mwaka 2009 na Sheria Namba 6 ya mwaka 1995.

Kwa upande wa utekelezaji wa bajeti, afisi hii inahusika na programu ndogo ya kuratibu Jumuiya zisizo za Kiserikali yenye lengo kuu la kuanzisha mazingira bora ya NGO's ili ziweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi nchini.

**Mafanikio ya Afisi ya Mrajis wa Jumuiya zisizo za Kiserikali**

Kiufupi mafanikio yake ni mengi na yanahusisha nyanja zote za kiuchumi, kisiasa na kijamii kutokana na mchango wake mkubwa unaotokana na kazi za jumuiya hizo.

Kamati inaipongeza kwa dhati Afisi ya Mrajis kwa kuweza kuratibu na kusimamia vyema utendaji kazi wa jumuiya zisizo za kiserikali (NGO's) kwa kufanikiwa kuboresha takwimu za usajili wa jumuiya kupitia Mfumo wa Usajili wa Kielekroniki (ORS) na kuzitambua jumuiya zote

ambazo hazimo katika Mfumo wa (ORS) kwa lengo la kurahisisha usimamizi bora na ufutiliaji wa karibu wa utendaji wake.

Imeelezwa kwamba Afisi pia, imefanikiwa kuzifutia usajili jumuiya ambazo hazipo hai kutokana na kushindwa kukidhi matakwa ya katiba zao na muongozo wa kisheria wa kuwasilisha ripoti za utekelezaji wa majukumu yao katika Afisi ya Mrajis licha ya ukumbusho wanaopatiwa mara kwa mara.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Afisi**

*(i)* Kamati inaiagiza afisi kuhakikisha wanazisimamia na kuzifuatilia kwa karibu jumuiya zote zilizopata usajili na kutekeleza kazi zake hapa nchini ili kubaini uhalali wa kazi zao.

*(ii)* Kamati vile vile, inaishauri afisi kuzichukulia hatua stahiki jumuiya zote zinazokwenda kinyume na malengo yake ya usajili kwa mujibu wa katiba zao na sheria za nchi.

*(iii)* Katika kipindi hiki tunachoelekea cha uchaguzi mkuu wa 2025, kamati inaiomba Afisi ya Mrajis kusimamia jumuiya zake kwa kuzihimiza kulinda na kudumisha amani na utulivu uliopo nchini ili zisijihusishe na viashiria vinavyochochea kuvunjika kwa amani na mshikamano uliojengwa kwa muda mrefu.

## 6.25 WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, nambari *3* ya mwaka *2018*.

Majukumu ya Wakala ni pamoja na kusajili matukio ya Kijamii (Ndoa, Talaka, Vizazi, Vifo na Utambulsho. Kutoa vyeti na vitambulisho. Kutunza kumbukumbu za matukio ya kijamii pamoja na kutunza mapato yanayotokana na huduma za usajili kwa niaba ya Serikali.

**Mafanikio ya Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar**

*(a)* Kuingiza kumbukumbu za kizazi hai kwenye mfumo wa usajili wa kielektroniki (CRVS) kutoka kwenye nakala ngumu na kulifanya zoezi la usajili, uthibitishaji na upataji wa vyeti kwenda kwa njia ya haraka.

*(b)* Kuimarisha mfumo wa kiusalama katika majengo ya ZCSRA kwa kufunga kamera za ufuatiliaji katika majengo yanayozalishwa vitambulisho.

*(c)* Kukamilisha kazi ya utengenezaji wa moduli ya uhakiki vyeti yenye lengo la kuwarahishia wananchi mbali mbali na wanafunzi wa bodi za mikopo ya elimu ya juu kuhakiki vyeti.

*(d)* Kufunga mfumo wa usimamizi na ufatiliaji wa miundombinu ya usajili.

**Changamoto zinazoikabili Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar**

Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii katika utekelezaji wa majukumu yake inakuwa ikipambana na changamoto zifuatazo:

*(i)* Ofisi kukabiliwa na madeni makubwa yanayopelekea kukosa baadhi ya huduma kwa baadhi ya watoa huduma kutokana na kuchelewa kuingiziwa fedha za matumizi mengineyo.

*(ii)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri katika vituo vya Wilaya na ofisi kuu Unguja na Pemba.

*(iii)* Ufinyu wa ofisi na ukosefu wa vitendea kazi kwa ofisi za Wakala ikiwemo vifaa vya kielektroniki jambo ambalo linarejesha nyuma juhudi za utendaji kazi.

*(iv)* Ufinyu wa nafasi katika ofisi za wilaya ya Wete, Mwera wilaya ya Magharibi *A* na Gamba wilaya ya Kaskazini *B* ambapo hupelekea utoaji huduma usioridhisha kwa wananchi.

**Maagizo ya Kamati kwa Ofisi ya Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar**

*(i)* Kamati inashauri Serikali kuiangalia Afisi ya usajili Wilaya ndogo Tumbatu kwa kuwezesha watendaji wake kimaslahi ili kutoa huduma bora kwa jamii.

*(ii)* Kamati inaitaka Wakala kuweka umuhimu katika usajili wa matukio ya kijamii ikiwemo vizazi, vifo, ndoa na talaka na vitambulisho ili kupunguza mikusanyiko ya watu katika vituo vyao.

*(iii)* Kamati inaishauri Serikali kuzidi kuziboresha ofisi za usajili wa matukio ya kijamii wilayani ili wananchi wapatiwe huduma za uhakika na kwa wakati.

*(iv)* Kamati inaitaka Wakala kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa usajili ya matukio ya kijamii na faida zake kwa maendeleo ya nchi yetu.

*(v)* Kamati inashauri Serikali kuwapatia Wakala fedha za matumizi kwa wakati na kwa kuzingatia maombi yao ili kutekeleza malengo ya kazi zao.

*(vi)* Mwisho, Kamati inawaagiza watendaji wa Wakala kufanyakazi kwa uadilifu, busara na mashirikiano makubwa ili kutoa huduma zilizobora zaidi.

# SEHEMU YA TATU

---

## 7.0 MAAGIZO MAAGIZO YA JUMLA YA KAMATI NA HITIMSHO

Katika sehemu ya Tatu, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa itaelezea Maagizo ya jumla ambayo yatajumuisha hoja kuu zilizoibuliwa na kamati kwa kila taasisi husika. Aidha, sehemu hii imebeba hitimisho la ripoti kwa Wizara tano zilizo chini ya Kamati hii kama ifuatavyo: -

**MAAGIZO YA JUMLA**

Kwa mwaka 2024/2025 katika ufuatiliaji wa taarifa za utekelezaji za wizara na taasisi zake ambazo kamati inazisimamia Kamati imeridhishwa na utendaji wa Taasisi hizo kutokana na juhudi kubwa wanazochukua pamoja na kutekeleza majukumu yao kwa kufuata miongozo na taratibu za kisheria. Hivyo basi, Kamati pia inatoa maagizo ya jumla kwa taasisi hizo kama ifuatavyo:

**Ofisi ya Rais Ikulu**

*(a)* Kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya ujenzi wa jengo jipya la makao makuu ya taasisi ya nyaraka katika eneo la Kilimani ili kukamilika kwa wakati na kuondosha changamoto ya uhaba wa nafasi kwa watendaji.

*(b)* Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufanya juhudi za makusudi za kununua nyumba zilizopo pembezoni mwa jengo hilo ili kupata nafasi ya kujenga maegesho ya gari kwa ajili ya huduma za ofisi.

*(c)* Kamati pia, inaendelea kuishauri Serikali kuzidisha kasi ya kutafuta eneo jipya na la kutosha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi mpya ya Nyaraka kisiwani Pemba.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais**

*(i)* Kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya kutoa elimu kwa jamii juu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuacha ukataji wa miti kiholela, kuchafua mazingira na kupelekea ukame wa mvua na mazao lengo likiwa ni na kuimarisha uhifadhi wa mazingira katika visiwa vyetu.

*(ii)* Ofisi kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya kwa kushirikiana na Taasisi na wadau mbalimbali iendelee kuelimisha Jamii juu ya athari za madawa ya kulevya inavyoteketeza vijana ambao ni nguvu kazi yaTaifa, kuwa na ujasiri na kuondosha muhali katika kutoa mashirikiano na Serikali, aidha, kamati inaishauri Serikali kupitia mamlaka ya dawa za kulevya kuanzisha idara maalumu ndani ya mahakama ambayo itashughulikia kesi za dawa za kulevya.

*(iii)* Kamati inaigiza Serikali kutafuta vyanzo vipya vya kifedha kwa lengo la kusaidia Tume ya UKIMWI Zanzibar kupata fedha za uhakika kwani uwepo wa vyanzo hivyo kutaisaidia Tume kutotegemea michango ya wahisani kutoka nje.

*(iv)* Kutokana na uwepo wa taasisi zenye kutoa mikopo ya kifedha kwa ajili ya vikundi vya watu wenye ulemavu, kamati inashauri Serikali kuzielekeza taasisi hizo kuregeza masharti ya mikopo kwa watu wenye ulemavu ili kuweza kutoa mikopo kwa mtu mmoja mmoja kulingana na aina ya ulemavu alionao kwasababu ni vigumu katika nchi yetu kupata kikundi cha watu 10 au zaidi wenye ulemavu wa aina moja katika eneo moja ambao watakua na aina moja ya ulemavu.

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

*(a)* Kwa kuwa lengo la Serikali ni kutoa huduma bora kwa wananchi wake na kuwapunguzia ukali wa maisha, kamati inashauri Serikali kufuatilia na kusimamia kikamilifu taasisi za umma zenye kutoa huduma kwa jamii ili kwenda sambamba na juhudi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

*(b)* Kamati inashauri afisi ya Baraza la Wawakilishi kuongeza kasi ya taratibu za ujenzi wa jengo jipya ndani yam waka huu wa fedha ili kuondoa changamoto ya ufinyu wa nafasi kwa michoro kwa ajili ya ujenzi huo imeshakamilika na kusubiri taratibu nyengine za kisheria ziweze kukamilika.

*(c)* Kupitia mradi wa Kunusuru Kaya Masikini Tanzaia, Kamati inazipongeza Serikali zetu mbili ambazo ni SMZ na SMT kwa namna zinavyoshirikiana kuendesha mradi huu ambao umekuwa na maslahi makubwa kwa wananchi wetu. Shukran za pekee ziende kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Samia Suluhu Hassan na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Hussein Ali Mwinyi pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa TASAF ndugu Shedrack Mzirai kwa namna wanavyoendesha mradi huu kwa mafanikio makubwa.

*(a)* Kama tunavyofahamu kuwa awamu ya tatu ya mradi wa TASAF imekamilika na maandalizi kwa ajili ya awamu nyengine ya mradi yanaendelea; kamati inawaomba wananchi kuwa watulivu na makini katika kuendeleza miradi yao midogo midogo ambayo waliibua kipindi kilichomalizika ili kutafakari miradi mipya ambayo itatekelezwa katika awamu mpya inayokuja.

**Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora**

(a) Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa Ofisi hii kwa kusimamia vyema majukumu yake na kutoa miongozo kila inapostahiki juu

ya masuala ya sheria na utumishi. Kamati inaiagiza Ofisi kufuatilia na kusimamia watumishi wa umma kwa lengo la kutoa huduma zenye ufanisi na kufikia maendeleo endelevu.

(b) Kamati imeridhika na utendaji wa Taasisi za Dini katika kuhamasisha amani na utulivu kwa waumini na jamii iliyo wazunguka. Hata hivyo, Kamati inazishauri taasisi hizo kuzidisha kasi ya kusimamia na kutatua migogoro yote ya kidini kwa mujibu wa sheria za nchi na sharia za dini husika.

(c) Kutokana na sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana namba 2 ya mwaka 2007 kupitwa na wakati ambapo imepelekea kamisheni kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa kupata faida, Kamati inaiomba Serikali kuharakisha marekebisho ya Sheria hiyo ili iweze kukidhi haja ya kujiendesha kibiashara, kuongeza mapato yake na kusimamia vyema mambo ya mirathi katika jamii ya waislamu.

(d) Kwa upande wa Sekta ya Utumishi wa Umma, Kamati imeridhishwa na namna bora ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizi zinavyoendelea. Hata hivyo, kamati inaishauri Serikali kufanya juhudi za haraka za kuwatafutia mradi wa ujenzi wa ofisi ya kudumu Tume ya Utumishi Serikalini ili kuepusha kuhamahama kila siku kwenye majengo makongwe.

(e) Kamati wakati ikipokea taarifa za utekelezaji wa Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) tawi la Pemba ilipata pia ya kutembelea eneo la kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa chuo. Hata hivyo, kamati haijaridhishwa na maendeleo ya mradi wa ujenzi huo kutokana na kuahidiwa mara kadhaa kuanza kwa ujenzi huo bila ya mafanikio yoyote hali ya kuwa kamati inaelezwa kuwa taratibu zote za awali zimeshakamilika. Kwa mnasaba huo, Kamati inaigiza Ofisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora kusimamia kikamilifu maendeleo ya ujenzi huu kwa kufuatilia

utaratibu unaendelea juu ya ujenzi wa chuo hiki kwa upande wa Pemba.

**Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ**

*(a)* Kamati inaipongeza wizara kwa namna inavyosimamia majukumu yake ya kulinda amani na usalama wa nchi yetu kupitia Idara Maalum za SMZ. Aidha, kamati inaziagiza idara maalumu zinazozalisha kujipambanua katika uzalishaji kwa kuzitangaza bidhaa zao kila wanapopata nafasi ya kufanya hivyo.

*(b)* Aidha, kamati inaziagiza idara za Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) na Chuo cha Mafunzo (MF) kuendelea na mradi wa kilimo cha miwa kwa gharama zao wenyewe kuanzia hatua za mwanzo hadi mavuno na kuuza kama bidhaa yake bila kushirikisha wawekezaji ambao wamekuwa wakikosesha mapato kwa visingio mbali mbali.

*(c)* Kamati pia, inaigiza wizara kufuatilia taasisi za umma na binafsi ambazo zinadaiwa na Wakala wa ulinzi wa JKU ili kufanya mchakato wa malipo kwa mujibu wa mikataba yao na endapo itashindikana kulipa; kamati inaiomba Serikali kwa zile taasisi za umma kuchukulia hatua kwa kulipa deni hilo kupitia fedha zao za matumizi ya kawaida (OC).

*(d)* Kamati inaigiza Ofisi hii kuweka kipaumbele katika kutoa elimu kwa wafanyabiashara wadogo wadogo kupitia Serikali za Mitaa ili kupata jamii ya wafanya biashara wenye uzalendo wa kulipa ada na tozo kupitia maeneo yao ya uzalishaji.

*(e)* Kamati inaziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha wamezidisha nguvu ya kufanya usafi kutokana na maeneo ya mji kuwa machafu na kutoridhisha kwa wakaazi wa mji. Aidha, kamati inaziagiza Halmashauri na mabaraza ya manispaa kutafuta kampuni za wawekezaji wazalendo ambao

watakubaliana kimkataba kuendesha zoezi la usafi katika maeneo yao na kuwaongezea chanzo cha mapato.

*(f)* Kamati pia, haikuridhishwa na hali ya usafi wa Baraza la Manispaa Magharibi 'B' kutokana na kuongezeka kwa kiwango kikubwa cha taka na kupelekea kufanyika majaa yasiyo ya lazima. Aidha, kamati hairidhishwi na ujenzi holela ambao unafanyika katika manispaa hii kutokana na watu kujenga bila kuzingatia taratibu za kisheria na mipango miji. Hivyo, kamati inaigiza wizara kufuatilia kwa karibu maendeleo ya manispaa hii na kutoa miongozo ya mara kwa mara dhidi ya uendeshaji uliobora ili kulinda haki na fursa za wananchi.

*(g)* Sambamba na hayo, kamati inaliagiza Baraza la Manispaa ya Kaskazini 'A' kukaa pamoja na wawekezaji wa kampuni za usafi kwa lengo la kutafuta suluhu ya kudumu kwenye mikataba yao na endapo wawekezaji watakataa kufanya hivyo, basi Baraza litafute wawekezaji wengine wazalendo wenye kufuata matakwa ya Baraza.

*(h)* Aidha, Kamati haikuridhishwa na baadhi ya wawekezaji wazalendo wa kampuni za usafi kwenda kinyume na mikataba yao na Manispaa hali inayopelekea kukosekana kwa mapato. Hivyo, kamati inaziagiza kampuni zote za usafi yenye madeni na Mabaraza ya Manispaa kulipa madeni yao kwa haraka na kwa kufuata makubaliano ya mkataba waliofunga na Halmashauri husika.

*(i)* Vile vile, kamati inaziagiza Serikali za Mitaa kusimamia kikamilifu vyanzo vyake vya mapato bila ya kufanya muhali kupitia sheria na kanuni ndogo ndogo ambazo wanazitunga ili kuwa na uendeshaji bora wa maeneo yao.

*(j)* Kamati pia, inaigiza wizara kusaidia upatikanaji wa vifaa vya usafi na ukusanyaji wa mapato ili kufanya kazi kisasa kwa mabaraza yetu kutokana na changamoto ya uhaba wa fedha ambao unawakabili.

(k) Kamati imeridhwa na utekelezaji wa Afisi ya Mrajisi wa Taasisi zisizo za kiserikali kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Kamati inaishauri afisi hii kuzidisha kasi ya kufuatilia na kusajili jumuiya mpya ambazo zitaleta tija kwa jamii na nchi kwa ujumla.

## 8.0 HITIMISHO

Katika kukamilisha kazi hii, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa haina budi kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kusimamia vyema sera na mipango ya Serikali katika utekelezaji wa shughuli zake za kuwaletea wananchi maendeleo ambao ni msingi mkuu wa utawala wake na kwa kutimiza malengo hayo wananchi wa Zanzibar wameendelea kumuamini na kumchagua tena kugombea nafasi ya urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi katika uchaguzi mkuu wa 2025.

Kwa upande mwengine, Kamati inatoa shukurani zake za dhati kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ndugu Raya Issa Msellem, Mratibu wa Kamati pamoja na wanasheria wetu wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa msaada wao mkubwa ambao wamekuwa wakiipatia Kamati hii wakati wa utekelezaji wa majukumu ya upitiaji wa Miswada ya sheria.

Aidha, pongezi maalum ziende kwa upande wa uongozi na watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba, watendaji wa Afisi ya Rais Ikulu; watendaji wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora; watendaji wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ; watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais; watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais,

Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi; pamoja na Afisi kuu ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii. Kwa pamoja tunasema AHSANTENI SANA.